ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tisa – Tarehe 27 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 122

Utumiaji Mbaya wa Misaada Tunayopewa na Wafadhili

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Kny: Mhe. Panya Ali Abdalla) – Aliuliza:-

Ni miaka sita sasa tangu ndugu zetu wa UNDP kutupatia msaada wa choo cha *flash* cha dawa za Kulevya ambacho kilitegemewa kufungwa Uwanja wa Ndege Unguja, ambapo panafikiriwa kuwa ni kitovu kikubwa cha kuingizia na kusafirishia dawa za kulevya. Hata hivyo, mpaka sasa hakijafungwa.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kuchelewa kufungwa choo hicho?
(b) Je, hatuoni kama kuchelewa kwetu huko tunawavunja moyo Washirika hao wa Maendeleo?
(c) Je, ni lini choo hicho kitafungwa?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 122 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, suala la kuchelewa kukamilishwa choo ambacho kingesaidia katika shughuli za kupambana na dawa za kulevya katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ni suala la muda mrefu, na nimewahi kujibu maswali zaidi ya mawili kuhusiana na suala hilo.

Ofisi yangu kwa kuona umuhimu wa kuwepo choo kile katika kusaidia shughuli nzima ya kupambana na dawa za kulevya, ilifanya juhudi zote za kuhakikisha kwamba choo hicho kinamalizwa haraka, ili kiweze kufanya shughuli zake na kisaidie mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iliiandikia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo ndiyo inayosimamia shughuli zote za serikali kuitaka izungumze na Jeshi la Polisi, ili kukamilisha choo hicho kwa sababu wao ndio wenye dhamana hiyo.

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa bahati nzuri sana tokea tarehe 15/03/2012 imeiandikia Jesho la Polisi kutaka iipatie makisio ya vifaa ambavyo vinahitajika, ili choo hicho kikamilishwe. Kwa bahati mbaya sana ofisi hii bado haijapokea jibu kutoka Jeshi la Polisi.

Kwa hivyo, niendelee tu kusema kwamba serikali itaendelea kulifuatilia kuona kwamba choo hiki kinakamilika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri wakati wa majibu yake amesema swali hili amekuwa akiulizwa kila wakati na kutoa majibu.

(a) Je, kuulizwa huku kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawaridhishwi na utekelezaji wa jambo hilo.

(b) Kwa kuwa serikali inafanya kazi kama *collective responsibility*, je Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inasemaje juu ya jambo hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli na naomba nimhakikishie kwamba hata ofisi yangu hairidhiki na kuona kwamba choo hicho hakijakamilishwa.

Kutokana na hali hiyo, ndipo jitihada za makusudi zikachukuliwa na ofisi yangu kuiandikia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha kwamba inalitaka Jeshi la Polisi liweze kuhakikisha kwamba choo hicho kinakamilishwa. Hatua hiyo kwangu imekamilika zamani sana, lakini kwa bahati mbaya ushirikiano tulioupata kwa ndugu zetu wa Jeshi la Polisi sio mzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais naomba niongezee jibu la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli hakuna atakayeridhika kwa kuona kwamba choo kile cha *Airport* mpaka leo bado hakijakamilika. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha hasa ukitilia maanani tatizo gumu liliopo mbele yetu la kupambana na dawa za kulevya.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba tuliombe Baraza lako tukufu hili, liendelee kutustahamilia na sisi tuchukue hatua nyengine za kidharura ambazo kwa kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba Jeshi la Polisi liweze kutuletea hayo makadirio yanayotakiwa, na choo kile kiweze kufungwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Pamoja na majibu yasiyoridhisha yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawarizi wote wawili napenda kuwauliza swali la nyongeza.

Kwa mujibu wa kilipo kile choo, kwanza hawaoni kwamba si usalama kukifunga mule na ikawa wengine wanageuza ni sehemu ya kufichia mambo yao, kwa sababu sasa tumepata Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na pale choo kilipo ni kichochoro ambacho wengine wanaweza kufichia mambo yao tulipokwenda.

(a) Kwa usalama wa Uwanja wa Ndege haoni kukibakisha choo kile katika hiyo sehemu iliyo ni kuhatarisha usalama wa ule Uwanja wa Ndege.

(b) Kwa kuwa kile choo kililetwa au kilitolewa msaada kwa ajili ya kufuatilia dawa za kulevya, na wala haijatoka ripoti yoyote kwamba dawa za kulevya haziingii tena Zanzibar. Je, serikali haioni kwamba ndio inayosaidia kuleta dawa za kulevya?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kuhusiana na sehemu ambayo choo hicho kipo. Napenda nimhakikishie Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwa jumla kwamba, mazungumzo ya kina yalifanyika kati ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Anga kuona ni eneo gani choo kile kiwepo na ikakubalika kiwepo hapo.

Kwa hivyo, ni imani yetu kwamba Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinakiweka Kiwanja chetu cha Ndege katika usalama wa hali ya juu na wala hakitaruhusu masuala mengine yoyote ya kuficha vitu vibaya kama vile dawa za kulevya au vitu vyengine, kwa sababu usalama wa kiwanja chetu cha ndege ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusiana na swali la pili naomba nirejee tena kwamba kutokuwepo kwa choo kile hakujakwamisha sana au kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kazi ya choo kile inafanywa kwa kutumia njia mbadala katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa hivyo shughuli ambazo zinatakiwa kufanywa pale zinafanywa katika njia mbadala.

Nam. 197

Posho kwa Madereva wa Viongozi

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa Waraka maalum unaoelekeza kulipwa kwa nyongeza za posho kwa madereva na masekretari wa viongozi.

(a) Ni tatizo gani lililopelekea baadhi ya watumishi hao wakiwemo madereva wa Meya wa Manispaa ya Zanzibar kutolipwa posho hizo?

(b) Ofisi yako inachukua hatua gani kurekebisha hali hiyo, ili kuhakikisha wanaostahili kulipwa nyongeza hiyo kwa wakati?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 197 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kukubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa toleo linaloelekeza kulipwa posho madereva na masekretari wa viongozi katika viwango mbali mbali.

(a) Baraza la Manispaa ni miongoni mwa taasisi zinazopewa ruzuku na serikali, suala la kulipa posho lipo ndani ya uwezo wa Baraza hilo kwa kuzingatia Toleo la Serikali. Hata hivyo, kwa taarifa niliyonayo dereva wa Meya tayari ameshaanza kulipwa posho lake kuanzia mwezi wa Mei, 2012.
(b) Katika kurekebisha hali hiyo, ofisi yangu huwasiliana na taasisi husika kila tunapopokea malalamiko ya kutolipwa posho, ili wanaostahili kulipwa posho walipwe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Serikali imeweka utaratibu wa kuwalipa posho madereva wa viongozi na ikasahau wale viongozi wa madereva (*TO*), ambapo wakati mwengine madereva wa viongozi wasipokuwepo huwa wao wanachukua nafasi ya kuwaendesha viongozi hao.

Je, Wizara yake itafanya utaratibu gani kuhakikisha na *Transport Officers (TO)* nao wanalipwa posho, almuradi na wao wanafanya kazi shughuli zile za viongozi baadhi ya wakati?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli wakati tunaandaa utaratibu wa kulipa posho kwa madereva wa viongozi tuliwasahau *Transport Officers (TO)*. Kwa maana hiyo, katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ofisi yangu itahakikisha kwamba nao wanatengenezewa utaratibu wa kuweza kupata posho. *(Makofi)*

Nam. 111

Tatizo la Maji Jimbo la Matemwe

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Kuna tatizo kubwa la maji kwenye Jimbo la Matemwe kutokana na kisima kidogo kilichopo Kiashangwe. Kwa kuwa kisima hiki hivi sasa hakina uwezo wa kusambaza maji kwenye shehia mbili za Matemwe, yaani baina ya Shehia ya Kigomeni na Shehia ya Matemwe Juu kutokana na udogo wa mashine.

(a) Je, Mhe. Waziri ni lini serikali itawapatia wananchi mashine kubwa na kuweza kuwaondolea tatizo hili la maji?

(b) Ni sababu zipi zinazofanya mashine hii iungue mara kwa mara?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 111 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naomba nitoe ufafanuzi kwamba uingizwaji wa *pump* kwenye kisima siku zote inategemea uwezo wa kisima chenyewe, na inapotokezea kuungua kwa *pump* basi mafundi wetu hufunga *pump* nyengine inayoendana na kisima hicho, ili kuwapatia wananchi huduma hiyo ya maji safi na salama.

Kwa sasa kisima hicho kilichopo Kiashangwe ambacho kinapeleka maji Matemwe tayari kimeshafungwa *pump* ambayo inayoendana na kisima hicho, na wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Sababu hasa zinazopelekea kuungua kwa mashine ni hitilafu za umeme, ikiwemo umeme mdogo katika eneo hilo. Mhe. Spika, tayari *ZAWA* na Shirika la Umeme kwa pamoja inategemea kulishughulikia tatizo hilo na kuwaondoshea usumbufu wananchi wa eneo hilo.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante pamoja majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kuna Dokezo kutoka kwa Msaidizi Kitengo cha Utafiti na Maendeleo la tarehe 15 Februari, 2012 linaloelezea uunguaji wa mashine ovyo katika Mamlaka ya Maji na hususan Zanzibar.

Je, Mhe. Naibu Waziri katika Dokezo hili la Mtafiti wizara yako imelifanyia kazi namna gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, uunguaji wa *pump* kwanza kama nilivyoeleza unasababishwa na hitilafu za umeme. Lakini kama kuna kitengo ambacho kimechunguza na kuona kwamba mashine zinazoletwa si za uhakika, basi taarifa hiyo mimi mwenyewe sina.

Kwa hivyo, ningewaomba hiki kitengo kilichochunguza basi tukutane mimi na wao na tulizungumze suala hili na baadae tuweze kulitafutia njia ya kuliweka sawa.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Wakati alipokuwa akijibu Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba tatizo hilo tayari limeshatatuka kwa kijiji cha Kigomani hadi Matemwe Juu.

Lakini kuna taarifa Mhe. Naibu Waziri ulizozileta hapa si za kweli, kwa sababu maji yalitoka muda wa siku mbili tu na hadi sasa maji hayatoki.

Je, Mhe. Waziri unawaambia nini wananchi hao wa Jimbo la Matemwe.

Vile vile kuna vijiji vyengine kama vile Kijini, Mbuyu Mtende bado hawajapata maji safi na salama.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwatatulia tatizo hilo wananchi hao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, inawezekana kwamba nguvu ya maji imepungua kwa baadhi ya maeneo, lakini hilo niseme ni suala la kawaida, kwa sababu wakati tunapofunga *pump* tunafunga *pump* zenye kiwango na zinakuwa na nguvu katika kipindi cha mwanzo. Lakini kutokana na ongezeko la matumizi, basi nguvu hiyo huwa inapungua na husababisha baadhi ya maeneo huduma hiyo isifike.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia wananchi kwamba huduma hiyo wataipata vizuri, kwa sababu tayari tumeshaongeza kisima chengine kipya kwenye maeneo ya Kiashangwe ambacho tunakielekeza maeneo ya Matemwe pamoja na sehemu nyengine. *(Makofi)*

Vile vile tunao mradi ambao tumesaidia tarehe 31 Mei, 2012 Mradi wa *ADB*, ambao utaanza shughuli zake rasmi za ujengaji katika kipindi hiki kifupi ambao utapeleka maji Matemwe, Nungwi kwa Kaskazini pamoja na Pwani Mchangani. Kwa hivyo, naomba niwatoe wananchi wasi wasi na kwamba serikali yao suala hili inalishughulikia, na wote watafaidika na huduma hiyo ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali mama alisema kwamba, suala linalosababisha *pump* hizo kuungua mara kwa mara ni suala la umeme mdogo ndilo linalosababisha hivyo.
Kwa kuwa wananchi wanapata shida ya maji na pia wao tayari wameshakaa pamoja na Shirika la Umeme (*ZECO)*.

Je, ni lini hasa watawaondolea wananchi dhiki hiyo ya umeme, kwa ajili ya kutatua tatizo hilo la umeme mdogo, ili wananchi wafaidike kwa sababu maji ni uhai na kwa kuwa wananchi wanapata sana shida ya maji?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme pamoja na Mamlaka ya Maji, tunategemea suala hili litapatiwa ufumbuzi karibuni sana, kwa sababu kuondoka kwa tatizo la umeme mdogo ni kufunga *line* nyengine mpya ambayo itakuwa na uwezo wa kuhifadhi *Mega Watt* 100, ambao kwa hivi sasa iko njiani na muda mdogo sana itafika Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafikiri wengi harakati hizi mnaziona, na kwa hivi sasa tayari tunafunga *line* kutoka Mtoni hadi Fumba, ingawaje kuna matatizo kati ya shirika langu na wananchi. Kwa mfano, jana tulikuwa na mzozo mzito maeneo ya Darajabovu, ambapo wananchi walikuwa wanazuia baadhi ya maeneo isipite hii *line* ambayo inapeleka umeme Mtoni pale.

Lakini pamoja na hayo, Shirika pamoja na serikali kwa jumla imelisimamia suala hili, tukijaaliwa baada ya muda mdogo meli ambayo inayoleta *cable* hiyo itafika Dar-es-Salaam, na tunategemea kufunga line hiyo. Kwa hivyo, tatizo hili si kwa visima vya maji tu mpaka wale wananchi wanaotumia ndani ya nyumba zao basi litaondoka kabisa. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 –
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuruni kabla sijamuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuja kuanza kutoa majumuisho, kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Naomba niwaombe radhi Waheshimiwa Wajumbe, kwa siku kama tatu hivi mfululizo sikuwa pamoja nanyi katika shughuli zetu za Baraza, hali yangu haikuwa nzuri. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametupa nafuu na leo kumudu kuja kushirikiana na nyinyi katika shughuli zetu. *(Makofi)*

Kwa kweli nilikuwa nanyimika sana kwa kutopata nafasi ya kuwa na nyinyi kuendelea na shughuli zetu, lakini hali ilikuwa hainiruhusu kuja. Kwa hivyo, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote, kwamba mlishirikiana na wasaidizi wangu Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti pamoja na watendaji wa Baraza kuendesha shughuli hizi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wakati mkiendelea na shughuli basi mimi moyo wangu imani na maarifa yangu yote yalikuwa huku, ili kuona na kumuomba Mwenyezi Mungu shughuli zetu ziwe zinakwenda vizuri kwa manufaa ya wananchi wetu.

Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba sikupata taarifa ya kwamba kulikuwa na mashirikiano mabaya katika kuendesha shughuli zetu kwa kipindi chote hicho. *(Makofi)*
Kwa hivyo, sina budi kukushukuruni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwaafikisha nyinyi mkashirikiana kiasi hivyo. Hivyo, nawaomba tuendelee na mashirikiano haya kwa muda wote wa shughuli zetu, ili tufanikishe masuala na majukumu ya wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, tulionjwa kidogo, lakini tunashukuru kwamba tumerudi tena katika shughuli zetu. Kwa hiyo, nakuombeni tuendelee na mashirikiano, ili ratiba ya shughuli zetu ambayo imetetereka kidogo tu, lakini kwa sababu ya kufanya vyema shughuli zetu, basi naamini huko mbele tutaweza kusawazisha, ili twende kwa mujibu wa ratiba na mambo yetu yamalizike kwa muda ambao tumeupanga.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ili naye atoe mchango wake kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhai na kutuwezesha tena kukutana katika Baraza lako tukufu tukiwa wenye afya.

Mhe. Spika, pia nichukua fursa hii kukuombea wewe ili uzidi kupata afya njema na uweze kutuongoza katika Baraza letu hili. Nikushukuru sana kwa namna ambavyo unaliongoza Baraza hili tukufu. Aidha nikuhakikishie kwamba yalikuwepo mashirikiano makubwa na wasaidizi wako uliowaachia katika kutuongoza katika Baraza hili akiwemo Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti na tulifanyakazi nao vizuri sana, tunawashukuru sana. Aidha niwashukuru sana, Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kwa namna walivyokuwa nasi na kuendelea kutupa michango yao ya kina kabisa.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kutoa maelezo yangu naomba pia nichukue fursa hii kuanza kumshukuru sana Makamo wa Pili wa Rais kwa namna anavyotuongoza Wizarani kwetu, hekma na busara zake ndio zilizotuwezesha kufikia hatua tuliyofikia.

Mhe. Spika, kwanza niseme na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pia nawaomba Wajumbe wenzangu wote waunge mkono hoja hii ili tukamilishe shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu Mhe. Makamo wa pili wa Rais atakuja hapa kutoa hoja na kueleza kwa kina zaidi, majibu mbali mbali yanayohusu Wizara yetu. Kwa hiyo Mhe. Spika, naomba kwanza niendelee kuwashukuru Wajumbe wako wote na hasa niishukuru Kamati ya Viongozi wa Kitaifa iliyochini ya Mwenyekiti wake Mhe. Hamza kwa namna walivyotupa mawazo mazuri na michango mizuri katika shughuli zetu. Pia nawashukuru waheshimiwa wajumbe wote waliochangia katika hoja hii.

Mhe. Spika, imeonesha wazi nia ya wajumbe wako kwa namna walivyokuwa tayari kuleta mabadiliko makubwa ya kuijenga Zanzibar. Waheshimiwa wameonesha nia njema na mapenzi makubwa kwa serikali yao. Wameonesha wazi kabisa imani yao kwa nchi yao na walivyotayari kuwatumikia wananchi wan chi hii na kutetea haki za Wazanzibari. Imeonesha uwezo mkubwa walionao wajumbe wa Baraza hili, hapana shaka hali hii itaisaidia Zanzibar kupiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo.

Niseme wazi Mhe. Spika, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeridhishwa sana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe na nataka kuchukua nafasi hii kusema tumeipokea kwa mikono miwili na tutaifanyia kazi kama maelekezo.

Aidha nichukue fursa hii Mhe. Spika, niwashukuru sana, wananchi wa Zanzibar kwa kuunda mkono serikali yao yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Imani yangu kubwa ya kuunga mkono serikali hii na kuiwezesha nchi yetu kuwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa, Mhe. Spika, hapana shaka inatubi sote tuwashukuru Waheshimiwa wananchi.

Mhe. Spika, nianze na hali ya siasa. Ukweli sikupendelea sana kujibizana na viongozi wa dini, sipendi kabisa kabisa Mhe. Spika. Nikiamini kwamba viongozi wa dini ndio sehemu kubwa ya uongozi wan chi yetu, busara zao na hekma zao zinahitajika sana katika kusaidia mchango wa kuendesha nchi yetu. Kutokana na *nature* ya kazi yangu na kutokana na yaliyotokea sina budi niyaeleze machache ili Baraza lako tukufu na wananchi wa Zanzibar waelewe hali halisi inavyoendelea katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza niseme mimi pamoja na wengi humu ndani tumekuja tumeukuta Muungano ulikuwepo leo. Mimi pamoja na wengi waliokuwemo humu ndani muungano huu ulipoanzishwa tulikuwa na umri mdogo sana,

kwa hivyo tumekuja na tukaukuta. Kwa maana hiyo muungano huu tumeukuta ukiwa na katiba na sheria na sisi kama viongozi tumeapa mbele ya Baraza lako tukufu kwamba tutalinda na kutetea Katiba na Sheria za nchi hii.
Mhe. Spika, tulishika mas-hafu matukufu katika kufanya hivyo. Kwa hivyo ni wajibu wetu kuwa wakweli, kuwa waadilifu na kueleza hali halisi iliyopo katika nchi yetu. Mhe. Spika, kulijitokeza sana katika Baraza lako tukufu katika michango kuonesha kama kwamba serikali ilikuwa na niya ya kuwabana baadhi ya wananchi, hasa hasa Kikundi cha Uamsho na Washirika wake wasiweze kutoa maoni katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hali haikuwa hivyo, serikali hata siku moja haikatazi kwa wananchi wake kutoa maoni yao. Ni nia ya serikali kabisa kupata maoni ya wananchi wake, tulichosema ni kwamba Sheria na taratibu za nchi zifuatwe. Maana kutokufuata sheria na kutokufuta taratibu za nchi matokeo yake nchi inaingia vurugu na matatizo makubwa. Na hilo ndio kitu ambacho hatungependa kitokee katika nchi yetu.

Hasa tukitilia maanani kwamba rasilimali kubwa ya Wazanzibari ni amani na utulivu wan chi yetu. Na hasa ukipima kwamba uchumi wa nchi hii unategemea sana suala la utalii ambao kwa kiasi kikubwa unategemea amani na utulivu. Siku zote tulikuwa tunayasema haya msingi wake nchi yetu ikae katika hali ya amani na ikae katika hali ya utulivu, ili tuendelee kuimarisha uchumi wetu na tuweze kupiga hatua ya kimaendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo hatukuwa na nia hata siku moja, kunyima watu wasitoe mawazo yao, ama kumuonea mtu mwengine. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba hali ya amani na utulivu katika nchi yetu inaimarika.

Mhe. Spika, siku ile ya tarehe 26/5/2012 nini kilitokea? Mhe. Spika, ndugu zetu hawa walikuwa na mkutano pale Lumumba na mkutano huo maarufu ulijulikana kama Baraza la Wasomi. Mkutano ule uliendelea kama kawaida yake yakasemwa yaliyosemwa, lakini baada ya kumaliza mkutano Mhe. Spika, kitu cha kushangaza ni pale mmoja katika kiongozi alipouliza. Je, kuna mtu yeyote anaweza kutuzuia kufanya lolote katika nchi hii? Wafuasi wakajibu hakuna. Je, kuna mtu yeyote anaweza kutuzuia tusifanye maandamamo? Wafuasi wakasema hakuna. Baada ya hapo ndipo yalipofanyika maandamano wakaingia mitaani ambayo hayakuwa na kibali rasmi cha serikali.

Kutokana na hali hiyo ndio polisi baadaye ikabidi iwatafute viongozi wale ili wasaidie polisi katika kupata taarifa kamilifu ya yaliyotokea na ndiyo wakamkamata Shekhe Mussa Juma, na kumpeleka kituo cha Madema. Katika kumchukua kumpeleka kituo cha polisi na kuendelea na uchunguzi wa polisi ndipo ilipotokea baadhi ya kundi la vijana kwenda kituo cha polisi na kuwataka polisi wamuachie mara moja huyu Shekhe. Polisi wakawaomba vijana wale kwamba tuachieni tufanye kazi yetu na kwa vyovyote mtapata taarifa za maendeleo ya uchunguzi tunaofanya baada ya kwisha kuchukua taarifa kwa ukamilifu wake.

Mhe. Spika, ndio baada ya hapo vijana wale wakaambizana na kupelekeana jumbe mbali mbali ili wakusanyike kwa nia ya kutumia nguvu na waweze kumtoa Shekhe kutoka kituo cha Madema. Kutokana na kadhia hiyo ndio maana Polisi walichukua hatua ya kuzuia kundi hilo la vijana wasiende pale kituo cha Madema kumtoa kwa nguvu huyu Shekhe.

Kwa kawaida ya kazi ya Polisi Mhe. Spika, unapofikia hatua kama hiyo kwa njia moja au nyengine unasababisha vurugu. Ndipo Polisi walipochukua hatua ya kupiga mabomu ya machozi. Lakini cha kushangaza Mhe. Spika, wakati vurumai ile ikiendelea vijana hawa walikuwa na matairi mengi ya magari, wakayachoma barabarani, wakayawasha moto, wakaweka mawe makubwa, magogo na kadhalika ili kuzifanya barabara hizo zisipitike. Kwa kawaida mji wa Unguja Mhe. Spika, kuona matairi mengi ya namna ile unastaajabu kwa muda ule waliyapata vipi au walikuwa na mpango gani hata ikatokea vile.

Mhe. Spika, kutokana na kadhia ile na mabumu yale, ukweli yaliathiri wananchi wengi na wananchi wengi walitulalamikia, lakini ilikuwa hakuna njia nyengine isipokuwa ililazimika polisi kutawanya kundi lile na kuwaondoa ili wasifanye fujo. Iliwachukua karibu siku mbili mpaka kumaliza tatizo lenyewe. Hiyo ndiyo hali halisi iliyotokea Mhe. Spika.

Sisi kabla ya hapo kama serikali tulichukua hatua mbali mbali ya kuwaonya na kuzungumza nao. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alizungumza na Jumuia hii, wakakubaliana vizuri, lakini baadaye wakaendelea kufanya yale yale ambayo yalikuwa kwa njia moja au nyengine yanachochea kutokea fujo. Baadaye Mwanasheria Mkuu alizungumza nao, Kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi iliundwa tukazungumza nao, Mashekhe, Mufti Mkuu, Kadhii Mkuu na Mashekhe wengine walizungumza nao. Wote walizungumza nao ili kuwaonya na kuwambia kwamba nchi ni kitu muhimu ikikaa katika hali ya utulivu na kufuata sheria. Lakini juu ya yote hayo Mhe. Spika, bado Kikundi hichi

kiliendelea kufanya vile ambavyo kiliona wenyewe wafanye. Hata serikali ilipotoa tamko bado kikundi hichi kiliendelea. Kwa hiyo uwamuzi ule wa Polisi umekuja baada ya kuzungumza nao kwa muda mrefu.

Kwa hivyo nataka kuwaomba Waheshimiwa wenzangu waijue hali halisi iliyotokea. Lakini kwa bahati nzuri sasa kikundi hichi kimekubali kufuata sheria za nchi na kimekubwali kutoa maoni yake. Kwa kweli tokea walipotoa tamko lile mpaka leo nchi imekaa kwa utulivu mkubwa sana. Nataka niwashukuru wale wote waliochangia na waliochukua jitihada za kuzungumza nao na mashekhe wenyewe kufikia kuamua jambo hili.

Kama nilivyosema Mhe. Spika, sijambo zuri kwa sisi wanasiasa kabisa kabisa kujibizana na Mashekhe wetu ambao tungetegemea tunapopata matatizo wao ndio watupe fat-wa, ndio watuelekeze, wao ndio watusimamie ili tukae katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Nawaomba sana wananchi wote wa Zanzibar, tusameheyane yaliyopita yamepita, sasa tujenge Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, kuhusu sheria ya Tume ya Katiba. Mheshimiwa kwa mara ya kwanza kabisa katika sheria ambayo Zanzibar imeshirikishwa kwa ukamilifu wake ni sheria hii. Tulishirikiana vizuri sana na wenzetu wa upande wa Jamuhuri ya Muungano. Kila hatua ambayo ilifikiwa tuliifikia kwa pamoja. Ndio maana Mhe. Spika, sheria ile inauwakilishi sawa kati ya Zanzibar na upande wa Tanzania Bara. Wale wajumbe 30 wa Tume walioteuliwa 15 kutoka Zanzibara na 15 ni kutoka Tanzania Bara. Hii inaonesha wazi kwamba utaratibu wote utakaoshughulikia katika kupata maoni utakuwa ni wahaki na wa wazi. Tutahakikisha kwamba mambo haya yanakwenda kama yalivyo matarajio ya wananchi.

Kwa sasa Tume ile itaanza na mikoa minane, Mikoa sita kwa upande wa Tanzania Bara na Mikoa miwili kwa upande wa Zanzibar, tutaanza Mkoa wa Kusini Pemba na Kusini Unguja. Kutakuwa na Makamishna wanne na katika Makamishna wanne hao wawili watatoka Zanzibar na wawili watatoka Tanzania Bara. Vile vile kutakuwa na Wajumbe wa Sekretarieti wawili, mmoja kutoka Zanzibar na mmoja kutoka Bara. Vile vile na wataalamu wa IT wawili, mmoja kutoka Zanzibar na mmoja kutoka Bara.

Kwa hivyo utaratibu mzima utakwenda katika njia za haki na njia za kuwasikiliza wananchi kile wanachokisema. Nawaomba Wazanzibar wenzangu, hii ni fursa pekee na ni fursa adhimu kwa nchi yetu, kwenda tukatoe maoni yetu. Tena tuyaeleze yale yote bila ya kuyaonea haya, kila tatizo tuliseme na kila pendekezo tunaloliona linafaa kulitoa kwa nchi yetu tulitoe ili tufikie maoni mazuri.

Nataka niwahakikishie waheshimiwa kwamba hakutokuwa na mazingaombwe yeyote isipokuwa kitakachofanyika ni yale maoni ya wananchi yataheshimiwa. Cha msingi sisi wenye tuvumiliane sana, maana katika kuvumiliana ndipo tutakapopata kutoa maoni yetu kwa nafasi na kwa furaha bila ya woga.

Serikali haitopenda kutoa msimamo kwenye hili, uwamuzi wa serikali ni kusikiliza maoni ya wananchi wenyewe. Wananchi wenyewe waunde Katiba yao wanayoitaka. Wananchi wenyewe ndio wawe waamuzi wa mambo yao wanayoyataka. Wananchi wenyewe ndio watuelekeze nini wanakitaka. Serikali kazi yake imeunda ile Tume iratibu na ikusanye maoni ya wananchi.

Nataka niwahakikishie kwamba Tume ile kwenye kukusanya na kuratibu haimalizi kazi , wao kazi yako watakusanya, wataratibu, baada ya hapo tutakwenda kwenye Bunge la Katiba. Wajumbe wa Baraza hili tukufu ni miongoni mwa wabunge wa Katiba. Mimi naamini kwa umakini huu hawatokubali kuona yapo maoni yalitolewa na Wazanzibar na wasiyaseme kwamba haya hayakutolewa. Umahiri na ubingwa wa Baraza hili naamini kila lililotolewa kwa maslahi ya Zanzibar watalitetea ndani ya Bunge la Katiba na mambo hayahishii hapo, hata baada ya Bunge la Katiba kupitisha hiyo rasimu ya awali bado.

Wananchi ndio watakaokuwa waamuzi wa mwisho, Kutakuwa na kura ya maoni kwahivyo wakiona Katiba ile hawaitaki na sio yale waliyoyasema wataikataa na hakuna atakayewakataza kuikataa. Kwa hivyo maoni ya wananchi ndio silaha na ndio dira itakayofanya tuwe na katiba itakayotufaa sisi, vizazi vyetu na taifa letu. Kwa hivyo tuwe makini katika kujenga hoja. Hapa tuache jazba, tuache kutuhumiana, tuache kulazimishana, hapa tujenge hoja za msingi zitakazoleta maslahi kwa nchi yetu, zitakazokidhi matarajio ya watu wetu. Chamsingi hapa tuwe wamoja na tusibaguane.

Jana ndugu yangu Mhe. Subeti alisema sana suala la kubaguana wenyewe kwa wenyewe. Hili si jambo zuri na wala si vizuri kabisa kuanza kuandika vikaratasi vya kuchochea, vikaratasi vya kubaguana, vikaratasi vya kuanza kuhasimiana hili si jambo zuri. Wazanzibari niwamoja, sisi ni ndugu moja wala hakuna tarehe iliyoanzishwa Pemba na Unguja. Hii ni asili na asili nchi hizi ni moja kwa hivyo tusifikishane huko, haina haja kabisa kupandisha chuki, haina haja kabisa kupandikiza hasama, haina haja kabisa kupandikiza jazba cha msingi tutoe maoni kwa uhuru, haki na vile unavyoona inafaa.

Mola ni muweza ni mjuzi, atatusaidia tuvuke kwa salama katika kipindi hichi, hichi ni kipindi cha mpito. Mwenzangu mmoja alisema jana cheche ndogo hapa ikiruka inaweza kuzaa hatari kubwa sana. La msingi ni subra na kuvumiliana ili tufikie maamuzi vizuri, tuelekee kuzuri, tupate hatma njema na kuanzia sasa haina haja ya kukashifiana, kuchenjeguana na kusema maneno yaliyokuwa sio. Kwa sababu hatutopata mustakbali mwema wa nchii yetu.

Mhe. Spika, kuhusu Muungano. Mhe. Spika, muungano unatokana na nchi mbili huru zilizoungana. Kwa maana iliyokuwa Zanzibar yaani Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika, ziliungana zikaunga Jamhuri ya Tanzania. Tokea kuasisiwa kwake yapo mafanikio yaliyopatikana katika muungano huo. Wala hatuwezi kusema kwamba hakuna mafanikio, mafanikio yapo. Lakini vile vile tunakubali kwamba na matatizo hayo yamelalamikiwa kwa muda mrefu na yamezaa malalamiko mengi. Ndio tukaona tumefikia hali hii ya kila mmoja analalamika leo. Kila mmoja amefikia kuuchukua Muungano kwa sababu ya matatizo yenyewe.

Mhe. Spika, mimi ninachosema hakuna Muungano usiokuwa na matatizo ulimwenguni. Matatizo ni lazima yatakuwepo kwa sababu ni sehemu ya maisha yetu. Kwa hivyo jambo la msingi ni kuyazungumza matatizo yenyewe na kutumia busara ya hekma katika kuyatafutia ufumbuzi ili tuwe na Katiba nzuri itakayotuelekeza namna nzuri ya kuwa na Muungano wetu utakaotusaidia kwa maendeleo na watu wake.

Mhe. Spika, ni vizuri sana tukayazungumza matatizo haya, tukayajua ni yepi na baada ya hapo basi Katiba hii itategemea maoni ya wananchi watakayoyatoa ili tujenge Muungano wenye maslahi, wenye kutetea haki za pande zote na utakaoridhisha wananchi wa pande zote.

Jambo kubwa ni kuwaachia wananchi waweze kutoa suluhu ya matatizo ya hiyo. Kamwe serikali zetu hazitoingilia maamuzi ya wananchi, hazitoingilia busara za wananchi, hazitoingilia maoni ya wananchi. Tutakachofanya ni kuhakikisha usalama wa wananchi unakuwepo, taratibu nzuri zinakuwepo. Tunawaomba wananchi waipoke Tume itakapokuja ili waweze kutoa maoni yao na hatima ya muungano wetu ionekane katika hali ya kila mmoja ambaye itamridhisha kwa Zanzibar waridhike wa Bara waridhike wa Bara waridhike ili tuwe na njia nzuri ya kuishi kwa salama katika nchi yetu, matatizo yaondoke, tuishi kwa furaha, tuishi kwa maelewano.

Sisi viongozi wa serikali hatutakiwi kabisa kabisa kuwa na misimamo, tukaieleza bayana. Kila mtu lake atakuwa nalo ndani ya moyo wake siku ikifika akaliseme. Kwa sababu tunachokitaka ni maamuzi ya wananchi ndio yachukue mkondo wa kuwa na Katiba tunayoitaka. Kwa hivyo mimi nitakuwa na mawazo yangu, Mhe. Makamo wa Pili atakuwa na mawazo yake, Waheshimiwa Mawaziri watakuwa na mawazo yao. Lakini hatutakiwi mawazo yetu hayo huenda ikawa ni misimamo na kuhamasisha wengine wayaunge mkono. Kila mmoja akatoe mawazo yake ili tuje na Katiba nzuri.

Mimi ninachotaka kusema Waheshimiwa Wajumbe hapa kwamba wananchi wetu wana uwezo na upeo mkubwa wa kutoa maoni, wanajua kinachoendelea, wanayajua matatizo yao, wanaijua suluhu ya matatizo yao. Wala tusidhani kwamba sisi tunajua zaidi kuliko wao. Inawezekana wanajua zaidi kuliko tunavyoyajua sisi, wanazijua shida zao kuliko tunavyozijua sisi, wanayajua matatizo yaliyopo kuliko tunayoyajua sisi. Mimi ninachosema kwamba tuwape nafasi wananchi watoe maoni yao tufikie muafaka na tuwe na nchi ambayo tutakaa kwa raha mustarehe bila ya kutuhumiana bila ya bila ya kuonesheana vidole, bila ya kubughudhiyana ili tuendelee kuishi kwa amani na utulivu mkubwa.

Sisi ndani ya serikali tuna wajibu wa kulinda Katiba, tuna wajibu wa kulinda sheria zilizopo mpaka hapo zitakapokuwepo Katiba nyengine mpaka hapo zitakapokuwepo sheria nyengine. Kwa sasa sheria hizi ni lazima ziheshimiwe, lazima zifuatwe ili tukae katika hali ya salama na utulivu mkubwa.

Mhe. Spika, kuhusu migogoro ya ardhi nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alieleza kwa undani sana na kwa umakini mkubwa matatizo yetu ya ardhi yaliyopo. Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Spika, migogoro ya ardhi ipo na serikali haijashindwa kuingilia migogoro ya ardhi. Serikali ilitoa nafasi kwa waliosababisha migogoro hii wende wakairekebishe na watakaoshindwa kuirekebisha basi serikali itachukua hatua dhidi yao. Hayo ndio maoni ambayo Mhe. Rais alikuwa anayasema kila wakati na huo ndio uwamuzi wa serikali. Serikali haishindwi kabisa kuondoa tatizo hili.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe dawa ya kuondoa tatizo hili ikojikoni. Serikali inalifanyia kazi vizuri sana karibu Ishallah itakuja na utaratibu mzuri wa kumaliza tatizo. Nilitoa nafasi kwa makusudi kwamba wale wahusika wenyewe waliosababisha matatizo wakayatatue matatizo ambayo wameyasababisha. Ni kweli ardhi yetu ni ndogo, ni moja katika tatizo kubwa sana ambalo linasababisha mgogoro wa ardhi. Lakini vile vile yapo matatizo ya viongozi na watendaji kutofuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za ardhi. Na vile vile wananchi wakati mwengine nao kutofuata sheria zilizopo za mambo ya ardhi, haya kwa kiasi kikubwa ndio chanzo cha matatizo yenyewe. Hivi sasa Serikali kuna mambo mbali mbali inaendelea kuyafanya.

Kwanza kuna mkakati maalum wa kupima masuala ya uchambuzi wa ardhi yetu, ili baadae kila mmoja ajue eneo lake ni lipi, lipi la Serikali, lipi lililobaki, lipi la matumizi haya, lipi la kwenye shughuli hiyo, kwa hivyo kazi hiyo inaendelea. Inaendelea sambamba na kufanya *master plan* ya miji yote mikuu Unguja na Pemba inafanyiwa *master plan* ili maeneo ya miji ijulikane, utaratibu mzuri wa miji ujulikane mambo yaende vizuri. Na nia ni kuwa na matumizi mazuri ya ardhi. Ardhi yetu ndogo tuitumie vizuri kwa mahitaji ya watu wetu ili tuweze kuitumia sisi na vizazi vinavyokuja. Kwa hivyo hatua hizo zinaendelea kuchukuliwa. Naomba sana sana Waheshimiwa kwamba katika wakati huu Serikali kushughulikia tatizo hili, basi tuipe nafasi ishughulikie ili tupate ufumbuzi wa kudumu.

Lakini Waheshimiwa hawakatazwi wananchi ama Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wanapoona matatizo ya ardhi basi waseme, wayaseme tena wayaseme kwa undani, na ushahidi watuletee ili hatua zichukuliwe. Kwenye hili napenda sana nimpongeze sana rafiki yangu Mhe. Saleh amenifurahisha sana matatizo ya jimboni kwake ameyaleta Serikalini, ametwambia hapa kuna tatizo, hapa kuna tatizo, hapa kuna tatizo. Tukasema basi kama hali ni hiyo tukutane na wahusika, tumekutana na wahusika wametueleza matatizo. Baada ya kutueleza matatizo tukasema sasa tuwe na kamati ya pamoja, wananchi na Serikali, ili sasa tuyazungumze na tuyapatie ufumbuzi matatizo ya ardhi yaliyojitokeza katika eneo la Vitongoji na maeneo mengine. Kwa hivyo ninakupongeza sana Mheshimiwa, na mfano huu ni vyema ukawafahamisha na Waheshimiwa wengine wakajua kwamba pale penye tatizo, basi Serikali iko tayari kusikiliza, kukaa pamoja na Wawakilishi na wananchi pale tutafute ufumbuzi muafaka, na matatizo ya ardhi nia ni kuyaondoa.

Mhe. Spika, kuhusu utafiti, ninaposema ninajua kuna Waheshimiwa walichangia kwenye maeneo yote haya. Ninaamini kweli niyarudie majina yao kila mara, kwa sababu takriban majina yote yanahusu katika maeneo yote, ninaomba ninaposema wanielewe kwamba nimetoa jibu husika kwenye lile eneo husika. Lakini hata hivyo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atakuja kuwatambua Waheshimiwa wote na Wajumbe wa Baraza hili waliochangia kwa ufasaha zaidi.

Nia ya kuimarisha utafiti ni kuona mambo yetu yanakwenda kisayansi na kimaendeleo zaidi, na yanakuwa endelevu zaidi, na ndio maana Serikali yetu imeamua kabisa kabisa tuwe na kitengo maalum cha utafiti katika kila Wizara, ili mambo yetu mengi yaende kisayansi, yaende kisasa tuyaendeleze kwa misingi ya kutuletea maendeleo mazuri zaidi. Na nia yetu ni kuendelea kuwasaidia watafiti chipukizi ili sasa watafiti wetu hawa wasiachwe peke yao, waweze kupewa kila aina ya msaada ili kuibua vipaji vya watafiti wetu wa ndani, ili baadae tuwe na watafiti wazuri zaidi watusaidie zaidi, iwe hatuna haja ya kutafuta wataalamu kutoka nje wakati wapo vijana wetu wazuri wana uwezo mzuri, wana vipaji vikubwa. Kwa hivyo jitihada na nia yetu kubwa ni kuendeleza suala hilo.

Vile vile kuanzisha mahusiano na taasisi mbali mbali za ndani na nje katika masuala ya utafiti ili tuimarishe utafiti nchini. Na kwa hili nataka sana nichukue fursa hii kuwapongeza sana sana ndugu zetu wa COSTEC, wameshirikiana na sisi vizuri na tumeanza vizuri nao. Kwenye hili ni eneo moja ambalo nataka niseme kabisa kabisa katika Jamhuri ya Muungano tumekubaliana tukafanya vizuri. Na hili lazima haki yake mwenye kutenda haki mpeni. COSTEC kwenye hili wametusaidia vizuri, tumeanza vizuri katika muda mfupi wameweza kusaidia chuo chetu cha utafiti pale Kizimbani zaidi ya shilingi milioni 641, wamewasaidia wataalamu wetu wa utafiti wa ndani zaidi ya milioni 550 jambo hili linatia moyo vizuri.

Mhe. Rashid Seif alizungumzia sana suala hili la utafiti, na hasa hasa kuhusu utafiti wa wadudu waharibifu na hasa kwa matunda. Jambo hili ushauri wake ni mzuri tunaupokea tunaufanyia kazi kama ambavyo ameusema kwa sababu ni jambo la msingi sana. Matunda yetu yakiharibika yanapunguza soko la wakulima wetu. Kwa hivyo hili ni jambo la msingi na tunaliunga mkono tutachukua kila jitihada tuendeleze utafiti huu. Jitihada hizi zishaanzwa, zikachukuliwa hatua na nia hasa ni kufanya utafiti zaidi ili matatizo yaliyopo yaondoke moja kwa moja.

Lakini katika eneo hili limejitokeza suala la kwamba Mhe. Abdalla amesema kwamba kwa nini huyu mtu wa SUGU II amepewa zawadi ya milioni mbili, wakati huo huo apewe vifaa vya 12,700,000. Hii inatokana na umahiri wake na fedha hizi zimetolewa na *COSTEC* hazikutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kutokana na umahiri wake wa utafiti wa kuweza kuunda gari lile kalianza mwanzo kaliunda peke yake ndio tena kaja na SUGU II. Sasa kadiri alivyokuwa ana- *improve* katika utafiti wake wa kufanya hivyo, watafiti wameona wampe moyo kutokana na kipaji chake, ili na wenye vipaji wengine wajitokeze wasaidiwe. Kwa hivyo alipewa milioni mbili kama zawadi, lakini na vile vifaa alivyovihitajia vya 12,700,000 alipewa fedha akanunue vifaa hivyo kwa msingi viweze kumsaidia kufanya vizuri katika shughuli zake. Kwa hivyo, hiyo ni nia ya kuendeleza wale wenye vipaji wajitokeze zaidi, wafanye vizuri zaidi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyojitokeza na hii imezungumzwa na Waheshimiwa kuhusu Baraza la Wawakilishi na sheria yake ya utawala. Mhe. Spika, niseme wazi kabisa sote tuliomo humu ndani tunaiunga mkono sheria hii, Serikali nayo inaunga mkono sheria hii. Lakini sheria hii ni muhimu ikawa sheria nzuri, ikawa sheria endelevu itakayotusaidia kukidhi mahitaji yetu, itakayotusaidia kuliweka Baraza katika utawala mzuri, itakayosaidia kulipa fursa zaidi Baraza, kulipa uwezo zaidi Baraza, kulipa mamlaka zaidi Baraza ili liweze kufanya wajibu wake vizuri. Kwa hivyo ni vizuri sana kuona wenzetu waliokuwa na uzoefu wa sheri hii tukawaiga, ni vizuri sana kujifunza zaidi ili tulinganishe wao na mazingira na hali yetu ya uchumi wa Zanzibar, ili tuje kuwa na sheria endelevu.

Na hili napenda nimpongeze sana Mhe. Hamza amechukua hatua kubwa sana kwenye jambo hili, na anaendelea kuchukua hatua yeye na baadhi ya Waheshimiwa wenzake, tunaunga mkono jitihada zake na sisi katika Serikali tunaendelea kuchukua hatua ili kuja kuwa na sheria iliyo nzuri itakayoweza kutusaidia katika kuliendesha vizuri Baraza letu. Lakini lazima sheria hiyo iangalie na hali halisi ya uwezo wetu wa kiuchumi. Mimi ninaamini sheria tutakayokuja nayo itakuwa ni bora kuliko sheria nyingi katika nchi za Afrika Mashariki, sheria yetu ina muelekeo wa kuwa sheria nzuri zaidi, kwa sababu ina mashirikiano makubwa na wadau mbali mbali ninaamini tutakuja na kitu zaidi kitakachoridhisha Wajumbe. Ijapokuwa kimechukua muda lakini ninaamini Mungu akitujaalia si muda mrefu tena basi tutaweza kuwa na sheria, ili Baraza letu liweze kufanya vizuri zaidi.

Lakini jambo jengine ambalo ni muhimu sana Mhe. Spika, ni kamati zetu za kudumu kupata muda wa kutosha katika kufanya kazi zake, hili ni jambo la msingi sana. Sote tungependa jambo hili lifanyike vizuri, wapate muda wa kutosha, lakini tatizo letu kubwa la nchi yetu ni hali halisi ya uwezo wetu kiuchumi. Lakini hicho kidogo kilichopo tunajaribu kila njia kiwezeshe shughuli za Baraza lifanyike vizuri. Hata mkitizama mara hii mtaona tofauti kubwa ya kibajeti kwa Baraza la Wawakilishi, nia ni kuziwezesha kamati zetu ziweze kufanya vizuri za kudumu na zile nyengine zinazoundwa Kamati Teule na kadhalika, ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na bila ya vikwazo.

Na hapa ningependa nitoe wito kwa watendaji wote wa Serikali kuheshimu kamati hizi, kuwaheshimu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kutekeleza wajibu wao mbele ya kamati hizi na mbele ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Bila ya mashirikiano, bila ya kuheshimu Baraza hili tukufu hatuwezi kwenda. Kwa hivyo cha msingi watendaji lazima sasa tutaweka utaratibu maalum kwa wale watendaji ambao hawako tayari kufuata taratibu na sheria na kanuni za Baraza hili, itabidi tuweke utaratibu wa kuwashughulikia. Kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe hawa wamenun'gunika muda mrefu, na mtu mzima wanasema akilia kuna jambo. Kwa hivyo kwa vyovyote vile tutafanya kila jitihada kwa wale ambao wanakuwa ni sugu kutosikiliza wito wa Waheshimiwa Wajumbe hawa ambao uko kisheria, itabidi sasa hatua kali dhidi yao zichukuliwe ili taratibu za nchi, mambo mema ambayo Waheshimiwa wetu wamekusudia kuyafanya yafanyike kwa utaratibu mzuri na tupate sulhu njema.

Mhe. Spika, vile vile kulikuwa kuna hoja nyingi kuhusu Tume ya Uchaguzi. Mheshimiwa nia yetu ni kuimarisha Tume ya Uchaguzi, tuwe na Tume ya Uchaguzi iliyo huru na yenye kutoa haki na yenye kufanya vizuri itakayoondoa malalamiko. Kumekuwa kukijitokeza malalamiko ya mara kwa mara kila wakati wa Uchaguzi Mkuu. Tunataka Mhe. Spika, uchaguzi unaokuja usiwe na malalamiko yoyote, na kila mmoja na kila mdau aridhike na Tume yetu ya Uchaguzi. Kwa hivyo jitihada zinachukuliwa kufanywa, tulikuwa na matatizo kidogo ya kifedha lakini mwaka huu mambo yataanza vizuri kwenye kuimarisha daftari letu na kuanzia mwaka huu kila mwaka

tutaendelea kuliimarisha daftari letu, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi, na ili tuondoe matatizo wakati uchaguzi unakaribia, mambo yote haya yawe yametayarishwa, yako safi, yako tayari na kila mmoja wetu aridhike.

Tunaendelea kuchukua ushauri wa kutoa elimu ya uraia, kutoa elimu ya uchaguzi ili wananchi wetu waelewe vizuri na tuje tufanye uchaguzi vizuri. Na jambo lolote kwenye maandalizi ya mapema yatatusaidia sana. Kwa hivyo maandalizi ya uchaguzi kufanyika mapema ni ushauri mzuri tumeupokea na tunaufanyia kazi. Na ninaamini kabisa Waheshimiwa wajumbe nimeona *practice* yetu nzuri kwenye uchaguzi wa Uzini, na vile vile mtaona *practice* yetu nzuri katika uchaguzi wa Jimbo la Bububu. Na huo utakuwa ndio *maximum* yetu ya kufanyia Uchaguzi Mkuu, nina hakika sote tutaridhika. Nia ni kufanya uchaguzi huru na wa haki utakaomridhisha kila mdau katika suala zima la uchaguzi.

Kuhusu masuala ya maafa. Mhe. Spika, kwanza niungane na wale wenzangu waliosema kwamba tuwe kila mwaka tunafanya dua maalum kuwaombea wenzetu hawa waliopatwa na ajali hii ya MV Spice Islander. Ni jambo zuri kuwaombea dua wenzetu ili wapate kulala mahala mema huko mbele ya haki, na sisi wengine sote njia yetu ni moja tunaelekea huko huko. Kwa hivyo jambo hili ni jema kuombea dua wenzetu kadiri tutakavyoweza kuwaombea dua, tuwaombee dua mmoja mmoja, tukipata kukusanyika, kwenye misikiti yetu na kadhalika, kwa hivyo hili ni jambo la kheri sana, tuendelee kuwaombea dua wenzetu. Na mimi nirudie tena kuwapa pole wale wote walioathirika katika ajali ile, na kuwatakia wale walioumia wapate afya njema, na wale waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi.

Mhe. Spika, kwanza niseme fedha zilizotoka sio fidia kwa wananchi, fedha zilizotoka ni misaada iliyotolewa na wananchi na wahisani mbali mbali. Fedha hizo zilizochangwa zilikuwa ni bilioni moja, milioni mia mbili arubaini na nane laki tano na nusu mia saba na sitini, hizo ndio fedha zote tulizokusanya. Mpaka sasa tumetumia asilimia 76 ya fedha hizo ambazo ni sawasawa na milioni mia tisa na arubaini na tano na laki nne na nusu. Kwa hivyo tuna bakaa ya milioni mia tatu na tatu, laki moja mia saba na sitini na moja. Lakini si bakaa hizo maana kuna watu 266 waliofariki dunia bado majina yao hayakuonekana katika orodha ile iliyoletwa na Tume ya Rais. Na tunaona sisi katika uchunguzi wetu kwamba watu hawa wana haki ya kupata haki hii. Vile vile kuna watu walio hai 37 majina yao hayakuwemo katika orodha ile ya Tume bado tunawasiliana na wenzetu kufanya tathmini, ili na wao 37 wapate haki yao. Kwa hivyo hizi pesa zilizobakia bado zitatumika na nyengine kidogo tutaongezea ili utaratibu uende vizuri na kila mmoja aweze kupata haki yake.

Sasa Mhe. Hija aliniuliza pale unayo habari ya dola laki tatu za Bima? Ninayo habari lakini walipotuletea sisi Serikalini sie hatukuwa tayari kuzipokea, tuliwaambia ziende huko huko kwa sababu wenye chombo ndio wanaopaswa kulipa fidia. Na wao walitakiwa walipe *insurance* ile kwa ukamilifu wake. Hapa pana mitego lazima tuelewane, tungekuja sisi tungeambiwa Serikali imeshapewa fedha za fidia za *insurance* za watu waliofariki na watu walioumia, wenye chombo ndio wakalipe, kiwango hiki kidogo.

Kwa mujibu wa Tume Makadirio yake iliona hivi kwamba waliofariki walipwe kima cha miezi thamanini cha mshahara wa chini. Maana 125,000 mara 80 maana yake ni milioni kumi. Sasa dola laki tatu hizi ni ujanja, hapa peke yake tukichukulia watu 1526 ni zaidi ya bilioni kumi na tano, laki tatu hazifiki milioni mia tano mtawapelekea vipi na hii ndio haki yao. Walionusurika walitakiwa walipwe milioni nane kila mmoja. Kwa hivyo ukichukulia hawa walionusurika 941, hapo kuna zaidi ya bilioni 20 zinatakiwa zilipwe lakini uamuzi huo utafanywa na mahkama tutajua. Lakini hii ndio iliyokuwa *proposal* ya Tume.

Kwa hivyo mtego huu mimi sijaukubali, wapo watu na ujanja wao mwingi wanataka kutuingiza. Na si huko tu na hata kwenye kulipa tunapata matatizo sana, ndio maana tukataka watu wetu waende mpaka kwenye shehia waone, utaletewa majina tu watu wanjanja wanataka wachukue haki za wenzao. Kuna mmoja anasema bwana umetupatia kweli mimi nilikuwa nataka nifungue genge langu. Sasa genge lako kwa pesa hizi za watu waliokufa. Kwa hivyo mjue kabisa kabisa kwamba kuna watu wajanja, ulimwengu wa leo upo ujanja mwingi. Kwa hivyo watu wetu tunaposema waende pale na mtu ajitokeze pale kwenye shehia watu wanajuana wanasema huyu hakai hapa, na huyu anakaa hapa ndio inachotokea. Kwa hivyo hakuna kificho kila mmoja mwenye haki yake apate.

Na kama yuko mtu amepewa fedha chini ya kiwango mtu huyo aje atuone, maana hapo sasa tuliwapeleka watendaji wetu kule, kuhakikisha kama watu wanapata pesa zao kamili, huyu sasa atatueleza kwanini kapata chini ya kiwango. Maana aliyenusurika laki nne kumi na mbili elfu na mia tano. Waliofariki laki tano na nusu, na nasema hizi fedha sio fidia ni haki yao Serikali iliamua wapewe kwa sababu chanzo chake ni nini? Fedha hizi zilitolewa na wafadhili,

wahisani na wananchi kutaka kusaidia operasheni ya ajali iliyotokea. Serikali ikasema fedha hizi zikae zije ziwasaidie wahusika. Serikali ndio iliyofidia zile pesa zote za operesheni na ule ubani wa mwanzo umetolewa na Serikali hizi mbali. Saa yoyote tuulizeni 1.2 bilioni zilivyotumika na aliyepata nani lazima orodha iwepo nyie mkinishika shingo hapa, na mimi ninawashika shingo watendaji.

Kwa hivyo, hii nataka niwahakikishie wapo wajanja watafanya ujanja, na nitakaemgundua kaila huyo ni wangu hakuna mchezo kwenye hili, watu haki zao wapewe, huu mchezo mchezo wa kulanalana umekwisha. Kwa hivyo wajue tu kila mjanja atakuja kunaswa, kwa sababu wana ujanja mwingi wengine wanalalamika hivi na hivi ni ujanja tu Mhe. Spika. Ukienda kule kwenye *field* ndio utajua yalivyotokea. Shauri ya kuchelewa kwetu ni kufanya tathmini, na Tume yenyewe ilitakiwa watoe maoni yake na sisi tuendeleze operesheni. Ninajua imechelewa tunaomba radhi wananchi kwenye hili.

Kuhusu chakula kilivyogaiwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza vyakula vyenyewe havikuwa vingi mchele ulikuwa polo 130 za kilo 50, Unga wa ngano polo 21, sukari polo 29, majani ya chai kilo 2, maharage kilo 50 mafuta ya kupikia geloni 88, wapi yalipelekwa ni kama ifuatavyo. Vituo 11; unguja 4 Pemba 7, Nyumba ya watoto Mazizini, nyumba ya wazee Sebleni, kituo cha watoto SOS Mombasa, nyumba ya wazee Limbani, kituo cha ugonjwa wa ukoma Makondeni, Istiqama Chake Chake, Alfunurania Pujini, kituo cha mayatima Barawa, African Muslim Agency Mabaoni na Juhudi Maarifa.Hivyo ndivyo vituo vilivyopelekewa. Kwa hivyo hiyo ndiyo hali iliyotokea kwenye utaratibu huu.

Waheshimiwa nia yetu safi ni kuimarisha kitengo hiki cha maafa, kiwe na uwezo zaidi kiweze kufanya shughuli zaidi, kiweze kutoa huduma vizuri zaidi. Ninajua kina kasoro nyingi mmetwambia, lakini niseme tumefanya tathmini yetu ya ndani tumeweza kujua mahitaji ya vifaa, lakini tulipozungumza na wenzetu wataalamu pale Israel, wakasema bado kwa mujibu wa *nature* ya Zanzibar, na ilivyo Zanzibar kunahitaji kufanywa shughuli hii kitaalamu zaidi muweze kujua zile *area* zote, mujuwe *source* ya *problem* ni ipi na kadhalika. Na wenzetu katika mazungumzo wamekubali kushirikiana nasi, ili tuweze kufanya vizuri katika masuala mazima ya kufanya tathmini tutaweza kujua wapi kikae kituo hiki, pafanyike nini, vifaa gani mnavyohitaji na shughuli gani waungane zaidi kitaalamu. Sote tunajua uwezo wa Israel kwenye mambo haya na hivi sasa wametualika katika mwezi wa Septemba, wataalamu wetu waende wapate ile semina ya awali halafu wajuwe utaratibu mzima wa kujiweka kimafunzo kwenye shughuli hii, ili waweze kusaidiana vizuri tuweze kufanikiwa vizuri zaidi.

Kuhusu Ofisi ya Faragha. Eneo hili Mhe. Spika, lilichangiwa na watu wengi, na hasa hasa ni ujenzi wa makaazi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, nia yetu viongozi wetu wote hawa Makamo wa Pili wa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Rais mwenyewe wakae katika majengo yenye hadhi stahiki. Kwa kweli majengo wanayokaa sasa hayafikii hadhi inayotakiwa. Tatizo letu la msingi ni uwezo wa kifedha kwa ajili ya ujenzi huu. Hasa kwa Pemba viongozi wetu wanapata shida sana wanapokwenda Pemba. Tumeanza kazi ya mwanzo ya kutafuta viwanja kwa ajili ya Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais, viwanja tumepata hivi sasa tumo katika shughuli za michoro ili kuwa na michoro inayokidhi haja ya makaazi ya viongozi wetu hawa. Haitakiwi nyumba tu inakiwa iwe nyumba na mahala pa kukaa na wasaidizi wake na kadhalika na kadhalika. Kwa hivyo iwe ni hadhi kamili, tatizo letu ni uwezo wa fedha, lakini Serikali ina mpango hivi sasa wa kuuza nyumba zake za zamani. Mpango huu utasaidia katika ujenzi wa kujenga nyumba za kisasa.

Sasa hapo Waheshimiwa mna haki ya kutoa maoni yenu, lakini Serikali iliamua kuuza nyumba za zamani zile na ikaweka utaratibu ziuzwe kwa tenda, ziuzwe kwa utaratibu maalum na iwe kuna uwazi katika kuuza kwake, taratibu zote za manunuzi zifuatwe, na sheria zote zifuatwe, ili nyumba hizi ziuzwe kwa thamani sahihi. Na tayari zimeshafanyiwa *evaluation*, kwa hivyo nyumba hii ijulikane ya thamani gani. Kwa hivyo hata wakija watu wa tenda wale wakija chini ya kiwango, Serikali ina haki ya kuuliza na kinachotajiwa hata wakishafikia ile thamani ya tenda kiasi gani kidogo, walete mawazo yao kwenye Baraza la Mapinduzi ili uamuzi ufanyike.

Kwa hivyo ninaamini mimi utaratibu utakwenda vizuri. Lakini wale watakaokwenda kinyume na utaratibu Waheshimiwa mpo mna wajibu wenu wa kusimamia mambo yaende vizuri. Kwa hivyo nia ni kuuza majengo ya zamani, tupate fedha tujenge majengo ya kisasa yakiwemo ya viongozi wetu wakuu. Kwa hivyo nia ni kujenga nyumba Pemba, nia ni kuziimarisha nyumba za Dar es Salaam. Vile vile ya Makamo wa Pili ya Dodoma, lakini kwa

kweli Dar es Salaam nyumba ziliopo si za kufanyiwa ukarabati baada ya kwenda kuonekana ni nyumba za kujengwa upya. Na bahati nzuri tunacho na kiwanja kwa hivyo kuwa-*accommodate* viongozi wetu wawili hawa itawezekana vizuri, kwa maana Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili, kwa hivyo taratibu zinaendelea za kuhakikisha kwamba namna gani tutakipata hiki kiwanja, hii nyumba ambayo sasa hivi Makamo wa Pili wa Rais anakaa, ili ilipiwe na Zanzibar na baada ya hapo basi shughuli nyengine zifuate. Dodoma tutaifanyia matengenezo ili ikidhi haja ya kihadhi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Kuhusu safari za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Mtando alitaka kujua anaofuatana nao. Napenda niseme anaoufatana nao katika safari za nje kwenye safari ya China; Mheshimiwa alifuatana na Mhe. Thuwaiba Edington Kissasi Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, alifuatana na Mhe. Subeit Khamis Faki. Safari ya Marekani alifuatana na Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango ya Maendeleo

Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Kamamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Kwa safari ya Israel alifuatana na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na safari ya Cuba pia niliukwaa mimi na Mhe. Waziri wa Afya. Hizo ndizo safari zake za nje na hao ndio aliofuatana nao.

Kuhusu Kiwanda cha Uchapishaji. Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe hatua mbali mbali zimechukuliwa katika kukiimarisha kiwanda chetu ili kiwe cha kisasa, ili kikidhi mahitaji ya leo na mahitaji ya ndani ya serikali na mahitaji watu binafsi, ndio nia yetu. Na hapa lazima niseme kidogo, wataalamu wetu hawana uwezo mkubwa sana wa kujua mahitaji yetu yote tunayoyahitajia ya aina gani ya kiwanda tunachokihitaji. Kwa hivyo, ilitubidi tupate kazi kidogo na kutumia uzoefu wa hapa na pale mpaka tuweze kufikia kujua ni aina gani ya mitambo tunayoihitajia itakayoweza kutusaidia, itakayoweza kutoa huduma vizuri na sahihi.

Napenda nishukuru kwa mashauriano na kwa imani za mawakala mbali mbali tumeweza sasa kujua ni mitambo ipi itakayotusaidia na tukawa nayo tukaweza kuwa na kiwanda cha kisasa kitakachokidhi mahitaji yetu. Lakini katika kufanya hivyo lazima vile vile ilikuwa tupate na jengo la kisasa litakalokidhi kuichukua mitambo yenyewe ikaweza kufanya kazi bila ya matatizo.

Serikali ilitupa eneo la Maruhubi lakini jengo lile limechakaa la zamani. Ilibidi kwanza kuijua mitambo gani tutaihitajia iweze kwenda pale ndio uweze kutengeneza mchoro, bahati nzuri sasa tunaijua mitambo tunayoihitajia tumeweza kutengeneza michoro na hivi sasa michoro tayari na kutokana na mahitaji hayo basi, ndio maana sasa tumeweza kuiambia serikali tunahitaji fedha hizi kwa ajili ya ujenzi na fedha hizi kwa ajili ya awamu ya mwanzo ya kununua mitambo ili shughuli ianze. Naamini mtakapoipitisha bajeti hii itakuwa fedha za kuendeleza Kiwanda cha Uchapishaji zimo humo na hatua za ununuzi zitaendelea baada ya kupitishwa kwa bajeti hii.

Lakini serikali ilitupa muongozo kwamba sasa kiwanda hiki kinatakiwa kijiendeshe kibiashara, kiwe na uhuru zaidi, kijenge uwezo zaidi wa kufanya faida. Kwa hivyo, tunachoendeleanacho sasa tunatengeneza *business plan* na mpango mzima wa kuanzisha shirika lililo huru litakalojitegemea, litakaloweza kufanya shughuli hizi kibiashara na litakaloweza kuzaa faida. Kwa sababu tukishakupewa fedha hizi ni tabu tena kupewa fedha nyengine, tunatakiwa fedha hizo tutazopewa tukiimarishe kiwanda, tukiendeleze, kizalishe, kifanye kazi vizuri kwa maslahi yetu na vizazi vinavyokuja.

Pia serikali imefanya uamuzi wa kuanzisha Bohari Kuu. Kwa hivyo, tutakuwa na shirika hilo ama kampuni jambo lolote litakalokuja lakini itakuwa lina *wing* mbili inayosimamia kiwanda na inayosimamia bohari kuu ili na *stationery* zote za serikali zinunuliwe kutoka katika bohari kuu ya serikali. Kwa hivyo, tuna kazi na wajibu wa kuitekeleza vizuri kwa maslahi ya nchi yetu.

Kuhusu Idara ya Sherehe na Mapambo. Hii ni Idara mpya waheshimiwa na ilikuwa inahitaji kabisa kabisa kuimarishwa ili ifikie viwango vinavyostahiki tunapofanya sherehe zetu, tunapofanya maazimisho yetu na mambo mengine yanayofanyika kwa mikutano ya viongozi wetu.

Sasa Wajumbe wengi walidhani kwamba idara hii inafanya shughuli zake mara moja moja, idara hii ina shughuli za kila siku sio tu inasimamia sherehe zote zinazofanyika katika nchi yetu, lakini hata ile mikutano ya viongozi wetu namna ya kuweka mapambo, namna ya kushughulikia na kadhalika ni idara hii inayosimamia. Kwa hivyo, mambo ya maadhimisho, mambo ya mazishi, kila shughuli ya serikali inapotokea inafanywa na idara hii sio sherehe za Mapinduzi peke yake, kwa hivyo ni shughuli zinazoendelea.

Kwa sasa idara hii imewaajiri watu 14, jumla ya wafanyakazi wataalamu na watoa huduma ni watu 14 na mishahara yao kwa mwezi ni shilingi milioni tatu na nusu, kwa maana kwa mwaka ni shilingi 42 milioni na *ZSSF* ni shilingi milioni tano kwa hivyo jumla hapo inakuja karibu shilingi 48 milioni na shilingi 20 milioni ni posho maalum kwa mwaka za wafanyakazi ndio maana Mhe. Rashid Seif kikaja kiwango hiki. Hii ni kutokana na kwamba wafanyakazi hawa wanapofanya kazi katika idara hii wanawekewa posho maalum kutokana na shughuli zao za kufanya kazi wakati mwengine mpaka usiku wakati wowote tu, kwa sababu shughuli zinapotokea, mazishi yanapotokea na mambo mengine hayana wakati kwa hivyo wakawekewa posho maalum kwa mwaka shilingi 20 milioni ndio maana kikaja kiwango kile.

Kuhusu thamani. Thamani zile mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:

Shilingi 13 milioni ni kwa ajili ya vifaa vya ofisi, meza, makabati, *photocopy machine*, viyoyozi, *fax* na *binding machine*. Kwa sababu wanakwenda kuhamia kwenye jengo jipya watakuwa hawakodi tena jengo, wanakwenda kwenye jengo jipya ambalo linajengwa la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wanakwenda kuhamia na vifaa hivi shilingi 13 milioni na shilingi 20 milioni ni mashamiana, viti 400, vipaza sauti, meza na viti maalum vya viongozi pamoja na zulia jekundu. Hiyo ndio *break down* ya shilingi 33 milioni. Ili vitu hivi vipatikane vitu hivi pia vitafanyika kibiashara, vitu hivi kama mashamiana, viti pia watakodisha kwa hivyo mbele ya safari idara hii itazalisha pia. Waheshimiwa hiyo ndio hali halisi.

Mimi mwenyewe mwanzo waliponiletea *estimate* kama swali alilouliza Mhe. Rashid Seif niliuliza, nilipopata *break down* hii nikaridhika. Kwa hivyo, Mhe. Rashid hiyo ndio hali halisi na ndio tathmini iliyofanyika.

Mhe. Spika, kuhusu kuongezeka kwa gharama katika idara mbali mbali, jambo hili alilizungumza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Ni kweli gharama zinasababishwa na sababu mbili, sababu ya kwanza ni hali halisi ya kupanda kwa bei ya vitu mbali mbali, lakini sababu ya pili ni kutokana na huu mfumo wetu wa sasa wa kupeleka *quarterly report* kwa maana ya bango kitita. Hili limeweza kutuwezesha kujua uhalisia wa shughuli zetu.

Huko nyuma tulikuwa na mtindo wa kuongeza asilimia tu, ukishafika mwisho wa mwaka unaongeza 10% au 15%, sasa huwezi kufanya hivyo kwa sababu unapokwenda pale kwenye bango kitita unajipeleka mwenyewe tena msidhani kwamba ni kazi rahisi wala msidhani kwamba mnaweza kudanganya hata ukidanganya utajitia mwenyewe kwenye tenga mana huyo wa kudanganywa yuko wapi? Bwana mkubwa mwenyewe anaweka rekodi zote za kila miezi mitatu ukifika anazo ndani ya kibindo. Sasa wewe unajikata mwenyewe pale na kwenye hili limetufanya kujua sasa mahitaji yetu ya kila idara, ya kila *section* na mtaona sasa uhaulishaji utapungua mana unajua uhalisia wa jambo ndio uliotufikisha hapa, lakini hatukufanya tu.

Kule ukienda bwanamkubwa pale ukifika tu anakwambia ehe hiyo asilimia ngapi, sasa wakati mwengine unafikia asilimia 1,000 ya kitengo fulani, hiyo maana yake hukujua makisio yako toka awali, hata ukifikia asilimia 200 hukujua makisio yako toka awali. Kwa hivyo, ilibidi sasa kutokana na bango kitita limetuelimisha, limetuwezesha kujua mahitaji yetu, kujua uhalisia wa mahitaji yetu na ndio maana tukapata haya yanayotokea, juu ya hivyo hizo fedha huwa hazitoshi kwa asilimia 100, lakini ndio hali halisi iliyotokea tukawa hivyo.

Sasa Mhe. Ismail Jussa aliulizia kwenye fungu lile la 220,400 Gharama ya mafuta na vilainishaji, kifungu hiki kimeongezeka kutoka shilingi milioni kumi kufikia 48 milioni. Hii ni makadirio ya makusanyo ya Kasma nne tofauti ambayo ni gharama za *petrol*, *diesel*, maji na umeme kama kitabu kinavyoonesha. Sababu za kuongezeka ni kutokana na kupanda kwa bei ya umeme, kuongezeka kwa bei za *petrol* na *diesel* na vile vile kwa sababu hiyo niliyoitaja ya suala zima la mahitaji na uhalisia wake.

Vile vile kwenye magazeti. Magazeti kutoka shilingi milioni mbili na laki moja na nusu tumefikia shilingi milioni nane na laki nane na ishirini elfu, nazo kwa gharama za magazeti peke yake bila ya majarifa ni shilingi milioni tano laki nne na ishirini na tano elfu, tufanye hesabu tu ya kiharaka haraka tutapata majibu hapa hapa ndani ni magazeti mangapi kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa siku tunafikia hatua hiyo, hizi ni pesa za mwaka mzima. Sasa Waheshimiwa hiyo ndio hali halisi, uamuzi mnao nyinyi lakini mkitupunguzia tutakuwa hatuwezi kufanya kazi zetu vizuri sana.

Vile vile kwenye posho la vikao tumetoka kwenye shilingi milioni moja tumekwenda shilingi milioni kumi, kwa nini tumefika hivyo? Mhe. Spika, hii ni kwamba vikao vya Bodi ya Zabuni, Kamati za Ukaguzi wa Ndani, Kamati za Mafunzo, lakini tuna vikao vya dharura Waheshimiwa kweli kabisa. Wizara yetu inakabidhiwa mambo kufanya shughulikia hili, hili, kamati hii chini ya Ofisi Makamu wa Pili wa Rais. Wakati mwengine wanatakiwa wapelekwe Pemba, wakati mwengine Dar es Salaam, wakati mwengine shughuli ndio kama hivyo mara limetokea la UAMSHO, mara la kwenda kupima viwanja Pemba, mara tatizo la ardhi, mara hili na lazima lishughulikiwe. Kwa kweli tunatoa vifungu vyetu vya ndani, inatunyima nguvu ya kufanya kazi na kila mara lazima kutazuka kikao na kikao na kikao kwa *nature* ya ofisi yetu. Kwa hivyo, kipato hiki ukikitizama kwa undani hakikidhi haja lakini inabidi ufanye kutokana na mazingira yalivyo.

Kuhusu hoja ya kuongezeka kwa kifungu cha malipo ya kujikimu na malazi ya Idara ya Maafa kutoka shilingi laki tano kwa mwaka 2011 kufikia shilingi milioni kumi kwa mwaka 2012. Kifungu hiki kilikuwa kidogo na hakikishi mahitaji hasa na kutokana na kazi za uandaaji wa mikakati ya kukabiliana na maafa katika wilaya ikiwemo utoaji wa mafunzo wa kamati za kukabiliana na maafa. Hawa viongozi wetu wanakwenda wanatoa mafunzo na wanatakiwa watoe kwa shehia zote Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hiyo wenyewe wanajua hata wakipeleka shilingi laki tano uhaulishaji unakuwepo ama kazi hazifanyiki. Kwa hivyo sasa utaona vifungu vingine viko chini na vyengine vinakuja juu kutokana na mazingira ya bango kitita. Kwa hivyo, Waheshimiwa hiyo ndio hali halisi ya kwa nini gharama zimeongezeka.

Kuhusu sensa. Mhe. Spika, sensa ina umuhimu wake na hapa inatubidi Waheshimiwa sote tukasimamie tuwahamasishe wananchi wende wakajiandikishe siku ya sensa. Na siku ile haitakuwa siku moja tu huenda ikaendelea kwa siku tano au siku saba ili wananchi wetu waweze kuandikishwa, nia na madhumuni ni kujua wananchi wetu wako wapi, mahitaji yao ni nini, matatizo yao ni nini, vipi wasaidiwe, vipi tuweze kujenga shughuli zetu vizuri za kimaendeleo na kiuchumi. Unapokuwa hukuandikisha watu hawajulikani walipo ndio tunapata matatizo, unaona leo unapeleka kisima cha maji chenye uwezo wa kutoa geloni 20 kwa siku kumbe panahitajika chenye uwezo wa geloni 50 au 100, lakini kwa sababu hujui idadi huwezi kufanya hivyo. Unajenga hospitali unafikiri kuna watu 200 kumbe kuna watu 1,000.

Kwa hivyo, ni muhimu sana jambo hili na lazima tuwaeleweshe mashehe wetu, wazee wetu wasisusie jambo hili, kususia jambo hili ni kujirudisha nyuma kimaendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo sote tushirikiane tukahamasishe suala la sensa. Na ninapokea ushauri wa Mhe. Hija Hassan Hija alisema hawajaona ushirikishwaji kwenye kamati za wilaya. Hili tutalifanyia kazi tunapokea huu ushauri tutashirikiana na wenzetu wanaosimamia kwa upande wa Wizara ya Fedha tujue ni nini lililokwamisha hili lakini tunatakiwa tuwemo tujue maendeleo yetu kwa sababu sisi ndio watu tunaowajibika zaidi katika kusimamia maendeleo ya watu wetu.

Kuhusu *TASAF*. Hapa Waheshimiwa mimi nataka niupokee sana ushauri wenu. Tunayo matatizo ya msingi ya miradi mingi ya maendeleo hasa inayopitia katika majimbo, fedha nyingi zinakwenda huko matokeo hakuna kabisa kabisa, tuna miradi ya *TASAF*, tuna *MACEMP*, tuna AK, JK miradi mingi fedha zinakwenda, Waheshimiwa wenyewe Wajumbe wa Baraza hili wana Mfuko wa Maendeleo zao wenyewe mfukoni lakini *impact* kule chini haionekani.

Tatizo la msingi sana, ingekuwa mambo haya yanafanyika vizuri wala leo tungekuwa hatuna haja tena ya kuongeza pesa humu ingekuwa huko chini kunaanza kuzalisha kwa fedha zilizoingia, kama tumepigwa, sijui ruhani gani huyo aliyeingia kwamba kila kinachofanyika huko chini hakitoki tena huku wala huoni matokeo. Kwa hivyo, serikali imeona jambo hili na ndio imeona umuhimu wa kufanya marekebisho kwenye Tawala za Mikoa ili huku kwenye viungo vya chini kuwe na watendaji pia wa kutusaidia na kusimamia wenye uwezo wa kiserikali hasa kusimamia fedha hizi za umma zinapokwenda. Kwa hivyo, utaratibu wa Tawala za Mikoa utakuja kutusaidia sana kwenye eneo hili.

Lakini kwa sasa mimi nakubaliana na wao sana ushauri wa Waheshimiwa kushirikisha Kamati za Maendeleo ya Jimbo kwenye masuala ya *TASAF* naamini kutakuwa na usimamizi zaidi kuliko ulivyo leo, yapo matatizo. Miradi mingine imejengwa katika maeneo yasiyostahiki, unakwenda unalikuta soko la samaki liko huko bandari iko huko mambo mawili tofauti, ni kichekesho. Kwa hiyo, sasa tuendelee kufanya tathmini ya kina na sasa katika mradi lazima tuamue kabla ya kufanya mradi wa *TASAF* tufanye tathmini ya kina tuone na wananchi wenyewe wote wa eneo wakubali kwamba huo ndio mradi wao wanaoutaka hapo. Inaonekana kulikuwa na *influence* nyengine zikisababisha mambo haya yasifanyike vizuri, kwa hivyo lazima sasa tuyasimamie vizuri na kwa uadilifu maana pia

inaonekana *value for money* kidogo ni mtihani pia. Kwa hivyo mimi nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa yafanyike vizuri zaidi na miradi yetu hii ilete manufaa kwa wote.

Mhe. Spika, yako mambo mbali mbali yamejitokeza, moja lilizungumzwa na Hajjat hapa Mhe Mtumwa Kheir Mbarak, huwa sipendi kuzungumza sana kuhusu mashehe wangu hawa lakini kidogo kaniongezea jambo si langu. Alisema nimesema kwenye hotuba yangu serikali italipa makanisha yaliyochomwa moto, sikusema hivyo mimi, mimi hotuba yangu nilisema waliochoma moto makanisa wana wajibu wa kuyalipa na wao wawajibike kulipa, wale waliochoma wale ndio wawajibike kulipa sio serikali ndio nilivyosema mimi. Kwa hivyo Bi Mtumwa hivyo ndivyo nilivyosema tusitumie *forum* hizi jamani kutugombanisha na mambo ya kidini, sote Waisilamu, humu ndani asilimia kubwa ni Waisilamu na tunaupenda Uisilamu lakini serikali haina dini wenye dini zao ni wananchi wenyewe. Kwa hivyo sisi ijapokuwa Waisilamu lakini tuna wajibu wa kusimamia pia na dini nyengine, tunapoona kumetokea tatizo tuna wajibu na tunafanya hivyo kwa nia njema kuepusha shari na matatizo.

Tulipata mtihani mkubwa sana kwenye mambo ya uchomaji wa makanisa, tulipata ujumbe mkubwa kutoka kwenye Jumuiya ya Makanisa ya Tanzania na walikuwa wakali sana na mimi nasema kuna maneno mengine tuwe na vipimo kwa sababu yanaweza kuanzisha chuki, hasama na ugomvi wa bure. Wenzangu wengi wamesema hapa, Mhe. Ismail Jussa alisema katika nchi ulimwenguni ina *tolerance* ya kidini moja ni Zanzibar, kwa hivyo tabia na utamaduni huo tuuendeleze tusirudie tulikotoka, yaliyopita yamepita tugange yajayo, lakini tuishi na wenzetu hawa.

Mhe. Omar Ali Shehe alisema vizuri sana, Waisilamu wana haki yao, Wakiristo wana haki yao, Wahindu wana haki yao na hata wasioamini dini wana haki yao mana ni wananchi wapo na wote hao wanataka kulindwa na serikali na hasa *minority*, likitokea jambo wanaona kama wanaonewa zaidi wao na hawasimamiwi inabidi tufanye kila aina ya jitihada ili kuendesha nchi yetu kwa busara, hekma na kutafuta njia ya kubakiwa na amani na utulivu. Kwa hivyo hatuna nia yoyote mbaya na Mwenyezi Mungu anajua imani zetu inawezekana sisi tunaonekana imani yetu ndogo kumbe tuna imani kubwa ndani ya moyo wetu Mwenyezi Mungu anajua na mimi jitihada zangu zote ni kuhakikisha nchi yetu inakuwa na amani na utulivu, ndio ninachokitaka tu hicho sina chengine.

Kwa *nature* ya kazi yangu lazima wajibu huo niufanye lakini kwa imani yangu ya nchi nataka hilo, nataka umoja, upendo, amani na maelewano na hiyo pia ni *nature* yangu mwenyewe binafsi. Sijajaribu hata siku moja nasikia tabu kweli kuona kunatokea tatizo hili na hili sipati usingizi mimi, ninachotaka tutulie kabisa kabisa lakini watu wanaotaka kutafsiri Mungu yupo na atanisaidia *Inshaallah*.

Kuhusu suala la kubaguana Waunguja na Wapemba jambo hili si zuri hata kidogo, tusifikishane hapo. Sisi watu wamoja ubaguzi haufai hautufikishi popote, Mwenyezi Mungu anapenda watu wamoja, watu wanaoelewana, watu wanaosikizana na nchi itapata baraka. Nyinyi nyote tizameni tumeanza kuelewana watu mbali mbali, nchi mbali mbali zimeanza kutuunga mkono na ziko tayari kutusaidia. Kumetokea vurugu hii ndogo tumepata mtihani mkubwa sana, tena mtihani mkubwa sana wa kiuchumi, kijamii na ile sifa kubwa tuliyokuwanayo inaanza kupungua. Tuchukueni hadhari tuhakikishe tunakaa pamoja, tunaelewana tunafahamiana.

Kuna maneno kunajengwa *base* ya Marekani Tunguu. Jamani unapoambiwa na wewe jiambie, Tunguu kunajengwa Chuo Kikuu hakujengwi *base* ya Marekani, mana lazima tufahamu sio kila jambo unaloambiwa ulifikishe katika chombo kikubwa hiki papime. Tunguu pana viwanja wananchi wanakaa hata mimi ninacho kiwanja pale, Tunguu panajengwa Chuo Kikuu ndicho kinachoendelea, Tunguu kuna Ofisi ya Mkoa, Tunguu kuna Ofisi na majengo ya makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiyo yaliopo hakuna *base* ya Marekani. Sasa je, kuna kero ngapi kwa Tanzania Bara za Muungano na kwa Zanzibar kwa Muungano.

Kero za Watanzania Bara watazijua wenyewe walizonazo mimi nazijua zetu hapa zipo tumezizungumza, tunaendelea kuzizungumza, hata Rais juzi alizisema kwenye hotuba yake na mimi ninazo wala sina haja ya kuzirudia kila mmoja anazijua hapa. Kwa hivyo, kero zipo nia ni kuziondosha tukasemeni vizuri namna ya kuziondosha zisiwepo kero hizo tuishi kwa raha mustarehe na furaha.

Uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi hii ilikuwa yako ya Bahari Kuu. Naona kwenye eneo hili tunaendelea vizuri, tumeshapiga hatua kubwa, jengo linaendelea vizuri na nia ni kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu. Kubwa zaidi ni kukaribisha wawekezaji. Jitihada zinachukuliwa ndugu yangu Mhe. Said Ali Mbarouk aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi alianza kazi hii na sasa Mhe. Waziri aliyepo sasa wa Mifugo anaendeleza kazi hii kwa vizuri sana ya kutafuta uwekezaji na namshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili jambo analizungumza

sana, katika maeneo mengi na dalili nzuri za wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika viwanda vya kusindika samaki zinaonekana. Vile vile katika uvuvi wa Bahari Kuu zinaonekana, Mwenyezi Mungu atatuletea heri cha msingi ya kuvutia yote ni amani, umoja, na utulivu.

Kuhusu polisi kupata nyumba za makazi na magari tunalichukua Mhe. Makame Mshimba hili tuwapelekee wenyewe watu wa mambo ya ndani wafanye hizi shughuli. Ni kweli kuhusu umuhimu huo polisi kupata nyumba zao, magari, vifaa vya kisasa, zana za kisasa pamoja na za kujikingia. Kwa hivyo, jambo hili umelifikisha kwetu wizara husika tutawaandikia rasmi kuwaeleza matatizo ya polisi hapa Zanzibar.

Vikao vya pamoja SMT na SMZ visiendelee. Jamani yako manufaa ndani yake tuendelee kuzungumza, kuzungumza tuendelee na mengine yanafanyika kupitia maoni ya katiba, tukikataa kuzungumza hatujajenga msingi wa mustakabali mwema wa nchi yetu. Tukazungumze na sasa tuzieleze *concern* za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kuna mmoja hapa alisema Mhe. Makamu wa Pili hebu mkienda na mimi nitie ndegeni, nataka niwahakikishie maneno yanayosemwa kwenye vikao vyetu pengine ni zaidi ya haya tunayoyasema humu ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria shahidi yule pale, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika yule pale na wengine, makubwa yalitokea mara hii yakielezwa kinaga ubaga matatizo ya Zanziabar. Ninachoomba jamani tukazungumze, katika kuzungumza lazima litazuka lenye heri, tusikatae mazungumzo na utaratibu mwengine upo huu tuutumie wala hatuoni haya kwenye kuzungumza na mushatuzidishia kazi. Wakati mwengine tutakuja na *forum* hii baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hebu tuwachukueni mara moja waka-*witness* kile tunachokizungumza ili waje waeleze wayaone. Mhe. Hamza alikuwemo humu alikuwa ni *co-chairman*, alikuwa mkali kweli na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atamuwezesha tutakuwa naye pamoja.

Kuhusu mafuta na gesi asilia, hili jambo nimeshalizungumza mara nyingi, sina haja ya kulirudia tena. Kuhusu uwezeshaji kwa benki ya vijana Mhe. Haroun kasikia, na yeye ana mpango wa mambo haya ya benki na hili alilieleza vizuri sana serikalini kwamba nia ni kutafuta benki za maendeleo kwa sekta za vijana, wanawake, watoto na kadhalika. Lakini hivi sasa anaanza na benki ya ushirika ambayo ita-*serve* masuala ya vijana na kadhalika. Tutakushukuru sana kwa jitihada zako hizi.

Watendaji wasiounga mkono serikali ya *GNU*. Lazima tuunge mkono serikali yetu, usipounga mkono maana yake hufai. Sasa utafanyaje kazi katika serikali ambayo huiungi mkono na njoo useme sitaki tukuondoe. Sasa itabidi tufanye *venting* maalum, maana kama mwenyewe huji kujisema itabidi tuje tukutafute, musituharibie. Nia ya kuendelea, kuijenga Zanzibar na kuleta maendeleo ya watu.

Haya jana alieleza uzuri Mhe. Haji Omar Kheri. Hii mikataba inayokuja sasa itamkuta kila mtu, hata *increment* yako huipati kama hujafanya wajibu wako vizuri. Kwa hivyo mimi ninaamini tutakwenda vizuri kwenye mambo haya.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri sina hakika kama mumegawana vizuri na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, lakini muda ambao uliokwishautumia karibu saa moja na nusu. Sasa una dakika mbili tu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, hii ni kutokana na Waheshimiwa Wajumbe wako wengi wali-*raise* hoja nyingi ndio maana yakanikuta haya. Lakini Mhe. Spika, ninaamini Waheshimiwa wameshajua kwamba muda hauruhusu tena na kwa sababu ninaamini tuliyoyasema yatakuwa yamekidhi haja kwa kiasi fulani, na ninawaomba na kuwanyenyekea kabisa jamani tuipitishe bajeti yetu ili mambo yaende vizuri. (*Makafi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri nilitaka kukuzindua kwamba muda unayoyomea na tunategemea tupitishe vifungu kipindi hiki cha asubuhi. Ninashukuru kwamba Waheshimiwa Wajumbe umejitahidi sana kuwapa maelezo. Nadhani Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atamalizia pale ulipoachia. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais (*Makofi*).

Wakati Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anajitayarisha kutoa maelezo, niwaombe Waheshimiwa ambao wapo nje hapo kuvuta hewa kidogo, basi sasa waingie ndani ili baada ya hapo tuweze kuendesha shughuli nyengine iliyobaki.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nianze kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu waliochangia hoja hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Najua michango waliyoitoa yote ilikuwa na nia ya kuiongoza serikali namna ya kufanya mambo yake kwa ubora zaidi. Michango Mhe. Spika, ilikuwa ni mingi kuna Wajumbe 33 waliochangia kwa kusema na Wajumbe 6 walichangia kwa maandishi. Kwa hivyo ukiona kuna Wajumbe 39 wamechangia hoja hii, ujue michango mingi sana imechangiwa kwa nia ya kuendeleza, kuimarisha utendaji ndani ya serikali.

Mhe. Spika, kwanza naomba niwatambue wale waliochangia katika hoja hii. Nao ni:-

1. Mhe. Ali Salum Haji ambaye amewasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa niaba ya Mwenyekiti.
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Asha Bakari Makame
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Omar Ali Shehe
6. Mhe. Rashid Seif Suleiman
7. Mhe. Asha Abdu Haji
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
10. Mhe. Saleh Nassor Juma
11. Mhe. Nassor Salum Ali
12. Mhe. Mohamed Haji Khalid
13. Mhe. Hamza Hassan Juma
14. Mhe. Hija Hassan Hija
15. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
16. Mhe. Salum Abdalla Hamad
17. Mhe. Mgeni Hassan Juma
18. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
19. Mhe. Kazija Khamis Kona
20. Mhe. Abdi Mosi Kombo
21. Mhe. Salmin Awadh Salmin
22. Mhe. Fatma Mbarouk Said
23. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
24. Mhe. Subeit Khamis Faki
25. Mhe. Shawana Bukheit Hassan
26. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
27. Mhe. Hassan Mohamed Omar
28. Mhe. Rufai Said Rufai
29. Mhe. Panya Ali Abdalla
30. Mhe. Sira Ubwa Mamboya – Naibu Waziri wa Afya
31. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu – Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
32. Mhe. Haji Omar Kheri – Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora
33. Mhe. Othman Masoud - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
34. Mhe. Mohamed Aboud Mohamed – Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

Niwatambue pia waliochangia kwa maandishi. Nao ni:-

1. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
2. Mhe. Marina Joel Thomas
3. Mhe. Mohamed Said Mohamed
4. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
5. Mhe. Thuwayba Edington Kissasi – Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
6. Mhe. Farida Amour Mohamed

Mhe. Spika, pia niwatambue wale waliotaka kuchangia lakini hawakupata nafasi akiwemo:-

1. Mhe. Suleiman Hamad Khamis
2. Mhe. Ashura Sharif Ali
3. Mhe. Asaa Othman Hamad
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir

Kama yupo mheshimiwa yeyote ambaye amechangia na sikumtaja naomba radhi.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa kweli amefanya kazi nzuri na amenirahisishia sana kazi. Kwa hivyo sasa mimi kazi yangu itakuwa ni rahisi na haitochukua muda mrefu ili tuweze kupitia vifungu vya bajeti hii. Lakini nipitie mambo muhimu kwa haraka haraka yaliyoguswa na kila Mwakilishi.

Suala la Muungano kwa kila Mwakilishi Mhe. Spika, amezungumzia suala hili na kwa mujibu wa upeo wake na mwelekeo wake. Kuna wengine wamesema hawataki muungano, wengine wamesema wanautaka muungano, wengine wanautaka muungano wa serikali mbili, wengine wamesema muungano wa serikali tatu na kadhalika.

Kwa hivyo, kila mwakilishi hapa ameuzungumza muungano kwa namna anavyoona mwenyewe. Ninawapongeza sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kuchangia suala la muungano kadri mulivyoona inafaa.

Suala la muungano Mhe. Spika, sisemi kuwa halina kasoro, lina kasoro na lina kero. Sina hakika kwamba kero hizi za muungano zimesababishwa na muundo wa muungano au zinasababishwa na udhaifu wa utekelezaji wa mambo tunayokubaliana katika vikao vyetu.

Maana tukikubaliana kitu na halafu hakitekelezwi kama mulivyokubaliana, hili peke yake ni kero. Lakini tuangalie vile vile unakuja mchakato wa Katiba tuseme wazi, waliokuwa wanautaka muungano waseme, waliokuwa hawautaki muungano waseme, wanaotaka muungano wa serikali ngapi waseme ili hatimae tuwe na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyo nzuri na yenye manufaa kwa Zanzibar (*Makofi*).

Kwa hivyo na mimi ninaungana na wote waliosema kwamba wananchi wote wajitokeze kwenda kutoa maoni yao kwenye Tume ya Katiba itakayoanza kufanyakazi hapa Zanzibar. Lakini kuna wengi walisema kuwa serikali haijawaandaa wananchi katika kutoa maoni yao. Serikali haimuandai mtu kwa sababu serikali yenyewe kwanza haina maoni. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina maoni kuhusu Muungano. Maoni yapo kwa wananchi wenyewe.

Na sisi humu ndani kama kuwaandaa wananchi wetu tuna wajibu wa kufanya hivyo, kwa sababu sisi humu ndani ndio wenye watu. Tuelimishe wananchi wetu katika majimbo yetu. Tena tuwaelimishe vizuri na tusiwapotoshe.

Mhe. Hamza Hassan Juma alisema kwamba hata sisi Wawakilishi hatufanyi kazi vizuri kwenye majimbo yetu. Hakuna hata mwakilishi mmoja aliyekwenda katika jimbo lake akaelimisha juu ya Katiba hii ambayo itachangiwa na wananchi wetu. Watu wetu hawaijui Katiba hii. Kwa hivyo ilikuwa ni jukumu letu kufanya hivyo, sio jukumu la serikali.

Kwa hivyo hata sisi wawakilishi tunaopiga kelele humu ndani bado hatukuweza kufanya kazi yetu. Tukaanze kufanya kazi yetu hivi sasa, tuwaelimishe wananchi wetu mchakato wa Katiba unakuja, maoni munayotaka mutoe, kuna mambo haya na haya.

Tuseme suala la muungano basi muwaambie, hivi muungano huu una kasoro zipi, una faida zipi, una hasara zipi, nini kifanyike au tuseme kujitoa ndani ya muungano, kuna hasara zipi, kuna faida zipi. Haya yote tuwaelimishe wananchi wetu ili waweze kutoa maoni yao vizuri.

Si vizuri kutoka usiku usiku kwenda kuorodhesha majina ya watu, wewe unataka muungano au hutaki muungano, sio sahihi, hatuwezi kufanya hivyo, maana yake hakuna tija. Halafu ukishapata hao wanaotaka muungano elfu moja, wasiotaka muungano elfu mbili utafanya nini, hakuna cha kufanya. Twende kwenye Tume tutoe maoni yetu kwa uwazi na uhuru bila ya kulazimishwa na mtu yeyote. (*Makofi*).

Tusiwatie wananchi wetu maneno vinywani mwao kwamba nenda kaseme hivi na hivi, tuwaachie wenyewe almuradi tuwape elimu. Sisi hapa ndio wenye kutoa elimu na sheria imetoa vile vile uhuru wa vikundi mbali mbali kutoa elimu kwa wananchi juu ya Katiba mpya, na sisi tufanye hivyo.

Yapo maoni kwamba labda Baraza hili nalo litoke liunde Kamati kwenda kuwaelimisha wananchi hao almuradi tunafuata sheria. Kwa sababu haya ya kuwaelimisha wananchi kuhusu Katiba yamo ndani ya sheria. Tufuate sheria, tupate kibali cha Tume, tueleze fedha tumepata wapi halafu tukaelimishe wananchi wetu. Ndivyo sheria inavyosema.

Kwa hivyo mimi mwenyewe maoni yangu ninayajua mimi mwenyewe, maoni ya mwengine anayajua yeye. Lakini serikali kama ilivyo haina maoni, maoni yapo kwa wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, nizungumzie hali ya siasa nchini. Mhe. Spika, hali ya siasa nchini ni nzuri. Tunakwenda vizuri, tupo salama, tuna na amani. Tangu tuunde serikali ya Umoja wa Kitaifa hali imebadilika miongoni mwetu. Tuangalie tulivyokuwa kuanzia mwaka 1995 mpaka 2005 tulivyokuwa, tulikuwaje. Ilikuwa hatuendeani mazikoni, harusini, hatusalimiani, kazi yetu ilikuwa ni kutukanana tu, kukashifiana tu. Leo ndani ya Baraza ni shahidi kwamba hali hapa hata humjui nani CCM au *CUF* nani humu ndani.

Hata ndani ya Baraza la Mapinduzi si rahisi kumjua Waziri wa CCM ni nani na wa kutoka *CUF* ni nani. Sote tunafanya kazi kwa umoja wetu na kwa maslahi ya nchi yetu, na hicho ndicho tunachokitaka.

Ninaomba sana utulivu tuliokuwa nao, amani tuliyokuwa nayo na usalama tuliokuwa nao tuendelee nao. Tusikubali watu wengine kuchafua amani na utulivu tuliokuwa nao.

Ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi amezungumzia suala la Uamsho. Mimi ninasema tu Uamsho lazima itii sheria, lazima itii amri ya serikali ndivyo amani itaendelea. Wakati serikali inasema hakuna kufanya mihadhara, maandamano, makongamano, wewe kwa nguvu unakwenda kufanya, maana yake nini? Unaitakia nini nchi hii sasa si vurugu. Sote tutii amri za serikali.

Kama serikali imesema marufuku kufanya hivi basi tufuate. Lakini sasa tukianza kufanya mambo kwa nguvu, ndio matatizo yanakuja. Kwa sababu tuna vyombo hapa vya kulinda usalama wa wananchi na mali zao. Lazima vifanye kazi yake vikiona kama kuna hatari inakuja. Hatutaki tufike huko. Tuelimishane sawa lakini tuelimishane kwa utaratibu maalum wa sheria za nchi. Tufanye mambo tukaanza kuleta vurugu, tukaanza kuwaletea hasara wananchi wetu.

Zile vurugu za karibuni za tarehe 26 na 27, watu walikosa mapato yao siku, maana watu walishindwa kwenda marikiti, nasikia kulikuwa kutupu. Mwanakwerekwe sokoni kulikuwa hakuna kitu, watu wamekosa, uchumi wao umeporomoka. Hivi kweli tutakubali tuendelee katika hali hiyo? Hatuwezi kukubali. Wananchi wetu wanategemea kipato wanachokipata kwa siku ili waendeshee maisha yao.

Leo unamfanyia vurugu hawezi kufanya biashara. Tunamtakia mema mwananchi yule. Kwa hivyo mimi ninasema tutii sheria ili tuweze kuendelea kuwa na amani, utulivu na usalama ndani ya nchi yetu.

Suala la uwajibikaji limezungumzwa sana ndani ya serikali. Mimi ninakubali uwajibikaji ndani ya serikali bado ni mdogo. Watendaji wetu bado hawafanyi kama vile ambavyo wanatakiwa wafanye. Lakini mimi ninafikiri tatizo kubwa hapa ni usimamizi. Kwa hivyo mimi hapa ningeomba sana Mawaziri wawasimamie watu wao vizuri, wasimamie Makatibu Wakuu wao vizuri, na Makatibu Wakuu wasimamie Wakurugenzi wao na Wakurugenzi wawasimamie watu wao walio chini yao.

Bila ya hivyo ndio utakuta mtu anafanya kazi anavyotaka. Sisi serikalini kwenye ofisi yangu itajitahidi kuona kwamba kila wizara inatekeleza wajibu wake vizuri kwa kuwatumikia wananchi vizuri.

Lakini pia niwasihi sana Mawaziri kuwa na mashirikiano na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nimekuwa nikipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili, kwamba unajua ukenda kwa Waziri fulani, ukifika kule keshasikia nipo lakini ananiweka kwanza anamtia huyu, anamuingiza huyu, mimi nipo pale. Sio jambo jema Mhe. Mwakilishi akija kwako mpe heshima inayostahili. (*Makofi*).

Maana kuna Waheshimiwa wengine humu ndani wanakuja kuniambia kwamba kukuona wewe ni rahisi zaidi kuliko kumuona waziri fulani. Sasa hiyo sio *spirit* nzuri ya ushirikiano baina ya mawaziri na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tuwape heshima wanazostahiki Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Umesikia kuna Mhe. Salmin Awadh amekuja kukuona, kama kuna mtu hebu mwambie hebu subiri nimuone mheshimiwa kwanza, mpe heshima yake. Mimi kwangu nikisikia amekuja Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tutamwambia hebu subiri, sio ninamkaribisha kwa sababu ni Mwakilishi wa Jimbo langu, hapana. Nampa heshima yake kama ni Mwakilishi kwa sababu ninahitaji ushirikiano wake. Kwa hivyo lazima Waheshimiwa Mawaziri tufanye hivyo. Mimi nisingependa malalamiko haya yanaendelea.

Lazima tuwaheshimu, tushirikiane na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu wanapokuja kwako, lazima wana sababu, kama anakuja kwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ana tatizo huyo, kama anakuja kwako kwa Mhe. Waziri wa Uvuvi na nini ana shughuli fulani huyo. Sasa kwa nini umpuuze, umfanye ni s*econd grade*. Pale kama pana Waziri mwengine unaweza kuzungumza na Waziri baadae, hata hivyo unaweza kusema hebu tumpishe Mwakilishi tumsikilize. Lakini hatuwezi kufanya kazi hizi za kuwadharau Waheshimiwa Wawakilishi wetu ambao tunawahitaji sana katika kupeleka mbele maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo mimi ninasema Waheshimiwa Wawakilishi tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunawajibika ipasavyo katika utendaji wetu. (*Makofi*).

Pia kuna suala la utekelezaji wa Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, tumeipokea ripoti hii hatujaipuuza mpaka hivi sasa ninapozungumza hapa inafanyiwa kazi pale Ofisi ya Rais. Ninategemea sio muda mrefu taarifa itatoka katika vyombo vya habari hatua ambayo serikali imechukua kuhusiana na ripoti hii.

Lazima tuwe na subra ili na serikali nayo iifanyie kazi, kwa sababu Rais mwenyewe ameisoma ripoti ile *page by page*, sio kwamba ameidharau kuhakikisha kwamba anaielewa na vile vile atafakuri hatua za kuchukua. Kwa hivyo anayo, tumpe nafasi kabla serikali haijatoa maamuzi yake kutokana na ripoti ile.(*Makofi*).

Mhe. Spika, migogoro ya ardhi nayo imezungumzwa sana. Mpaka wengine walisema nilipoingia madarakani nilikuwa na nguvu, sasa hivi nguvu zimepungua. Lakini Mhe. Spika, (*Makofi*).

Mhe. Spika: Makofi hayo yalikuwa yanakupa muda unywe maji kidogo ili uendelee.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nikuhakikishieni kwamba nguvu hazijapungua, na kila patakapohitaji maamuzi yangu mimi, nitayatoa maamuzi yangu mimi kwa ufasaha na kadri Mwenyezi Mungu atakavyonielekeza.

Lakini tumekuja kugundua baadae ingekuwa mimi nimechukua hatua zile nilizokuwa nikizichukua ingekuwa hata ofisini sikai, maana migogoro hii ni mingi ya muda mrefu. Migogoro hii imetoka tokea miaka ya 1990. Sitegemei kwamba baada ya mwaka mmoja miwili tunaweza kuimaliza.

Lakini baada ya kugundua kwamba baadhi ya migogoro hii imesababishwa na sisi wenyewe, Masheha, Madiwani, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya. Ndipo Rais akatoa agizo kwamba sasa migogoro hii ishughulikiwe huko chini kwanza. Masheha, Madiwani, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wayashughulikie kwa sababu huko ndiko yaliko na wao ndio wanaojua chanzo chake.

Ndio maana yeye akatoa agizo pale patakapokushindeni nileteeni mwenyewe sasa. Haiwezi migogoro hii ikapelekwa juu wakati lazima yapatikane maelezo kutoka huku chini. Nyinyi ndio wenye maeneo. Historia ya maeneo hayo Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Masheha na Madiwani.

Kwa hivyo ni vyema utatuzi wa migogoro hii uanzie huko kwenye Wilaya, Mikoa, Shehia, Madiwani ili tuone namna gani tunakwenda. Taarifa nilizopata ni kwamba sehemu za Kusini naona kazi hii inafanywa vizuri na Rais anapelekewa taarifa. Sasa pale ambapo kazi haijafanyika vizuri katika eneo fulani lolote, basi tuje tuelezwe na sisi tutachukua hatua zinazopaswa. Lakini taarifa tulizonazo ni kwamba kazi aliyotoa Mhe. Rais inafanywa vizuri hasa katika Mkoa wa Kusini na hivi sasa kwa kutilia mkazo suala la kumaliza hii migogoro ya ardhi, hivi sasa Mhe. Rais ana semina na masheha, madiwani, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya. Miongoni mwa mambo mengine watakayozungumzia ni pamoja na suala la migogoro ya ardhi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala hili la migogoro ya ardhi bado halijatushinda serikali hii. Mimi nina uwezo kabisa wa kutoa maamuzi yoyote, mahali popote kadri imani yangu itakavyonielekeza. Kwa hivyo, hili suala tunalo na tutaendelea nalo, tupeane subra na kama kuna taarifa yoyote Mhe. Hamza Hassan Juma wewe niletee, hayo mapande manne yaliyogaiwa yako wapi, ili mimi niyafanyie kazi.

Mhe. Spika, ardhi ni mali ya serikali tangu lilipotolewa tangazo mwaka 1964 baada ya Mapinduzi kwamba ardhi ni mali ya serikali, hati zote zilizotolewa kabla ya Mapinduzi hizo hazifai tena. Kwa hivyo, Mhe. Asha Bakari Makame ardhi ina mwenyewe, ni mali ya serikali.

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia suala la ajali ya Spice Islander, nitowe pole na mimi kwa waathirika wote wa ajali hii. Ajali hii kweli imetupa tabu, imetupa masikitiko makubwa, lakini ndio jaalia ya Mwenyezi Mungu mwenyewe, hatuna cha kukifanya. Lakini Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ameeleza kwa kirefu hapa, kuhusu misaada iliyochangiwa na misaada iliyotolewa kwa wananchi walioathirika, na kama kuna mtu ambaye alipaswa apate msaada huu uliotolewa na wananchi wasamaria wema, basi aje atuambie na tukipata uthibitisho na yeye tutampa haki yake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, umeniletea ki-*note* hapa kwamba kuna mtu katika jimbo letu, basi wewe muachie aje kwangu, atuletee na ushahidi sisi tutampa msaada ambao anastahili kupewa. Kama atapewa kima cha chini kile ambacho sicho kilichopangwa. Kwa sababu Mhe. Waziri amesema hapa kwamba ni kiasi gani kwa waliofariki na kiasi gani kwa waliopona, *figure* zimeelezwa. Kama kuna mtu amepata chini ya hapo basi aje atuambie na kwa nini amepata kiasi hicho cha chini.

Mhe. Spika, katika ajali hii pia kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumza kwamba ni kiasi gani serikali ilichangia. Mhe. Spika, kwanza serikali ilichangia mazishi ya marehemu wote, yaligharimiwa na serikali. Pili, serikali ilitoa ubani kwa familia zilizoathirika zote kwa Unguja na Pemba. Mimi nilitoa kwa Unguja na Mhe. Rais na Makamo wa Kwanza wa Rais walikwenda kutoa kwa Pemba. Hizi hazikutoka katika mfuko wa msaada huu tuliopewa. Ubani huu ulikuwa ni kutoka katika mfuko wa serikali.

Pia serikali ilichangia gharama za ile tume iliyofanya uchunguzi, gharama zile zilitoka kwenye mfuko wa serikali, wala sio kwenye ule mfuko wa michango iliyotolewa na wasamaria wema. Kwa hivyo, hiyo ndiyo michango ambayo imetolewa na serikali kuhusiana na ajali hii tuliyoipata.

Kwa hivyo, suala la meli tuna uhakika kwamba ni jinsi gani tunajitahidi. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano jana alisema, zikatolewa taarifa ni namna gani serikali inavyojiandaa katika kutafuta meli kwa ajili ya usafiri kati ya Unguja na Pemba na Unguja na Dar es Salaam na sehemu nyengine. Tungependa wananchi wetu wasafiri katika chombo ambacho kina uhakika, na ni chombo kizuri ili wakati wote wa safari zao waweze kuona kwamba wako salama. Kwa hivyo, hiyo juhudi inafanywa na serikali kupata meli nyengine ya serikali ambayo itakidhi haja ya safari zetu baina ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitaka kulitolea ufafanuzi kidogo tu ni hizi safari za nje, ingawa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili amelisemea kwamba safari ya Marekani nilifuatana na watu wangapi, safari ya China nilifuatana na watu wangapi, kawataja. Lakini niseme tu kuna baadhi ya watu ninaofuatana nao hawalipiwi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wanalipiwa na ofisi zao.

Mhe. Spika, mfano nafuatana na watu kutoka Idara ya Mambo ya Nje, hawa wanalipiwa na wizara zao, sio SMZ inayowalipia. Lakini msione ule msururu mkubwa wa watu ninaofuatana nao mkafikiria wale wote, wale wengine ni lazima nifuatane nao. Kwa mfano, katibu wangu au naibu wake ni lazima nifuatane naye, kuna watu wa usalama ni lazima nifuatane nao na hao siwapangi mimi, wanapangwa kwa mujibu wa utaratibu wao wenyewe.

Kwa hivyo, huu msururu wa watu ninaofuatana nao wengine siwateui mimi. Ninaowateua mimi ni hawa ambao Mhe. Waziri aliwataja, pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hao ndio ninawateua mimi. Nasema mara hii nataka nifuatane na Mhe. Mshimba, mara hii nataka nifuatane na Mhe. fulani au Waziri fulani kwa mujibu wa maudhui ninayokwenda kuyafanya kule ninakokwenda. Lakini wengine kwa kweli napangiwa kwa mujibu wa wadhifa niliyokuwa nao sio amri yangu.

Hili Mhe. Spika, siwezi kulipinga, kwa sababu nikilipinga nikienda kule likanikuta jambo, nitaambiwa aah! Si ukaidi wako bwana, sisi tulikupangia hivi wewe ukakataa. Kwa hivyo, hilo liko nje ya uwezo wangu, lakini wale wanapangwa kwa mujibu wa utaratibu wa wahusika wenyewe.

Mhe. Spika, kuna mjumbe alisema vikosi maalum viundiwe wizara yake. Mhe. Spika, kuunda wizara. Wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi hapa walipiga kelele kwamba serikali hii tuliyokuwanayo ni kubwa, sasa wengine wanasema tuunde wizara nyengine. Ukisema tuunde wizara moja, hatuundi wizara moja tutaunda wizara mbili. Tufahamu kwamba kule tuna serikali ya umoja wa kitaifa, kwa hivyo tukiunda wizara moja itabidi tuitafute na nyengine, kwa sababu lazima mawaziri kutoka huku na huku watoke. Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Mshimba hili la vikosi tuliache kama lilivyo hivi sasa, halina madhara linafanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mimi nisingependa kuchukua muda mrefu kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais amefanya kazi nzuri, ameeleza mambo mengi. Tunajua yako mambo mengi sana, mengine kwa sababu watu waliochangia ni wengi, lakini mengine yale yote tunaweza kuyafanyia kazi kadiri tutakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo, kwa heshima na taadhima, isipokuwa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, waipitishe bajeti hii ili tuweze kufanya kazi vizuri, kwa uhakika na kwa ajili ya maslahi ya taifa letu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nichukue nafasi hii kukushukuru. Hoja Waheshimiwa Wajumbe, imetolewa. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu 0801	Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali	2,039,000
	Jumla ya Fungu	**2,039,000**

FUNGU 05 – OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Kifungu 003	Ofisi Kuu Pemba	357,256,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013. Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia hotuba hii. Kwanza naomba nimshukuru Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi mzuri pamoja na waziri wake katika ufafanuzi alioufanya.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia hotuba hii nilisema kwamba kuna umuhimu mkubwa wa serikali au kwa Baraza la Wawakilishi, kuandaa utaratibu maalum wa kwenda kupeleka elimu juu ya suala zima linalohusiana na mchakato wa katiba. Nilisema hivyo kwa hoja ya kwamba wakati nchi yetu ilipoingia katika mfumo huu wa serikali ya umoja wa kitaifa, Baraza letu kwa kuona umuhimu wake liliunda kamati ya watu sita Wawakilishi, ambao walifanya kazi nzuri sana kwa Unguja na Pemba na hatimaye wananchi tukaweza kuwashawishi na wakaileta

serikali hii. Tulifanya hivyo tukijua kwamba ndani ya serikali wako watu ambao walikuwa hawaitaki serikali ya umoja wa kitaifa, lakini kwa sababu serikali ilijenga *interest*, maana yake kwa kweli tukafuata *interest* ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alisema kwamba kuna watu wanajua Katiba. Mimi napingana naye kwamba kuna watu hadi hivi sasa hawaijui katiba ya Jamhuri ya Muungano. Wachilia mbali wananchi, hata sisi Wawakilishi hatuijui vizuri. *(Makofi).*

(Hapa ghafla umeme ulikatika)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, niendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Naona umeme utarudi hivi punde.

Waheshimiwa Wajumbe: tayari umesharudi.

(Baada ya dakika chache umeme ulirudi)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mbali ya wananchi, lakini nataka nikuthibitishie sisi Wawakilishi wako wengi wetu hatuijui vizuri hiyo Katiba ambayo tutakwenda kuitolea maoni. Lakini kama ikiwa wako wanaoijua. Nataka nikuambie Mhe. Mwenyekiti, kuna watu hawajui maana ya hivyo vifungu na kama kuna watu hawajui maana basi hawajui athari na faida zitokanazo na hivyo vifungu vya katiba.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, bado narudia hoja yangu kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa serikali ama chombo chetu hiki cha wananchi kuandaa utaratibu maalum wa kupeleka hoja hii kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Omar Ali Shehe kwa kutukumbushia jambo hili. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli elimu siku zote inasaidia na elimu ndio nguzo ya maendeleo kwa jamii yetu. Kwa kuwa jambo hili ni muhimu, Baraza lako tukufu iliiliona jambo hili. Nataka nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti na katibu wako kwa kuwasiliana na Ubalozi wa Norway na sasa naona mambo yanakwenda vizuri ili tupate fedha kwa ajili ya kutoa elimu kama hii. Kwa sababu ulishawasiliana na sisi, naona haya mambo ambayo anasema Mhe. Omar Ali Shehe na mawazo yako yanakwenda sambamba.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Omar Ali Shehe atupe muda ili tuweze kuliendeleza jambo hili, na kwa sababu Baraza linaandaa jambo hilo, naamini mambo yatakwenda vizuri na wajumbe watapata nafasi ya kupewa hiyo elimu ambayo inahitajika kutolewa. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kitu ambacho tulikuwa hatukijui, na sasa tumejua kwamba Norway itashirikiana na Baraza letu kwa ajili ya kuandaa programu hiyo. Nashukuru na naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Labda niongezee taarifa tu hapo, kwamba taarifa hii awali tuliitoa wakati wa *briefing* zetu. Nadhani jana tu mkataba umetiwa saini rasmi kwa ajili ya kazi hiyo ambayo Mhe. Waziri amejibu. Nilimuona Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kuniona. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hotuba hii nilizungumzia suala zima la migogoro ya ardhi, nilisema sana na nikamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hebu akubaliane na wazo langu la kwamba tuunde Kamati Teule juu ya migogoro ya ardhi.

Lakini hata Wajumbe wenzangu wengi waliochangia, wamechangia kitu hiki hiki cha migogoro ya ardhi, walithibitisha kwamba ipo migogoro na ipo mingi. Lakini hata majumuisho yaliyotolewa na Mhe. Waziri, mwenyewe amekiri hivyo. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amesema hivyo hivyo, kwamba migogoro hii ipo mingi na ya siku nyingi na inaendelea kuwepo. Sasa kwa kuzingatia hoja hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kwamba tuunde kamati, ili kuisaidia serikali katika kutatua migogoro hii, ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, maoni ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando sio mabaya. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara husika inakuja na hotuba ya bajeti na ina maelezo zaidi kuliko haya ambayo sisi tunayo, pengine maelezo yake yataweza kumridhisha Mhe. Mtando.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tuvute subira aisubiri wizara husika, aisikilize na ikiwa hakuridhika basi tutamuunga mkono mawazo yake Mhe. Mwenyekiti, naomba avute subira.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti pamoja na maelezo ya Mhe. Waziri, lakini bado hoja yangu mimi inasimama hapa hapa Mhe. Mwenyekiti. Kwa kuwa hili ni tatizo na hii migogoro iko ya aina nyingi, wacha migogoro tu kuna ufisadi mkubwa katika mambo ya ardhi. Mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Waziri anasema tusubiri wizara inayokuja. Mimi nakuomba basi kwa kupitia Baraza lako tukufu, tutumie kanuni ya 120 ili tuweze kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kwenda kutatua migogoro hii, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mtando, anahitaji kwa kutumia kanuni ya 120 kwamba Baraza liweze kuunda kamati teule kwa ajili ya jambo fulani, Kamati Teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na mjumbe na kuamuliwa na Baraza. Taarifa ya hoja hiyo haitajadiliwa. Kamati Teule itakuwa na wajumbe wasiopungua watano ambao watateuliwa na Spika, Mjumbe aliyependekeza kuundwa kwa kamati teule atakuwa miongoni mwa wajumbe wa kamati hiyo, lakini sio lazima kuwa Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Hayo ndio maelezo ambayo yako ndani ya kamati. Maelezo ya kamati kupitia kwa Mhe. Waziri ni kwamba migogoro hii ni mingi, jambo hilo amekiri na amekiri pia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kwamba migogoro hii imeandaliwa utaratibu na serikali. Kwanza ifanyiwe kazi katika huko ambako imeanzia kutokea. Jambo hili tukilitolea uamuzi hapa kwa kweli itatokea *precedent* ambayo kidogo ina matatizo. Kwa sababu hii Wizara kasma zake wala hazihusiani na ardhi hata moja, ni kwa sababu ya usimamizi wa serikali tu kwamba ndio ofisi inayosimamia serikali nzima. Sasa tukianza kutumia wizara hii kwa kuunda kamati teule za wizara nyengine, kwa kweli itakuwa hatuitendei haki sawa sawa.

Alichokisema Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa kweli hajakataa jambo hilo, lakini ni vyema tukasubiri wizara inayohusika ambayo nayo ina nafasi yake kwa kutoa maelezo, ili hatimaye baada ya hapo tuweze kujua nini cha kufanya baada ya maelezo ya wizara inayohusika. Nadhani hili liko wazi kabisa.
Kwa kweli hakuna kanuni inayosema hivi haya maneno ninayozungumza. Lakini ni mtiririko wa utaratibu wa shughuli za kawaida za serikali ndio unaeleza hivyo. Tukiruhusu hii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu pia angepasa hata kusema juu ya mambo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wizara ya Afya, mambo makubwa ya nchi hii wizara hii au ofisi hii inahusika. Nafikiri hapa tukubaliane kwamba tusubiri kwenye wizara inayohusika. Tuendelee, nilimuona Mhe. Mjumbe kasimama. Mbona mnasita sita, nataka nipate uchaguzi mzuri. Haya Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Aah! Samahani, haya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naona umenisahau badala ya kunipa ile haki yangu, angalau nikakubali yale maelezo yako ambayo umeyatoa. Nakubaliana na maelezo yako Mhe. Spika, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ilikuwa akoshe moyo tu kusema hivyo. Hii niliyopitikiwa namuomba radhi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala hili la athari ya baadhi ya *reaction* za ofisi hii inapotokezea matatizo kama hayo yaliyojitokeza karibuni.

Mhe. Spika, kabla sijazungumzia nukta yangu ambayo nataka kuizungumza, nataka nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa ufafanuzi wao mzuri. Nilimuandikia ki-*memo* Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kumwambia ameonesha *maturity* ya hali ya juu kabisa katika kulikabili suala hili na maelezo aliyoyatoa. Kwa hilo nampongeza sana hasa kwa kauli yake aliyoitoa mwisho, pale aliposema kwamba tusameheane, kwa sababu katika mambo kama haya mambo mengi yanakuwa yanajitokeza.

Lakini nukta yangu Mhe. Mwenyekiti, katika jumla ya ufafanuzi alioutoa Mhe. Waziri, alitamka kitu hapa ambacho mimi kidogo kimenipa wasi wasi kubakia katika kumbukumbu za Baraza bila ya kuwekwa sawa. Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake Mhe. Waziri alisema kwamba serikali haina dini. Sasa hili mimi kidogo linapohusu Zanzibar

linanipa matatizo. Mhe. Mwenyekiti, nataka kidogo mara nyengine tuwe waangalifu tusije tukachukua, kwa sababu tuna katiba mbili katika nchi yetu. Kuna katiba ya Jamhuri ya Muungano na katiba ya Zanzibar. Kwa hivyo, tusije tukatumia kitu ambacho kipo katika katiba ya Jamhuri ya Muungano, tukadhani kwamba kitakuwa kina-*apply* sawa sawa kote kuwili. Mhe. Mwenyekiti, nifahamike na hili nimuombe Mhe. Waziri tuliweke sawa.

Mhe. Mwenyekiti ukisoma katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 3(1), inasema "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa". Lakini ukitizama kifungu kinacholingana na hicho katika katiba ya Zanzibar, katika ibara ya 5, inasema "Zanzibar itafuata mfumo wa kidemokrasia ya vyama vingi vya siasa wenye kuheshimu utawala wa sheria, haki za binadamu, usawa, amani, haki na uadilifu".

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba hakuna sehemu yoyote ya katiba ya Zanzibar iliyotamka kama hivi ambavyo katiba ya Jamhuri ya Muungano imetamka. Ibara ya 19 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano na ibara ya 19 ya katiba ya Zanzibar, zote zinazungumzia uhuru na haki ya kuabudu, hapo zimetoa uwanja mpana kabisa kwamba kila mmoja kuwa na uhuru wa kuabudu anachokitaka na kubadilisha imani yake.

Lakini tunasema si vizuri kwa chombo kama hichi kukaa *record*, hasa tukitizama hata hicho kifungu cha 19 namna kilivyoandikwa ndani ya Katiba ya Zanzibar na ile ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuna tofauti ndogo, kwamba Katiba ya Zanzibar imeandikwa bila ya kuathiri sheria nyengine, kwa sababu tunajua kwamba katika utaratibu wetu wa Zanzibar. Kwa mfano, Mufti, Kadhi Mkuu wanachaguliwa au wanateuliwa na Rais wa Zanzibar.

Kwa hivyo, nataka hili tu Mhe. Waziri aliweke sawa, ili chombo hiki kisijekuingia kwenye *record* na kuharibu *tradition*, ambayo imekuwa ni msingi wa Zanzibar tokea kuwa na mfumo wa utawala katika nchi yetu, nilikuwa naomba marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi namheshimu sana ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nilivyosema kwamba serikali haina dini kwa maana haina dini rasmi iliyoandikwa kwenye Katiba yetu hii na tukatekeleza.

Lakini nakubaliana naye kwamba asilimia kubwa, zaidi ya asilimia 98 wananchi wa nchi hii ni Waislamu, na huo ni ukweli uwazi kabisa na sote tuliomo humu ndani nikiwemo na mimi ni Muislamu mzuri sana. Kwa kweli wapo ambao wengi wetu Mhe. Mwenyekiti lazima nibadilishe usemi wangu kwamba wengi wetu tuliomo humu ndani ni Waislamu. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile kama nilivyosema zaidi ya asilimia 98 ni Waislamu na mimi mwenyewe ni Muislamu, lakini kwenye kutekeleza majukumu yangu ya kiserikali sifuati Katiba ile kwa maana ya *Qur-an* Tukufu, lakini mimi mwenyewe naiamini, naheshimu pamoja na kuitekeleza *Qur-an*, lakini nchi yetu imetoa fursa hiyo na Katiba imesema kwamba kila mtu anao uhuru wa kuamini dini anayoitaka. Kwa hivyo, hakuna dini rasmi ambayo inayotuongoza kufanya shughuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye Mhe. Mjumbe kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar ni Waislamu, na utamaduni wao unaendana na mambo ya Kiislamu na wala hilo sina pingamizi nalo, tena naunga mkono yale aliyoyasema. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yake Mhe. Waziri na kwa sababu mwisho wa maelezo yake anasema kwamba anakubaliana na maelezo yangu. Nadhani hiyo itakuwa imesaidia kuweka *record* sahihi naomba tuendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba mniwie radhi ndio hali yenyewe hiyo. Tunaendelea na hoja tatu zimemalizika kwenye kifungu hiki.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 223,356,000/=
Kifungu 0501

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa tena nafasi hii. Katika mchango wangu kwenye eneo hili la Idara ya Uendeshaji na Utumishi nilihoji baadhi ya vifungu *specifically*, na niliomba maeneo, Mhe Mwenyekiti naomba kwa kifupi kabisa nivitaje.

Kwanza nilihoji katika kifungu 211100 kwenye mishahara ya fedha taslim kwenye kifungu kidogo cha 2111116 kuhusu Posho, Vikao na Kamati na nilisema hiki kimeongezeka sana kutoka shilingi milioni 1 mwaka jana hadi shilingi milioni 10,390,000/=.

Lakini nilipouliza hili nilimuomba Mhe. Waziri atakaponijibu alijibu kwa ujumla kwa nafasi yao kama ni Waratibu wa Shughuli zote za serikali na wizara nyengine, kwa sababu hili linaonekana limejirejea kwenye wizara nyingi.
Vile vile nilisema katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba tume-*consolidate* mishahara pamoja na marupurupu mengi. Lakini kumejengeka utamaduni ambapo hata wenzetu upande wa Bara unapigwa vita kwa nguvu sasa, hii tabia ya kujenga utamaduni wa posho za vikao kwa kazi ambazo ni zetu kikawaida ni sehemu ya wajibu wetu.

Kwa hivyo, bado naomba kutokana na maelezo yake Mhe. Waziri aliyoniambia kwamba kunakuwa na vikao vingi. Mimi naendelea kujiuliza je, ni sahihi kwa mtu ambaye analipwa mshahara pamoja na marupurupu mengine yote ambayo *consolidate* sasa, na mara nyingi wanaolipwa posho hizi ni watendaji wakuu katika maofisi haya, ni sahihi kuona fungu hilo bado maelezo yake hayakunitosheleza.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hiyo nilihoji maeneo mengine mawili, moja ni katika gharama za mafuta na vilainisho, pia nilisema kwamba mwaka jana imetoka shilingi 10,500,000/= hadi milioni 48,480,000/=. Katika majibu yake Mhe. Waziri aliniambia kwamba kumepanda gharama au bei ya *petrol*, *diesel* pamoja na gharama za maji na umeme.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia sikuridhika na maelezo yake, hivyo naomba anisaidie zaidi, kwa sababu pamoja na kuongezeka gharama hizo. Tunaishi hapa na tunajua kiwango kinachoongezeka, na wala haiingii akilini Mhe. Mwenyekiti kwamba wastani wa kupanda umetoka mwaka jana zihitajike shilingi milioni mbili kwenye *petrol* na mwaka huu zifike shilingi milioni 12, sidhani kama tumepandisha bei kiasi hicho.

Vile vile kwenye gharama za umeme pamoja na kwamba zimepanda siamini kuwa zimepanda kwa wastani kutoka shilingi milioni 6 mpaka iwe milioni 24 ambayo ni mara nne ya kiwango kilichokuwa mwaka jana, tunajua imeongezeka lakini haikuongezeka hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hoja yangu katika kifungu nilichokihoji cha ununuzi wa Magazeti kwenye *vote* ya 220500, ambapo nilisema kwamba imetoka milioni 2,150,000/= hadi milioni 8,820,000/=. Kwa kweli siamini kwa kipindi cha mwaka mmoja kwamba kumeongezeka magazeti mengi kiasi hicho, na bei ya magazeti imeongezeka kiasi hicho cha kufanya bajeti hii ipande mara nne ya bajeti iliyokusudiwa.

Kwa hivyo, bado naomba maelezo ya Mhe. Waziri kwa nini nipitishe vifungu hivi wakati kuna ongezeko kubwa sana, na kama tunavyojua watendaji wetu wengi wamekuwa wakitumia vifungu hivi vibaya Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nilimuona Mhe. Ismail Jussa Ladhu peke yake na kumuachia aende kwenye hoja tatu kwenye fungu lile.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa imani yake kubwa ya nchi hii na kuona matumizi yanatumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha kuna matengenezo ya *magari* yamefanyika wizarani kwetu yameongezeka, pia tunao utaratibu wa kununua gari mpya umeongezeka. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti gharama hizi zinaongezeka na huko nyuma Mhe. Mwenyekiti nilisema kwamba unaweza kuweka fungu likaonekana shilingi milioni 10,500,000/= lakini baadaye unahaulisha na kuja kiwango hiki ambacho leo kinaonekana hapa.

Kwa kweli tatizo letu huko nyuma tulikuwa hatuna utaratibu mzuri unaotoa mwanga sahihi kama tulionao leo baada ya kuwa Mpango huu wa Bango Kitita, yaani *reallocations* zilikuwa nyingi, sasa ku-*avoid* kuhaulisha na shughuli

zifanyike ndio maana tukaja na kiwango hiki. Mhe. Mwenyekiti, nia yetu si kutumia zaidi, isipokuwa nia yetu ndio ukweli halisi wa mahitaji yaliopo sasa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu akaliona hili, kwa sababu akituzuia tutapata namna ya kufanya uhaulishaji na matokeo yake kwenye Bango Kitita unaonekana umezidi kiwango kile ulichotengewa. Mhe. Mwenyekiti, ukweli shilingi milioni 48 kwa gharama za mafuta, *diesel*, maji pamoja na mambo mengine utaona kwamba *grease*, *service* na kadhalika, fedha hizo kwa wizara utaziona kwamba zitafikia. Hilo la kwanza.

Pili Mhe. Mwenyekiti, sisi tunajenga jengo jipya na tutahamia mwakani na zile wizara ambazo zilizokuwa zikikodi na kulipa fedha nyingi zaidi, yaani tutatumia karibu shilingi milioni 300 na watakuja kuhamia kwenye jengo jipya. Kwa mfano, umeme uliokuwa ukitumiwa na Idara ya Maafa, Sherehe na Mapambo sasa utatumika kwenye Makao Makuu kwa pamoja, kwa hiyo gharama za umeme zitaongezeka na kukua tu kwa vyovyote vile, kwa maana hiyo tunakuja kwenye uhalisia wake kutokana na ukweli ulivyo.

Halikadhalika magazeti Mhe. Mwenyekiti akitaka mimi kaka yake nisisome magazeti sina la kufanya, nitakuwa sisomi na itakuwa sipati taarifa na shughuli yetu Mhe. Mwenyekiti ya wizara yetu ni *coordination* na inahitajika sana kujua haya mambo.

Sasa Mhe. Mjumbe ukinifikisha hapo sina vya kufanya ndio uamuzi, lakini ukweli ni kwamba fedha hizi tunazihitajia kwa ajili ya kufanya kazi, vyenginevyo ananifunga kamba ya kufanya wajibu wangu vizuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia maelezo ya Mhe. Waziri na ninataka nimhakikishie kwamba sina lengo la kumfunga kamba, ili asiweze kufanya shughuli zake hasa ilivyokuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ni kaka yangu mpenzi sana. Lakini maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri bado siridhiki nayo, kwa sababu moja tu.

Anapotoa hoja kwamba inajumuisha gharama za matengenezo nataka nimkumbushe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hiyo kuna fungu lake mbali tena kwenye Idara hiyo hiyo na iko kwenye vote 220800 matengenezo ya Zana, na ukija kwenye *sub vote* kuna matengenezo ya magari, vifaa vya magari, gharama za Bima na leseni ya njia na hayo tayari yako kwenye fungu lake, nimedhani labda anayo maelezo ya kutosheleza zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nionekane labda ni mkorofi kwa hili nalikubali, lakini kwa hoja moja kwamba kwa sababu moja katika kazi zetu kwenye kamati ni kukagua *value for money*, thamani ya fedha ambayo inaidhinishwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niiombe sana Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Kamati nyengine zote, kuanzia sasa tunatumia buku hili wakati tunapokwenda kukagua, ili tujiridhishe kwamba matumizi haya ambayo tumeyapitisha hapa kwa niaba ya wananchi masikini, walipa kodi wa nchi hii, kweli yanatumika kwa shughuli zilizokusudiwa ama yanaishia mifukoni kwa wajanja wachache. Baada ya maelezo hayo, Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunakushukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ulituambia mapema kwamba ukaguzi utakuwa *strict* zaidi, na nzuri zaidi kuhakikisha fedha za wananchi zinahifadhiwa. Ahsante, tunaendelea.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi 866,184,000/=

Kifungu 0601

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia niliuliza mambo matatu katika kifungu hiki. Kwanza kwamba mishahara ya Idara hii imeipita mishahara ya Idara ya Uendeshaji na Mipango. Sasa nataka kufahamu kwamba je, idara hii ambayo shughuli zake sio nyingi kiasi hicho ukilinganisha na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye watumishi wengi zaidi kuliko hao na swali hili halikujibiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti anipe ufafanuzi.

Vile vile ilisema ikiwa wako kiasi hicho je, katika hali hii tunayokwenda nayo tunawahitaji watu wa aina hiyo, kwamba kitengo ambacho kinangojea sherehe au mambo mengine madogo madogo kuajiri watu wengi sana, wakati hivi sasa tunao utaratibu wa kuwachukua watu binafsi na viko vikundi vingi.

Pili ilikuwa kuhusu hii posho maalum ambayo inajitokeza sehemu nyingi na wala sio hapa tu. Je, ule utaratibu wa Wizara ya Fedha ku-*consolidate* mishahara umeshaondoka kwenye utaratibu. Kwa hivyo, hizi posho maalum Mhe. Waziri katika majibu yake alitaja tu, kwamba hii milioni 20 ni posho maalum kwa sababu wanakaa usiku na jioni.

Lakini tulivyoambiwa kwamba posho zimeingizwa kwenye mishahara moja kwa moja, sasa ule utaratibu umeondoshwa hata ikawa posho maalum sasa inawekwa kifungu mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi pia nimshukuru Mhe. Rashid Seif Suleiman. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba Baraza lako tukufu hili lina Wajumbe wa Baraza mahiri, makini ambao wako tayari kuitumikia nchi hii, kwa kweli hii yote ni mifano hai ya kwamba Waheshimiwa Wajumbe wako macho na wanaisimamia serikali vizuri, ili tupate manufaa na maendeleo na mimi naunga mkono kwa wanayoyasema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nia ni kuimarisha uwajibikaji wetu, kufanya mambo kwa kiwango, ili tukidhi haja yetu, tunataka tuwe na Idara hii ya Sherehe na Mapambo inayofanya wajibu wake vizuri. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi walioajiriwa wote ni 14 na kazi zao si kidogo, kwa sababu wanafanya shughuli za sherehe, maadhimisho, mapambo kwenye mikutano yetu na viongozi. Kwa hiyo, hawa watu 14 walioajiriwa walionekana kwamba wangetosheleza. Mhe. Mwenyekiti, tunachokihitaji ni kwamba nchi yetu ifanye vizuri katika mambo mbali mbali.

Vile vile nilisema hapa kwamba watu 14 hawa mishahara yao ni shilingi milioni 3,500,000/= kwa mwezi, na kwa mwaka utaona inakuja kama shilingi milioni 42,000,000/= na shilingi milioni 5,000,000/= ni *ZSSF* na hizo shilingi milioni 20,000,000/= ndio posho maalum, na siku hizi hakuna kitakachotolewa kinyume na utaratibu, kwa sababu taratibu lazima zinafuatwa na *breakdown* ya wizara lazima ioneshe haya ndiyo yanayotumika kwa ajili ya kazi hizi.

Kwa kweli wenzetu hawa wakati wa shughuli za sherehe Mhe. Mwenyekiti wanafanyakazi mpaka usiku, wakati mwengine wanafanyakazi ikiwa shughuli iko Dar-es-Salaam au Pemba inabidi waende, kwa hiyo lazima kuwe na posho ya kuwahudumia hao vyenginevyo haitowezekana, ndio hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, labda tuseme yanapoandikwa haya mabuku serikali iwe macho, kwa sababu hapa katika fungu hili inaeleza mishahara ya mwaka jana 2011/2012 ilikuwa ni shilingi milioni 3620/=, lakini mwaka 2012/2013 imepanda mpaka shilingi milioni 43,650/=. Sasa ndio haifahamiki kwamba wameajiri watu wengi kiasi hicho mpaka kutoka shilingi milioni 3 mpaka shilingi milioni 43, kwa sababu *column* inaonesha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa maelezo ya Mhe. waziri ni hivyo, basi nadhani serikali ikakae kitako tena kwa ajili ya kuandika mabuku haya, na wala wasituletee *figure* ambazo haziwezi kuingia akilini, kwa sababu kila kitu kinapanda na ukiuliza maelezo hayatoshelezi.

Kwa hivyo, tunaweza kukaa hapa mpaka kesho, lakini sisi haituingii akilini kwamba mshahara utoke shilingi milioni 3620/= pamoja na kupanda kwa mishahara au wenzetu wamepandishiwa kwa asilimia 500 wakati wafanyakazi wa kawaida wamepandishiwa kwa shilingi 20,000/= tutizame.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti ninalosema hizi idara ambazo zinafanya kazi kwa kipindi basi serikali ipunguze matumizi, ili waweze kuajiriwa watu kidogo na waweze kuwa *efficient*. Kwa kweli hapa maelezo ya kutosha hayapo Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa mimi nitakiruhusu hiki kifungu kipite kwa heshima ya Makamo wa Pili wa Rais tu, na wala hakuna maelezo. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe, Rashid Seif Suleiman. Lakini Idara hii ni mpya ambayo inaundwa sasa na wala huko nyuma haikuwepo hii, sasa ndio imeanza na kuna Idara rasmi ya kushughulikia masuala ya Sherehe na Mapambo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa zamani tulikuwa tukichukua wafanyakazi kutoka wizara tofatuti na hao pia kulikuwa na utaratibu wao wa malipo, na pengine ulikuwa mkubwa zaidi kuliko huu wa sasa, hivyo sasa tunacho kitu pahala pamoja na kinachofanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake hawa tunaowaajiri tukishanunua na vifaa basi watazalisha hawa, na *Inshaallah* mwakani mutaona matokeo yake na mwanzo hawakuwepo kama hivi na sasa ndio ukaona ndivyo ilivyo. Kwa hivyo, naomba nimshukuru pamoja na kumfahamisha hayo zaidi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0601 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa 868,375,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Huduma za Makamo wa Pili wa Rais 365,223,000/=
Kifungu 0801 Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa
Mkuu wa Serikali 512,555,000/=

Kifungu 1901

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri wangu pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nimeona kuna suala ambalo ameliacha, basi ni vyema kunisaidia.

Mhe. Waziri amekubaliana na suala la mambo ya askari kwamba tutaletewa Sakina mpya pamoja na nyumba, pamoja na matatizo mengine ya askari atayafuatilia nampa pongezi.

Lakini kuna suala ambalo ni muhimu sana amelisahau hivyo naomba anitolee kauli, na suala lenyewe nilisema kuwa kutokana na muundo wa hivi sasa kati ya Kamishna ya *IGP* kutuundia Polisi Jamii, nilisema je serikali nayo inatoa kauli gani kuhusu kuikubali. Sasa leo wenye Polisi Jamii wako chini ya television wanasikiliza kauli ya serikali wameipokea vipi Polisi Jamii. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo la muda katika kueleza, kwa sababu kwenye orodha yangu ilikuwa na hili nilieleze. Kwanza Kauli ya Serikali inaunga mkono Polisi Jamii na tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya na waendelee kuifanya na serikali nayo itashirikiana na Jeshi la Polisi kuona uwezekano wa kuimarisha Polisi Jamii. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa mawazo yake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, naomba msomaji atoe sauti kwa sababu mimi nimeshapitwa na mambo mengi na hata sikujua nipige buti wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sina azma ya kuzuia, lakini katika uchangiaji kwa sababu nimeona hapa huduma za Makamo wa Pili wa Rais. Wakati nilipokuwa nikichangia nilitoa maelezo kwamba tulitoa gharama serikali kuwapeleka watu nje ya kwenda kusoma namna gani wenzetu wanafanya kazi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Vile vile nilielezea na niliomba ofisi hii kwanza iwape mafunzo Wajumbe wake wa Baraza la Wawakilishi, kwamba tuelimishwe ni namna gani tunatakiwa na sisi tuendeshe mambo yetu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa naona hii huduma ya Makamo wa Pili wa Rais inielezee kwani humu kuna safari za nje, za ndani pamoja na mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani ni Idara ya Uratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa nimemfahamu vizuri Mhe. Asha Bakari Makame, dada yangu, mpenzi wangu ni kwamba mafunzo yapatikane kwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuhusu suala zima la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, nadhani kwenye ile *Program* ya Norway *component* hiyo itakuwa imo ya kuwataalimisha Waheshimiwa Wajumbe wetu, na wala hilo silioni kuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Baraza la Wawakilishi limeongezewa fungu kidogo kwa namna nzima Waheshimiwa Wajumbe wetu kupata mafunzo na kujitaalamisha zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nia yetu huko

mbele asili ya kutaka Sheria ya Utawala wa Baraza tupate fursa zaidi, ili mambo haya yafanyike vizuri zaidi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Asha Bakari Makame atusubirie, wakati nia ni kufanya shughuli ambazo amezitaja na ninamshukuru sana kwa kutukumbusha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Bakari Makame, nadhani Mhe. Waziri amekuridhisha.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sikusikia hasa vile alivyosema kwamba kweli itakuwepo na amezungumzia Baraza la Wawakilishi namna gani mfumo ambao tumepata kwa baadhi ya mafunzo. Lakini kwa Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa sababu yeye ndio mdhamini mkuu wa serikali tunataka ofisi yake itupe mafunzo kwa wale watu ambao walisafiri. Kwa upande wetu wa Baraza tunajua kwamba tunazo semina zetu mbali mbali.

Sasa nataka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ije ituweke, na wala si semina ya siku moja ije ituweke siku mbili hapo, kwa ajili ya kutupa mafunzo, ili tujue kitu gani tunafanya katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa vizuri dada yangu mpenzi Mhe. Asha Bakari Makame, anachotaka ni kwamba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itoe Semina maalum kwa Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ijapokuwa katika bajeti ya mwaka huu hatuna fungu la namna hiyo lakini kauli iliyotolewa na mjumbe namna hii mzito, lazima tukate pua tuunge wajihi tutafute namna mpaka Semina ifanyike. Na nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ili na mimi nikae vizuri Mhe. Mwenyekiti, naomba tu nikumbushe, tupo katika fungu 1901 la Idara ya Utumishi. Katika mchango wangu na michango mengine mingi ya wajumbe wakati tukijadili shughuli za idara hii tuligusia suala la vikao vya pamoja vya mashauriano, baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano kutatua kero za muungano ambavyo havileti tija yoyote.

Wajumbe wengi tulitoa hoja kwamba vikao hivi kwa upande wetu Zanzibar visitishwe kwa sababu havileti tija yoyote. Mhe. Waziri katika maelezo yake katuomba sana na katunasihi kwa kutumia maarifa yote ya Jimbo la Wawi kwamba tukubali kwamba mazungumzo yaendelee.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huko nyuma nilishiriki sana katika mazungumzo takriban yote mpaka yaliyopelekea kupatikana Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa hivyo sitaki kukataa mazungumzo. Lakini mara nyengine Mhe. Mwenyekiti, wanasema ndaro ni sehemu ya vita na ndaro inasaidia sana. Mimi sitaki nimkatalie Mhe. Waziri maelezo yake aliyotwambia kwamba wanapokwenda kule wanazungumza kwa hisia zote. Mimi nawaamini kabisa Mawaziri wetu, lakini katika hili mimi nataka leo Baraza lifanye maamuzi yatakayopeleka ujumbe ili angalau moja kubwa lilowagusa Wazanzibari litatuke ndani ya mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika maamuzi ambayo yaliyopitishwa ndani ya chombo hichi ni kuliondoa suala la mafuta na gesi katika mambo ya muungano. Hili limeshachukua miaka mitatu hadi sasa na hoja sasa hivi imeshakuwa kikapu cha kutumbukiza kila kitu kwamba tungoje Katiba mpya. Katiba mpya Mhe. Mwenyekiti, hatujui itamalizika lini kwa sababu tunaweza tukaipangia muda wenzetu Kenya walichukua miaka karibu kuliko waliyotarajia mwanzo.

Kwa hivyo katika hili mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri atukubalie kwamba tutoe tamko hapa na yeye atoe tamko kwa niaba yetu, kwamba vikao hivi kwa Zanzibar tunavisitisha mpaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakapochukua hatua ya kupeleka Marekebisho ya Katiba kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia ndani ya mwaka huu katika orodha ya mambo ya muungano. Halafu hapo tutaendelea na mambo mengine. Ahsante sana Mheshimiwa naomba kauli ya Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Ndugu yangu Mhe. Jussa, yote hayo ni mapenzi ya Zanzibar. Nakubaliana naye ndaro ni sehemu ya mafanikio katika mazungumzo. Nilijifunza mengi wakati tukizungumzia suala la kutafuta muafaka wa pili Mhe. Jussa kwake namjua umakini wake kwenye mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika mazungumzo yetu yapo mambo tulifanikiwa kwenye mazungumzo yetu na yakapata majibu vizuri. Kwa mfano:

- Uvuvi wa Ukanda wa Bahari Kuu.
- Mambo ya uwezo wa SMZ kukopa ndani na nje ya nchi.
- Lalamiko la wafanyabiashara japo lina matatizo bado lakini tumefikia hatua nzuri na tutalifikia pahala pazuri na mengine mengine mengi ambayo naamini tutafikia pazuri.
- Kuhusu ajira kwenye taasisi za muungano tumekwenda vizuri na baadhi ya mambo mengine.
- Mgawanyo wa mapato yanayotokanayo na misaada bado mazungumzo yanaendelea vizuri.

Kwa hiyo yapo mambo ya msingi ambayo yamefikia ukingoni, tukiyaacha njiani tunaweza kuharibikiwa zaidi. Tuwe na busara hii peke yake hapa si ndaro ndogo, tutayachukua haya kwenda kuyasema bajeti kasoro isipite kwa wenzetu. Na hili la mafuta Mhe. Mwenyekiti, sipendi nitoe ahadi mbele ya kikao hichi kitukufu, lakini ninavyojua mimi tumefikia pazuri. Hebu wajumbe watupe nafasi kidogo, hizi ndaro zilizopita sio ndogo. Mwenyemasikio anasikia na mwenye macho anaona, naamini miye haya yote tunayoyasema hapa masikio yote yapo Zanzibar hasa siku ya leo.

Mimi naamini ndaro zilizotokea na ukweli hasa uliofanyika katika Baraza hili naamini na hatua zaidi tutakwenda. Mimi nafikiri tutumie hekma na busara zaidi kwa hapa tulipofikia. Hasa hasa ukitizama na mchakato huu wa kusikiliza maoni. Naamini kabisa yapo mabadiliko yatatokea makubwa sana. Nawaombeni Waheshimiwa wenzangu tuungeni mkono tulimalize na hili. Sisi bado tutumie busara za Uzanzibari, hekma za Uzanzibari ili *massage sent*. Mhe. Jussa nakuomba na hili kama ulivyotukubalia yaliyopita na hili tukubalie tuendelee na wenzetu wote Wajumbe wa Baraza hili tukufu ili tumalize mchakato wetu vizuri. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyosema namuelewa sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Na namuelewa sana kama alivyosema mwenyewe katika maelezo yake pale kwamba kwa maumbile yake yeye si mtu anaependa mivutano na mimi nataka nimuhakikishie kwamba sote hatupendi mivutano, lakini mara nyengine katika kudai chako inabidi kama nilivyosema angalau upige ndaro.

Kazungumzia sana na kajitahidi kwetu kutumia hekma na busara. Lakini hekma ikiwa ipo upande mmoja na busara ikiwa ipo upande mmoja tu haisaidii. Wazungu wanasema ikiwa wewe utacheza peke yako mwengine hachezi lengo halipatikani hivyo. Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, kasema masikio yapo hapa, macho yapo hapa, mwenye macho ataona na mwenye masikio atasikia. Na mimi namuonesha katika *Qur-an* inasema kuna watu "*sumun, bukumun, umyun, fahum la-yarjiuun*." Wana macho hawaoni, wana masikio hawasiki, wana midomo hawasemi mabubu, wala hawarejei. Na kuna sehemu yengine inasema "*Fahum la -yaakilun*" na wala hawana akili.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema katika hili imefika pahala sasa tutoe kauli zetu. Mhe. Mwenyekiti, hili nalisimamia sana kuliko lile la mwanzo kwa sababu moja tu. Hili lina maamuzi ya chombo hichi katika kutunza heshma ya chombo hichi. Huko nje watu wanatuhoji wapiga kura tunaowawakilisha hapa ambao ni wananchi. Wanatwambia mna maana gani nyie ikiwa mnapitisha maamuzi miaka mitatu leo hayajatekelezwa. Kwa nini mnapoteza fedha zetu za walipa kodi kukaa kujadili hayo. Tunaulizwa hayo Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo katika hili kama kuna nia kama alivyotwambia yeye nasema basi nia njema tutaiona. Kwa sababu sijazuia vikao kama sheria inavyosema kwamba tuvisitishe mpaka tuone hatua. Katwambia kuna nia njema, basi kama ipo hiyo nia njema tutaiyona. Tuvisitishe mpaka tufike hatua ya kuchukuliwa marekebisho ya Katiba kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia ndani ya mwaka huu fedha. Hapo ndipo tutakapokubali vikao hivi viendelee. Vyenginevyo turuhusu fedha za walipa kodi wa Zanzibari kwenda katika vikao visivyokwisha ambavyo havina tija. Ningekuwa na muda ningekuwa sitaki kufungua mjadala mpya hapa. Ningemthibitishia ile orodha ya kero za muungano, yapo mambo zaidi ya matano hatujafika popote ni maneno tu. Katika hili naomba Baraza hili litoe ujumbe mzito kupitia kamati hii, Waziri atoe kauli hiyo ili wenzetu wapate ujumbe kwamba sasa tumechoka. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hakuna kazi ngumu kama kujibizana na mwanasheria, maana mwanasheria ana sifa ya uwakili huyu na anayoyasema yote ya msingi kabisa kabisa. Naamini hayo yote yanayosikilikana hao wenzetu wameshayasikia wanajua kabisa kwamba si kazi rahisi kwa hali ilikwisha kufikia. Nafikiri kila mmoja ameelewa na hata baadhi ya Wabunge katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano

wanalizungumzia jambo hili. Wameshaona dalili za uwezo na umahiri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na namna wanavyosimamia haki za Wazanzibari na ni wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tena na namuomba sana na kumnasihi kwa hatua tuliyokwisha kufikia ni vizuri kabisa tukaendelea. Haya anayoyasema kwa imani yangu yatafanyika muda sio mrefu. Sipendi nitoe ahadi hapa lakini Mhe. Mwenyekiti nayajua na yameshafikia hatua nzuri tena nzuri sana.

Naomba tusimnyanyue Makamo wa Pili wa Rais bure, kwa sababu naamini Mhe. Jussa ukituhurumia kwa hili na ujumbe huu umeshafika, umeshatuwekea base nzuri sana ya kujenga hoja ya kumalizia mambo haya. Bora twende tukayamalizie haya na hili madhali limeshaamuliwa na Zanzibar na Serikali yetu na Baraza hili tukufu hili ni lazima litatoka. Mimi nataka niwahakikishie Wazanzibari litatoka na halina muda tena. Mwenyezi Mungu yupo atatusaidia tutamaliza jambo hili vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa unapotoa maelezo au kutaka maelezo zaidi kwa serikali naomba uzingatie jambo moja na kwa kweli tuzingatie sote Waheshimiwa Wajumbe. Tume imeundwa, itachukua maoni kutoka kwa wananchi. Lakini serikali kwa sababu ya kuunda Tume Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakifika pahala wakisema kwamba jambo hili tunalimaliza kuanzia kesho, maana yake ni kwamba Tume itasema kwamba sivyo au hilo tulikatae. Kwa hivyo nafikiri tukisitisha vikao hivi tunazuia Serikali zetu mbili kuweza kufikia baadhi ya mambo ambayo pengine mashauri yake yametoka humu ndani. Nilikuwa nafikiri hivyo.

Nadhani Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mhe. Jussa tuzingatie hilo kwamba tusizi *cripple* serikali zetu mbili kuweza kuchukua hatua kwa yale ambayo wanaona yanaweza kuchukuliwa hatua.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niruhusu nikuombee umri mrefu na siha uendelee kutuongoza kwa hekma na busara katika Baraza hili. Katika watu ambao wanaji- *proud* Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa na Spika ambaye analisaidia sana Baraza hili basi mmoja ni mjumbe wako miye na naamini na wajumbe wako wengine wote katika hapa.

Kwa hivyo kwa kukuheshimu maelezo yako na kwa kumuheshimu Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu ni kiongozi wetu mkubwa huyu. Nakubali lakini niseme kabla ya kukaa chini Mhe. Mwenyekiti niseme kitu kimoja. Huu tukijaaliwa ndio mwaka wa mwisho nadhani kwa Baraza hili nitawashawishi wenzangu kupitisha fungu hili la Idara ya Uratibu kwa Mambo ya Muungano ikiwa mwakani tutarudi hapa tukaambiwa bado hakuna ufumbuzi katika suala hili.

Na nataka ieleweke Mhe. Mwenyekiti kwa sababu hapa tunasema na wananchi wetu vile vile. Hii haina maana kwamba tutachukua hatua nyengine katika suala la mafuta, inakuja Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wajiandae tena nawambia wajiandae vizuri kweli kweli katika hili. Kuna hatua tutachukua kama Zanzibar ili kusukuma maamuzi yetu. Lakini katika hili la kufanya marekebisho ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano nakubali lakini nasema kama halikupatiwa ufumbuzi tukijaaliwa mwakani hapa hapana bajeti ya Idara ya Uratibu mpaka suala hili tulijue mwisho wake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1901 Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ 346,377,000
Kigungu 2001 Idara ya Maafa

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niendelee kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyokuwa na busara na majibu mazuri mbele ya Baraza hili. Nilimuomba ili kusaidia serikali katika wale wajanja wachache ambao wanapenda kula pesa za wale wahanga. Basi tupatiwe orodha ya wale waliofaidika kwa kupata msaada ule wa serikali kila jimbo ili tuweze kuisaidia serikali kuweza kuwabaini wale wajanja ambao pengine watajipenyeza wasiweze kujipenyeza.

Namuomba Mhe. Waziri atupatie orodha ya wale marehemu na waathirika waliohai ambao wanafaidika ili kuzuia wale wajanja kujifaya wamekufa. Kuna mtu mmoja aliwahi kujitangaza yeye mwenyewe kama amekufa kumbe yupo hai kwa ajili ya kupata maslahi. Namuomba Mhe. Waziri atusaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo Wapili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. Mheshimiwa kwa sababu kazi hii tayari imefanyika sasa wajibu wetu ni kugawa tu ile orodha. Kwa sababu kabla ya kwenda kule kuwapelekea Wakuu wa Wilaya kuwapelekea kwenye Shehia ile orodha yenyewe. Orodha zipo, tutachukua hatua, ziwafikie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wajue katika kila Shehia nani na nani kapata na nani hajapata na utaratibu unaoendelea. Tutafanya hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2001 Idara ya Maafa	210,674,000
Jumla ya Fungu	**3,750,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0201 Utawala Unguja	10,392,327,000
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	1,987,859,000
Jumla ya Fungu	**12,380,186,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 30 – TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nilipokuwa nikichangia na bahati nzuri nilipata wasindikizaji, kwamba hii Tume ya Uchaguzi imeshakuwa ni mwaka wa pili tokea kumalizika kwa uchaguzi sasa hivi. Lakini sijasikia harakati zozote za kuandikisha watu wapya ambao wanatimia umri wa miaka 18.

Suala langu lilikuwa je, tutaingojea mpaka lini hii Tume ya Uchaguzi tukiipa fedha zetu kila mwaka halafu waje watupangie misongo. Hebu Mhe. Waziri atwambie hasa itaanza kazi lini naona katika maelezo yake alikuwa kapita juu juu tu lakini hakutwambia hasa kwamba itaanza kazi lini ya kuongeza wapiga kura wapya, wakati kuna majimbo yanafanya uchaguzi, kuna uchaguzi huu wa kura ya maoni unakuja. Sasa tueleze hii Tume ya Uchaguzi kwa nini ikatumia fedha zetu bure.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo Wapili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe. Sasa hivi inaonekana wazi kwamba hata ikipita Bajeti ni lazima uwe makini. Hii wanatwambia kwamba tuwe makini zaidi. Tunawashukuru sana kwa kutukumbusha na tutajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mwaka huu wa fedha Daftari la Kudumu la wapiga kura litaanza kuendelea na shughuli zake. Kwa hiyo mara tu tutakapomaliza bajeti yetu hii Tume itaendelea na utaratibu huo mapema iwezekanavyo ili kila mwaka kuanzia mwaka huu utaratibu usisimame na utaendelea vizuri.

Nataka niwahakikishie kwamba jambo hili limepewa kipaumbele na serikali na Rais mwenyewe na limeshatolewa muongozo ili Tume hii iweze kufanya kazi zake vizuri. Mheshimiwa naomba aelewe kwamba jambo hili litafanyiwa kazi vizuri sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu kama ingelikuwa kama hakutoa maelezo hayo ingelikuwa ni vigumu Mheshimiwa kwa Baraza hili, kukaa miaka mitano ikawa unawalipa watu ambao hawafanyi kazi zaidi ya kungoja uchaguzi 2015.
Naomba tuendelee kwa maana kwamba hayo maelezo yake yatatekelezwa.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	898,700,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	185,300,000
Jumla ya Fungu		**1,084,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 05 – AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Kifungu 1901	Idara ya Uratib wa Shughuli za SMZ	3,872,400,000	
Kifungu 2001	Idara ya Maafa		674,000,000
Jumla ya Fungu			**4,546,400,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizibila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 – BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0102	Utawala Unguja	605,424,000
Jumla ya Fungu		**605,424,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko. Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako iyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa mliyoyatoa kwa serikali, baki kwa mashirikiano makubwa mliyotoa kwa kiti ili kuendesha shughuli hii kwa mafanikio. Naomba sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili, kuchangia na hatimae liweze kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana leo hii katika Baraza hili tukufu, kwa lengo la kujadili masuala muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kazi ya kuwahudumia wananchi. Utaratibu aliouanzisha wa kukutana na taasisi za Serikali na kupokea taarifa za utekelezaji wa kila robo mwaka una madhumuni ya kukuza ufanisi katika utendaji wa shughuli za Serikali ili kuweza kuwatumikia wananchi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, vile vile sina budi kuwapongeza viongozi wetu wa kitaifa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zao za kumsaidia Mhe. Rais kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Mwaka mmoja wa utekelezaji wa bajeti umeonesha dhahiri umahiri na umakini walionao viongozi wetu hao.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Mhe, Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Ofisi hii, kwa ushauri wake na miongozo anayonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Kwa hakika busara, hekima na uwezo wake wa kusimamia majukumu yake, yananipa muongozo juu ya namna bora ya kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu yangu. Naendelea kumuhakikishia kuwa nitajitahidi kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha kusimamia vizuri majukumu yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, napenda pia uniruhusu kukupongeza wewe binafsi na wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kufuatana na sheria na kanuni za Baraza zikichangiwa na hekima na uadilifu mulionao. Umahiri wa utendaji kazi wenu unadhihirisha wazi pale inapotokea mijadala mizito na ikafikia maamuzi muwafaka.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mheshimiwa Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kwa kufanya nao kazi kwa mashirikiano makubwa. Kwa hakika Ofisi yetu inathamini sana michango, ushauri na maelekezo mbali mbali wanayotupa ambayo sio tu husaidia kutupatia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu lakini pia hutuwezesha kukabiliana na changamoto zinazotukabili.

Mhe. Spika, pia napenda kuwashukuru wajumbe wenzangu wa Baraza hili Tukufu la Wawakilishi, kwa kutoa ushirikiano wao wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa Ofisi yetu tukiwa ndani ya Baraza na hata katika majimbo yao.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu. Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa juhudi, bidii na ustahamilivu katika kutekeleza majukumu yao ya kazi na kuleta ufanisi na tija kwa Taifa.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu kwa ustahamilivu wao na msaada mkubwa wanaonipa katika kunijengea utulivu ili niweze kutekeleza majukumu yangu, nawaombea heri na baraka katika maisha yao.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais napenda kutoa mkono wa pole kwa ndugu na jamaa wa marehemu na kwa wale wote waliookolewa au kupoteza mali zao katika ajali ya meli ya MV. Spice Islander iliyotokea tarehe 11/09/2011. Tutaendelea kuzikumbuka roho za ndugu zetu waliotangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahala pema peponi Amin.

Mhe. Spika, vile vile kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais napenda kutoa mkono wa pole kwa familia pamoja na wananchi wa Jimbo la Uzini na Bububu kwa kuwapoteza wawakilishi wao wapendwa, marehemu Mussa Khamis Silima Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Salum Amour Mtondoo Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, tutawakumbuka kwa michango yao mikubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi Amin.

MALENGO MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya mazingira, watu wenye ulemavu, udhibiti wa dawa za kulevya na UKIMWI. Malengo makuu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni:

1. Kuimarisha na kutetea uzingatiaji wa haki za binaadamu na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu katika jamii.
2. Kuongoza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI.

3. Kuimarisha usimamizi wa mazingira na matumizi endelevu ya maliasili.
4. Kuratibu na kudhibiti usafirishaji na biashara haramu ya dawa za kulevya.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA 2011/12 NA MALENGO 2012/13

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejipangia kutekeleza majukumu yake kupitia Idara na Tume zifuatazo.

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Mipango Sera na Utafiti
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
4. Idara ya Mazingira
5. Idara ya Watu Wenye Ulemavu
6. Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya
7. Tume ya UKIMWI
8. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2011/2012
OFISI YA FARAGHA

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ina majukumu ya kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari za Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuimarisha huduma na mazingira mazuri ya utendaji kazi ofisini na nyumbani kwa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, hadi kufikia Aprili 2011/2012 Ofisi ya Faragha imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Spika, katika kuratibu shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais, mambo mbali mbali yametekelezwa yakiwemo; kufanya ziara za kikazi ndani na nje ya nchi na kuandaliwa ripoti ambazo zimewasilishwa Serikalini. Aidha, vikao teule 19 vilivyojadili mada mbalimbali zikiwemo masuala ya kilimo, uvuvi, dawa za kulevya n.k. vimefanyika.

Mhe. Spika, Miongoni mwa ziara za ndani ni pamoja na kutembelea Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Pia ziara za kufanya ukaguzi wa baadhi ya maeneo yaliyoharibiwa kimazingira kama vile, maeneo ya Uwanja wa Amani, njia kuu zinazopita umeme katika eneo la Kwarara, Uwandani, Kiwani, Wingwi n.k.

Aidha Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais amefanya ziara katika Mikoa mitatu ya Tanzania Bara ikiwemo Tabora, Lindi na Dar es Salam ambapo alipata fursa ya kushiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii, kuzindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi mbali mbali ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais alifanya ziara moja ya kikazi nchini India. Katika ziara hiyo, Mhe. Makamu wa Kwanza alipata fursa ya kutembelea majimbo ya Hydrabad, Karnataka (Bangalore) na Kerala. Mhe. Makamu wa Kwanza na ujumbe wake walipata fursa ya kukutana na Viongozi wa Serikali na taasisi mbali mbali pamoja na wawekezaji katika majimbo hayo matatu.

Mhe. Spika, Zanzibar inatarajiwa kufaidika na ziara hii katika Nyanja mbali mbali zikiwemo, teknolojia ya habari na mawasiliano, elimu, kilimo, biashara na uwekezaji. Ufuatiliaji wa mafanikio ya ziara hii kwa pande zote mbili unaendelea vizuri.

Mhe. Spika, zaidi ya wananchi 250 walifika ofisini kwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko yao pamoja na kupatiwa ushauri na maelekezo katika kuyapatia ufumbuzi mambo yanayowakabili. Aidha, mabalozi 12 wanaoziwakilisha nchi zao pamoja na wawakilishi wa mashirika tisa ya kimataifa na ya kikanda walifika kwa Makamu kwa ajili ya kujitambulisha na kuzungumzia mambo mbali mbali ya kimaendeleo pamoja na kuimarisha mashirikiano.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa kitengo cha habari katika Ofisi ya Faragha, kumepelekea kurahisisha upatikanaji wa taarifa na matukio mbalimbali ambayo Makamu wa Kwanza wa Rais anayafanya. Kitengo kimeweza kuanzisha mtandao wake wa kijamii *"weblog"* ambao unaojulikana kwa jina la "Zanzibar ni Njema" yenye anuani http://mkr1znz.wordpress.com. Mtandao huo wa kijamii hurusha hewani habari na taarifa mbali mbali za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, Kitengo cha habari katika Ofisi ya Faragha pia kina mashirikiano na mawasiliano mazuri na vyombo vyengine mbali mbali vikiwemo vile vinavyotumia mtandao ambavyo pia huchapisha habari na matukio ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, Jumla ya vipindi vitano vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia TV na radio za Serikali na zile za binafsi. Zaidi ya makala 15, zimeandikwa na kuchapishwa katika magazeti mbali mbali na mitandao ya kijamii. Mikutano miwili na waandishi wa habari "*Press conference*" imefanyika. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 1).

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi ofisini na upatikanaji wa huduma nyumbani kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, samani na vitendea kazi mbalimbali vimenunuliwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Mei 2012 Ofisi ya Faragha imekwishatumia jumla ya Shilingi 99,100,000 kwa kuendeshea kazi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari za Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi.
4. Kuimarisha huduma za Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia, Ofisi ya Faragha kwa mwaka fedha 2012/2013 inahitaji jumla ya Shilingi 511,324,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo T.Shs. 300,000,000 kwa kuendeshea kazi na T.Shs. 211,324,000 ni kwa ajili ya mishahara.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kukusanya, kutunza takwimu, ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuratibu shughuli za utafiti kwa Idara zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za mipango, sera na utafiti katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

2. Kuweka utaratibu utakaowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndani na nje ya nchi kwa wepesi.
3. Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo.
4. Kutafuta rasilimali ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi zake za kawaida za kuratibu, Idara hii imeandaa mipango ya utekelezaji, bajeti, pamoja na kuiwakilisha Ofisi katika kamati za kitaalamu na vikao mbali mbali ili kuhakikisha masuala yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yanazingatiwa katika mipango yote ya maendeleo.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango imekamilisha uandaaji wa tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa lengo la kutoa taarifa kiurahisi ndani na nje ya nchi, tovuti hii inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha mawasiliano baina ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na wadau wake (www.fvpo.go.tz).

Mhe. Spika, Idara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo ikiwemo mradi wa kuangamiza kunguru weusi, mradi wa usimamizi wa maji machafu Msingini - Kichungwani Pemba pamoja na mradi wa kuimarisha majengo ya viongozi.

Mhe. Spika, Mradi wa Kuangamiza Kunguru Weusi umeanza rasmi mwezi wa Machi 2012. Lengo Kuu la Mradi huu ni kuua kunguru weusi waliopo hapa Zanzibar kwa kutumia mitego na sumu. Aidha lengo la mradi la mwaka 2011/2012 ni kuua kunguru 408,000. Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Fedha za utekelezaji wa mradi huu zinatoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Finland kupitia Jumuiya isiyokuwa ya Kiserikali ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya Tanzania (*Wildlife Conservation Society – WCS*).

Mhe. Spika, kwa upande wa mchango wa Serikali, jumla ya Shillingi 50,000,000 zilipangwa kutumika na hadi kufikia mwezi wa Mei 2012 Shillingi 35,000,000 sawa na asilimia 70 zimetolewa. Mambo yaliyofanyika kwa fedha hizo ni pamoja na kutengeneza mitego 30 na kusambazwa maeneo mbali mbali (tafadhali angalia kiambatanisho nam. 2), kununua sumu ya kuulia kunguru kilo mbili kutoka New Zealand, kununua vifaa mbali mbali vikiwemo mabesini, ndoo, sinia, vijiko, glavu, mapanga na majembe pamoja na kununua chambo cha kutumika kwenye sumu na mitego.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Mei 2012 jumla ya kunguru 11,596 wameshauliwa. Idadi hiyo ni ndogo kwa mujibu wa kiwango cha mwaka kilichowekwa, hii imetokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha na muda mkubwa ulitumika kutengeneza mitego pamoja na kuagizishia sumu kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, mradi wa ujenzi wa mtaro wa maji machafu Msingini na Kichungwani ulizinduliwa rasmi Julai 2009. Mradi unatekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali kupitia Idara ya Mazingira na wananchi wa Shehia za Msingini na Kichungwani zilizopo katika Wilaya ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba kupitia mradi wa *TASAF*. Lengo kuu la mradi huu ni kulinda na kusimamia mazingira ya baharini na ukanda wa pwani wa magharibi ya bahari ya hindi kutokana na shughuli mbali mbali zinazofanywa kutoka nchi kavu ambazo zinasababisha uchafuzi wa mazingira. Jumla ya shilingi 440,000,000 zilitolewa na *UNEP* pamoja na Aqua- 4 All kwa ajili ya vifaa na kazi za mradi huu. Aidha jamii kupitia *TASAF* ilichangia jumla ya shillingi 69,000,000.

Mhe. Spika, Shughuli kubwa za mradi huu ambazo zimefanyika ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa mtaro wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 1,610, ulazaji wa mabomba ya kupitishia maji machafu na ujenzi wa mabwawa matatu ya kukusanyia na kusafishia maji machafu. Kazi kubwa zilizobakia kukamilisha mradi huu ni uwekaji wa kokoto kwenye mabwawa hayo na matengenezo ya mtaro wa zamani wa maji ya mvua. Mkandarasi wa kutoa huduma za usambazaji wa kokoto, mchanga na saruji kwa ajili ya kumalizia kazi hizo ameshapatikana na anatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

Mhe. Spika, mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 31 Machi 2011, lakini kutokana na ucheleweshwaji wa upatikanaji wa fedha kutoka *UNEP*, pamoja na ugumu uliojitokeza wakati wa mvua wa kufikisha vifaa vya kazi katika eneo lililochimbwa mabwawa umesababisha mradi huu kutomalizika kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa mradi wa kuimarisha nyumba za viongozi wa kitaifa, ununuzi wa vifaa na marekebisho ya makaazi mapya ya Makamu wa Kwanza wa Rais yamefanyika.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango iliendelea na juhudi zake za kutafuta rasilimali za kusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuandika pendekezo la mradi wa kujenga uwezo kwa Ofisi na kuiwasilisha *UNDP* hali ambayo imepelekea kufanikiwa kuingizwa katika mradi wa miaka minne wa *UNDAP*. Aidha pendekezo jengine la mradi wa kujenga uwezo limeandikwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango,Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikadiriwa kutumia Shilingi 170,010,000 kati ya hizo Shilingi 15,000,000 kwa kuendeshea kazi na Shilingi 155,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Mei 2012 Idara ilikwisha ingiziwa shilingi 15,000,000 sawa na asilimia100 kwa kazi za kawaida na Shilingi 140,000,000 sawa na asilimia 90 kwa kazi za maendeleo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo**:-**

1. Kusimamia, kuratibu na kuandaa, shughuli zote za mipango, sera, utafiti pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli mtambuka (UKIMWI, dawa za kulevya, jinsia, mazingira, watu wenye ulemavu, utawala bora na idadi ya watu)
3. Kuimarisha mazingira ya kazi na kujenga uwezo wa watendaji

Mhe. Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatarajia kutekeleza miradi mitano (5) kwa kupitia fedha za Serikali na mradi mmoja kwa fedha za wahisani. Miradi yenyewe ni:-

a) Mradi wa kuendeleza elimu ya mazingira
b) Mradi wa majaribio wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi
c) Mradi wa kuangamiza kunguru weusi
d) Mradi wa kuingiza masuala ya watu wenye ulemavu katika mipango ya maendeleo
e) Mradi wa kujenga kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya huko Tunguu (*Construction of Treatment and Rehabilitation Center)*
f) Na mradi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambao utatumia fedha za wahisani.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 176,251,000 kwa kazi za kawaida, ambapo T.Shs. 115,000,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na T.Shs. 61,251,000 kwa ajili ya mishahara. Idara pia inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 255,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali. Aidha Idara inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 705,600,000 kutoka kwa wahisani. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo kuhusu ongezeko la Fedha hizi za Mchango wa Wahisani katika Miradi ya Kimaendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia rasilimali watu pamoja na undeshaji wa kazi za kila siku za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Katika kutekeleza majukumu hayo inasimamia utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi pamoja na sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Pia inasimamia masuala ya nidhamu, uwajibikaji, mafunzo na mafao ya wafanyakazi wanaostaafu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilijipangia malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi.

2. Kukuza uwezo wa wafanyakazi na viongozi na kuwapatia maslahi

3. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.

4. Kuimarisha Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

5. Kuimarisha huduma za usafiri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

6. Kuratibu safari za kikazi nje nandani ya nchi.

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei, 2012 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

Mhe. Spika, Idara imeendelea na jitihada zake katika kuhakikisha kuwepo kwa mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vifaa mbali mbali vikiwemo samani za Ofisi na vitendea kazi. Hatua hiyo imetoa mwelekeo mzuri wa ufanisi hasa katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kuwapatia maposho wafanyakazi wanaostahiki na kufanya malipo ya fedha za likizo kwa wafanyakazi 18 waliokwenda likizo.

Mhe. Spika, Idara imeendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya muda mrefu, watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi wawili wameweza kusaidiwa baadhi ya gharama za mafunzo kama vile usafiri na vifaa vya kuandikia. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 3)

Mhe. Spika, Idara kupitia Kitengo cha Habari na Mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeendelea kushajihisha wananchi na kutoa elimu ya mazingira, dawa za kulevya, UKIMWI na masuala ya watu wenye ulemavu kupitia Televisheni, Radio na Magazeti. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 4)

Mhe. Spika, Idara imefanya matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili liweze kuwa na hadhi inayolingana na Ofisi hii. Miongoni mwa matengenezo hayo ni pamoja na kubadilisha mfumo wa maji machafu na safi, kubadilisha sehemu za mikingo ya vigae vya paa, kupaka rangi na kujenga sehemu ya kupokelea wageni.

Mhe. Spika, Idara imeweza kuhudumia safari sita za nje na kumi na saba za ndani kwa viongozi na watendaji katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, safari hizo zimewawezesha kuhudhuria shughuli mbali mbali za kazi na mikutano ambayo imepelekea kuimarisha utendaji kazi, mahusiano na kubadilishana uzoefu.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 imekadiria kutumia jumla ya shilingi 704,204,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo T.Shs. 388,770,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na T.Shs. 315,434,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei, 2012 ilikwisha kuingiziwa kiasi cha Shilingi 745,545,197 sawa na Asilimia 106. kati ya hizo shilingi 299,725,000 sawa na asilimia 77 kwa ajili ya kuendeshea kazi na shilingi 445,820,197 sawa na asilimia 141 kwa ajili ya mishahara. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa mishahara).

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia majukumu na utendaji wa wafanyakazi.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
4. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari
5. Kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ili iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 616,444,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo T.Shs.254, 749, 00 kwa kuendeshea kazi na Shs. 361,695,000 kwa ajili ya mishahara.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, majukumu makuu ya Idara ya Mazingira kwa mujibu wa Sera ya Mazingira ni kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango na miradi ya kimaendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya kimazingira, kukabiliana na matatizo ya kimazingira, kuhamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira pamoja na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa na malengo yafuatayo:-

1. Kuongeza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.
2. Kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo inazingatia vigezo vya utunzaji wa mazingira.
3. Kudhibiti uingizaji wa bidhaa chakavu zinazoharibu na kuchafua mazingira.
4. Kuendelea kuzuia uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plasitiki.
5. Kuandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera mpya ya Mazingira.
6. Kutekeleza mradi wa kuangamiza kunguru weusi hapa Zanzibar.
7. Kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (*climate change strategy*).
8. Kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2012 Idara ya Mazingira imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe.s Spika**,** Idara imeweza kutoa matangazo juu ya marufuku ya mifuko ya plastiki kwa siku za sikukuu kupitia Redio za *ZBC, Hits FM* na *Zenji FM*, pamoja na Televisheni za *ZBC* na *Zanzibar Cable*. Vipindi 9 vya redio na vipindi 3 vya TV vinavyohusu usimamizi wa mazingira vimerushwa hewani (Tafadhali rejea kiambatanisho Nam. 4). Filamu fundishi (*documentaries*) tatu kuhusu athari za mifuko ya plastiki, uchimbaji holela wa mchanga, na bidhaa chakavu za umeme na elektroniki ziliandaliwa. Semina kumi juu ya athari na udhibiti wa mifuko ya plastiki na uchafuzi wa mazingira zimefanywa skuli zote za msingi za Unguja na Pemba ambazo zina vilabu vya mazingira. Jumla ya skuli 146 (90 Unguja 56 Pemba) na wanafunzi 292 (180 Unguja 112 Pemba) walishiriki semina hizo. Mkakati wa mawasiliano kwa ajili ya elimu ya mazingira umetayarishwa.

Aidha, idara ilifanya mikutano mitano ya jamii huko Pemba katika maeneo ya Uwandani, Kangani na Mwambe na kuwahusisha wanajamii 157 (wanawake 30, wanaume 127). Mikutano hiyo imepelekea kuundwa kwa kamati za jamii za usimamizi wenye uwiano wa ukanda wa pwani (*Integrated Coastal Zone Management Committees – ICZM)*.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira imefanya semina ya siku tatu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wewe mwenyewe Mhe. Spika ulitupa heshima ya kuiongoza semina hiyo. Semina hiyo iliyohusu masuala mbalimbali ya mabadiliko ya tabianchi ilikuwa na lengo la kuwapa uelewa wa mabadiliko ya tabianchi na mwelekeo wa Zanzibar katika kusimamia suala hilo. Sambamba na hayo wafanyakazi 12 waliwezeshwa kufanya ziara ya kimasomo mjini Moshi na Arusha kujifunza na kupata uzoefu juu ya usimamizi wa taka, wafanyakazi hao ni kutoka Idara ya Mazingira, Manispaa, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, Mabaraza ya Miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani, Jumuiya ya Wakulima, Wafanyabiashara na Wenye Viwanda pamoja na jumuiya zisizokuwa za kiserikali ambazo zimewakilishwa na jumuiya ya *CODECOZ*. Aidha, viongozi 10 wa Kamati ya machimbo ya Uwandani walishiriki ziara ya kimasomo Mjini Mombasa nchini Kenya kwa lengo la kujifunza namna bora ya shughuli za uchimbaji na urejeshwaji wa maeneo yaliyochimbwa.

Mhe. Spika, katika kujenga uwezo wa kiutendaji Idara ya Mazingira ili kuweza kutekeleza majukumu ya kutoa elimu ya mazingira na kufanya tathmini ya athari za kimazingira, jumla ya wafanyakazi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu uandishi wa habari na tathmini ya athari za kimazingira. Aidha, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*) na Uandishi wa habari. Wafanyakazi watatu wamelipiwa gharama za masomo kwa ngazi ya cheti katika fani za kilimo, usimamizi wa kumbukumbu na Usimamizi rasilimali watu.

Mhe. Spika, Idara imefanyia mapitio ripoti 12 za Tathmini za Athari za Kimazingira na Kijamii na kutoa vyeti vya mazingira kwa taasisi husika kwa hatua za utekelezaji. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 5)**.** Jumla ya miradi ya hoteli 110 (80 Unguja na 30 Pemba) imefanyiwa ufuatiliaji katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ili kuona namna inavyozingatia masuala ya kimazingira katika uendeshaji wa shughuli zao (Tafadhali angalia kiambatanisho

Nam. 6). Katika ufuatiliaji huo, miradi iliyoonekana na kasoro za kimazingira ilitakiwa kuondoa kasoro hizo ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa kimazingira. (*Environmental Audit*).

Mhe. Spika, miradi ambayo imejenga ndani ya mita 30 kuanzia alama inayofikiwa na maji ya bahari yanapojaa (*high water mark*) imetakiwa kubomoa sehemu ambayo imejengwa ndani ya eneo hilo. Hadi sasa ni mradi mmoja tu wa *Zanzibar Ocean View* ndio umeripoti kutekeleza amri hiyo. Kwa miradi ambayo imekaidi amri hiyo majina ya miradi hiyo yamewasilishwa Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Kanuni ya kudhibiti matumizi ya ardhi kwa ajili ya uekezaji ya mwaka 2006 (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 7). Sambamba na utekelezaji huo, Kanuni ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira (*Environemntal Impact and Social Assessment – EISA Regulations*) imefanyiwa mapitio.

Mhe. Spika, rasimu ya kanuni ya kupiga marufuku uingizwaji wa bidhaa chakavu za umeme na elektroniki (*e-waste*) nchini imeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau husika. Hata hivyo, baada ya kanuni hiyo kupitiwa na Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na wadau wengine imeonekana ipo haja ya kuandaa viwango vya bidhaa zitakazoruhusiwa kuingizwa nchini badala ya kupiga marufuku ya moja kwa moja kuingiza bidhaa hizo. Idara inaendelea kushauriana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kuweka viwango vinavyohitajika vya bidhaa hizo chakavu.

Mhe. Spika, kanuni ya kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki imefanyiwa marekebisho yaliyohitajika. Kufuatia marekebisho hayo, matangazo kwa njia ya gari yametolewa kwa mikoa mitano ya Zanzibar. Aidha, operesheni za kila siku zimefanyika ambazo zinasimamiwa na mkuu wa operesheni wa Jeshi la Polisi Zanzibar. Kwenye operesheni hizo hadi kufikia mwezi wa Mei 2012 jumla ya watu 192 (5 wanawake na 187 wanaume) wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria na kutozwa faini jumla ya shilingi 7, 650,000 (shilingi 6, 350,000.Unguja na 1, 300,000 Pemba). Fedha zote hizo zimeingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali kupitia Mahakama husika. Aidha mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye operesheni hizo ni kupungua kwa kiwango kikubwa cha matumizi ya mifuko ya plastiki pamoja na kupungua kuzagaa kwa mifuko hiyo kwenye maeneo mbali mbali ya Zanzibar.

Mhe. Spika, rasimu ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera mpya ya Mazingira imeandaliwa. Hata hivyo, kukamilika kwa uandaaji wa Mpango Mkakati huo unategemea kukamilika kwa Sera mpya ya Mazingira ambayo itajadiliwa katika kikao cha Makatibu wakuu hivi karibuni. Sera hiyo imechelewa kukamilika kutokana na umuhimu wa kuingiza mambo mengine mapya ya kimazingira yakiwemo ya mabadiliko ya tabianchi ambayo utafiti wake ulikuwa haujakamilika.

Mhe. Spika, katika hatua za kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, utafiti juu ya athari za kiuchumi zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi umefanyika na ripoti yake imewasilishwa serikalini baada ya kujadiliwa na wadau. Kufuatia kupatikana kwa taarifa hizo, tayari hatua za kumpata mshauri mwelekezi wa kuandaa Mkakati huo zimeshaanza. Katika hatua nyengine, maeneo 148 yanayoingia maji ya chumvi Unguja na Pemba yameorodheshwa, kati ya hayo 25 yapo Unguja na 123 yapo Pemba (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 8)**.** Aidha, Kamati za Uongozi na Kitaalamu za kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa Zanzibar zimeanzishwa. Kamati ya Uongozi ina wajumbe 10 ambao ni Makatibu Wakuu na Kamati ya Kitaalamu ina wajumbe 23 katika ngazi ya Wakurugenzi na Viongozi wa taasisi zisizo za kiserikali.

Mhe. Spika, rasimu ya kanuni juu ya uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka imeandaliwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali. Hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kuchapishwa na kuanza utekelezaji. Sambamba na kanuni hiyo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pia inaendelea na taratibu za kuandaa kanuni ya usimamizi wenye uwiano wa ukanda wa pwani (*Integrated Coastal Zone Management {ICZM} Regulations)*.

Mhe. Spika, kutokana na kuwepo athari za mabadiliko ya tabianchi, Idara ya Mazingira ilibahatika kupata fedha za wahisani za kutekeleza mradi wa majaribio wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia mradi huu, Idara ya Mazingira ilipata jumla ya Shilingi 539, 414,800 ili kutekeleza kazi mbalimbali za mradi huo wenye lengo la kufanikisha upatikanaji wa maji yasiyokuwa na chumvi kwa Wananchi wa Shehia ya Nungwi, Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, kazi ambazo kwa sasa zimetekelezwa ni pamoja na kuchimba kisima katika eneo la Shehia Kilimani chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 30,000 kwa saa, kuchimba msingi wa Kilomita 7.5 kutoka eneo la kisima hadi Nungwi, kununua mabomba na kuyalaza katika msingi uliochimbwa, kujenga kibanda cha pampu ya maji, kununua na kufunga pampu ya maji. Aidha, kazi zinazoendelea ni kufunga tangi jipya lililonunuliwa kutoka Uingereza lenye uwezo wa kuhifadhi lita 150,000, kununua na kufunga transfoma pamoja na kuunga umeme kwenye kibanda cha pampu ya maji. Hivi sasa mradi huu uko katika hatua za mwisho za kukamilika.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikadiriwa kutumia Shilingi 239, 158,000 kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Mei 2012 ilikwisha ingiziwa shilingi 261, 426,046 sawa na asilimia 109.3 kati ya hizo shilingi 66, 680,000 sawa na asilimia 66 kwa ajili ya kuendeshea kazi na Shilingi 194, 746,046 sawa na asilimia 144 kwa ajili ya mishahara. Aidha, katika kufanikisha kazi zilizotekelezwa jumla ya shilingi 118, 105,066 zilitumika kutoka mradi wa *MACEMP* na *SMOLE*.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ilipangiwa kukusanya jumla ya shillingi 9, 000,000. Aidha, makusanyo hayo yamegawika katika sehemu mbili ikiwa ni pamoja na ada ya hifadhi ya mazingira ambayo ilipangiwa jumla ya shilingi 4, 000,000 na ada ya ukaguzi wa mazingira yenye jumla ya shilingi 5, 000,000. Kwa mwaka huu, Idara ya Mazingira ilihusika na ukusanyaji wa ada ya hifadhi ya mazingira pekee kwa kuwa ada ya ukaguzi wa mazingira imehamishiwa kamisheni ya Utalii. Ada hii imehamishiwa kwenye taasisi hiyo kwa kuwa ilihusika na fomu za maombi ya leseni za biashara za utalii ambazo hupitia kwenye taasisi mbali mbali kuridhia utoaji wa leseni hizo. Kwenye kifungu cha ada ya hifadhi ya mazingira hadi kufikia mwezi wa Mei 2012, Idara ya Mazingira imeweza kukusanya Shilingi 5, 978,000 sawa na asilimia 149 ya kifungu hicho.

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kudhibiti uchafuzi wa mazingira.
2. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo.
3. Kuongeza uwezo na kuimarisha muundo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.
4. Kuimarisha usimamizi endelevu wa maliasili.
5. Kuongeza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.
6. Kuimarisha utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za mazingira.
7. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shillingi 369,369,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 112,373,000 ni kwaajili ya kuendeshea kazi na shilingi 257,296,000 ni kwaajili ya mishahara.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2012/2013, imepangiwa kukusanya jumla ya shillingi 10, 800,000.00 ambazo zitatokana na ada ya hifadhi ya mazingira ikwa ni pamoja na vyeti vya Mazingira.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenye Ulemavu ina majukumu ya kuratibu masuala mbali mbali ya watu wenye ulemavu, pia inafanya kazi na Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu ambalo linaishauri serikali kuhusu maendeleo ya watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2006.

Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kuendeleza usajili wa Watu wenye Ulemavu kwa kupata taarifa zinazohitajika juu ya watu wenye ulemavu.
2. Kuongeza uelewa wa jamii juu ya Sera, Sheria na Mikataba ya Kimataifa ya haki za watu wenye ulemavu.
3. Kujenga uwezo wa Idara, Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Zanzibar na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu.
4. Kuratibu Shughuli za Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Zanzibar.

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2012 Idara ya Watu Wenye Ulemavu imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Katika kuendeleza usajili wa Watu Wenye Ulemavu, Idara imeweza kusajili watu wenye ulemavu katika mikoa yote miwili ya Pemba. Jumla ya watu 6,445 wenye ulemavu tofauti wamesajiliwa. Kati ya hao wanaume 3,556 na wanawake 2,878. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 9). Kabla ya kufanya usajili, mafunzo yalitolewa kwa masheha 121, wakusanyaji taarifa 25 na wasimamizi wa usajili 4 kwa ajili ya kushajihisha na kuwafichuwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, katika kuongeza uelewa wa jamii juu ya Sera, Sheria na Mikataba ya Kimatafa ya Haki za Watu wenye Ulemavu, Idara inaendelea kuifanyia mapitio Sheria ya Watu wenye Ulemavu. Vikao vitano vya awali vimefanyika vya kupitia Sheria Nam. 9 ya mwaka 2006 ya watu wenye ulemavu ambavyo viliwashirikisha wadau mbali mbali wa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kuhamasisha mambo mbali mbali ya Watu wenye Ulemavu na kwenda sambamba na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu, Idara imefanikiwa kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu, tarehe 3/12/2011 katika kiwanja cha Mahonda Wilaya ya Kaskazini "B", Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, idara imefanikiwa kushawishi uanzishwaji wa maafisa waratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu ili kusaidia taasisi husika kuingiza masuala ya Watu wenye Ulemavu katika mipango ya taasisi za serikali. Jumla ya maafisa waratibu 16 tayari wapo katika wizara zetu. Vile vile idara ilitoa mafunzo juu ya uingizwaji wa masuala ya watu wenye ulemavu kwa maafisa hao. Aidha, idara kwa kushirikiana na *"Save the Children"* imetoa mafunzo juu ya haki na uhifadhi wa mtoto kwa watu 80 wakiwemo wazazi, walezi na watoto wenye ulemavu katika mikoa miwili ya Pemba. Idara imeweza kuandaa vipindi 15 vya Radio na viwili vya TV kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*), Zenji FM na Radio Istiqama Pemba. (Tafadhali rejea kiambatanisho Nam. 4)

Mhe. Spika, katika kujenga uwezo wa Idara na Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, idara imeweza kununua vifaa vya ofisini kama vile samani za Ofisi na vifaa vya utendaji kwa wafanyakazi wake. Aidha, idara imemlipia mafunzo mfanyakazi mmoja katika ngazi ya Diploma ya kompyuta.

Mhe. Spika, kwa kutambua mchango wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika suala zima la kutetea haki na kuhakikisha Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zinakuwa na nguvu kiutendaji na kiuwezo, Idara imeweza kutoa ruzuku kwa Jumuiya tisa (9) za Watu wenye Ulemavu pamoja na kuwapatia visaidizi (viti vyenye magurudumu mawili) watu 31 Unguja na Pemba. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam.10a na b)

Mhe. Spika, katika kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, idara imefanya vikao vinne vya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya Watu wenye Ulemavu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikadiriwa kutumia Shilingi 177,995,000 kwa kazi za kawaida hadi kufikia Mei 2012 ilikwisha ingiziwa shilingi 139,424,888 sawa na asilimia 78.3 kati ya hizo shilingi 85,258,000 sawa na asilimia 62 kwa ajili ya kuendeshea kazi Shilingi 54,166,888 sawa na asilimia 127 kwa ajili ya mishahara.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu.
2. Kuwapatia visaidizi na kuimarisha juhudi za taasisi zinazoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu.
3. Kuanzisha mfumo wa taarifa za Watu wenye Ulemavu.
4. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za Watu wenye Ulemavu.
5. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 532,562,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo shilingi 96,992,000 ni mishahara na 435,570,000 ni matumizi ya kuendeshea kazi.

TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina jukumu la kuratibu mapambano dhidi ya matumizi, biashara na usafirishaji wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari ya dawa za kulevya na kutoa huduma za tiba na ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kuwasilisha Mswaada wa Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar katika ngazi zinazo husika.
2. Kuwajengea uwezo watendaji wa Sekta ya Dawa za Kulevya.
3. Kuendeleza upigaji vita dawa za kulevya.
4. Kuandaa Sera ya Dawa za Kulevya.
5. Kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya.
6. Kuziendeleza juhudi za Taasisi zisizo za kiserikali (*NGOs*) zinazotoa huduma za makaazi na marekebisho kwa vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya (*Sober Houses*).

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2012 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Spika, tume imeweza kufanya mapitio ya Sheria Nam.9 ya mwaka 2009 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar. Rasimu ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo ilipitiwa na wadau wa ngazi mbalimbali kabla ya kupitishwa na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, ili kufanikisha shughuli za uhamasishaji na ufuatiliaji wa mambo mbalimbali ya kikazi, jumla ya vespa nne (4) zimenunuliwa. Na kwa upande wa kujenga uwezo wa watendaji, wafanyakazi watatu wameweza kupata mafunzo ya muda mrefu juu ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa taasisi ya *"Center for Disease Control"* ya Marekani, Serikali ya Australia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, tume iliweza kuandaa programu na ziara za uhamasishaji upigaji vita dawa za kuleva kupitia vyombo vya habari na kuzitembelea shehia mbalimbali za Unguja na Pemba. Jumla ya vipindi 41 vilirushwa hewani, vipindi 24 katika radio na 17 katika televisheni. Jumla ya shehia 17 zilifanyiwa ziara za uhamasishaji na taaluma juu ya athari ya dawa za kulevya, kati ya hizo tisa Unguja na nane Pemba zenye wastani wa watu 783. Aidha, wanafunzi 5,422 katika Skuli 28 walipatiwa taaluma hiyo. Kati yao wasichana ni 2,991 na wavulana 2,431; wengi wao ni wenye umri kati ya miaka 12 hadi 18. Pia walimu 97 walifaidika na taaluma hiyo.

Mhe. Spika, Tume kwa kushirikiana na taasisi ya Umoja wa Mataifa ya Dawa za Kulevya na Uhalifu kanda ya Afrika Mashariki (*United Nations Office on Drugs and Crime Regional Office for Eastern Africa- UNODC-ROEA)* ilifanya semina maalum ya siku moja ya uhamasishaji upigaji vita biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu**.** Pia kwa kutambua umuhimu wa taasisi za kidini katika jamii, Tume kwa kushirikiana na taasisi ya *"American International Health Alliance" (AIHA)* iliandaa semina juu ya dawa za kulevya kwa mtandao wa taasisi za dini mbali mbali unaoratibiwa na Ofisi ya Mufti Unguja na Pemba. Jumla ya washiriki 84 walinufaika na mafunzo hayo. Lengo hasa ni kuwapa mwamko zaidi na kusaidia kuendelea na juhudi zao za kila siku za kuwaasa vijana, waumini na jamii kwa jumla juu ya athari ya dawa za kulevya.

Mhe. Spika, Uandaaji wa Sera ya Dawa za Kulevya haukuweza kukamilika kama ilivyotarajiwa kutokana na kuchelewa kupata fedha zilizoahidiwa na wafadhili. Hata hivyo, shughuli hiyo imeshaanza na imo katika hatua za awali za ukusanyaji wa maoni ya wadau.

Mhe. Spika, Tume kupitia kituo chake cha ushauri nasaha kilichopo mtaa wa Sogea kiliweza kutoa huduma kwa jamii na watumiaji wa dawa za kulevya wapatao 984 wakiwemo wanawake 510, na wanaume 474. Kati ya hao 97

walikuwa ni watumiaji wa dawa za kulevya (wanaume 82 na wanawake 15). Aidha, watu tisa (9) kati yao waligundulika na virusi vya UKIMWI, (w/ke 4, w/me 5). Kupitia huduma za kuwafikia wateja (*outreach programme*) katika maeneo yao (maskani), jumla ya wateja 125 (wanawake 20, wanaume 105) waliweza kufikiwa katika maeneo mbali mbali (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 11).

Mhe. Spika, kwa kutambua mchango wa taasisi zisizo za kiserikali katika suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilizipatia jumla ya shillingi 9,900,000 nyumba tisa (9) za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya (*Sober Houses*) pamoja na seti ya Televisheni na Radio Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 501 walipata huduma katika makaazi hayo. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam.12a, b na c)

Mhe. Spika**,** Tume kwa kushirikiana na taasisi ya AIHA iliweza kutoa mafunzo ya uongozi na uwekaji wa kumbukumbu za kifedha kwa taasisi zinazotoa huduma za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya (*Sober Houses*) Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 45 (wanawake 6, wanaume 39) walifaidika na mafunzo hayo. Aidha mafunzo ya programu ya upataji nafuu (Recovery Oriented System of Care –ROSC) yalitolewa kwa wadau mbali mbali, wakiwemo watendaji wa Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Chuo cha Mafunzo, jumla ya washiriki 75 kutoka Unguja na Pemba walifaidika na mafunzo hayo.

Mhe. Spika**,** Tume imekamilisha rasimu ya muongozo wa nyumba za marekebisho za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, Tume iliweza kuandaa mkutano wa mapitio ya Katiba ya Jumuia ya vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya (Drug Free Zanzibar*)* na kusimamia uchaguzi wa taasisi hiyo. Tume kupitia programu yake ya *Family Therapy* imekuwa ikikutana na wazee, familia na jamaa ili kubadilishana mawazo, kuwapa ushauri na kuzungumzia mafanikio na changamoto mbali mbali. Mikutano minne na wanafamilia iliyokuwa na wastani wa watu wapatao 3,022 ilifanyika.

Mhe. Spika**,** Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikadiriwa kutumia shilingi 142,527,000 kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Mei 2012 ilikwisha ingiziwa shilingi 138,965,297 sawa na asilimia 97.5 kati ya hizo shilingi 62,200,000 sawa na asilimia 73 kwa ajili ya kuendeshea kazi Shilingi 76,765,297 sawa na asilimia 134 kwa ajili ya mishahara.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo;

1. Kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.
2. Kuongeza mwamko wa jamii juu ya athari na udhibiti wa dawa za kulevya.
3. Kuimarisha utoaji wa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya.
4. Kuanzisha mfumo wa taarifa za dawa za kulevya.
5. Kuratibu na kuimarisha juhudi za taasisi katika kushughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya.
6. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 247,091,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Shilingi 146,607,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea kazi na Shilingi 100,684,000 ni kwa ajili ya mishahara.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Pemba.
2. Kuimarisha mazingira ya Utendaji kazi.
3. Kujenga uwezo wa wafanyakazi.

Mhe. Spika**,** hadi kufikia Mei 2012 Ofisi Kuu Pemba imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba imeweza kuratibu ziara mbali mbali za Viongozi zikiwemo ziara za Makamo wa Kwanza wa Rais, ziara za Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ziara za Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Pia Ofisi Kuu Pemba iliratibu ziara ya Mwakilishi wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (UK-Department for International Development -DFID) katika maeneo yanayoendeleza juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Ofisi ilisimamia utekelezaji wa msaada uliotolewa kwa ajili ya kuendeleza huduma kwa vijana wanaoendelea kupata nafuu ya kujikinga na matumizi ya dawa za kulevya katika nyumba za kurekebisha tabia (Sober Houses). Mikutano ya operesheni 'Mifuko ya Plastiki' kwa Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba nayo pia iliratibiwa.

Mhe. Spika**,** katika jitihada za kuimarisha mazingira ya utendaji kazi, Ofisi Kuu Pemba iliweza kununua vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi vikiwemo kompyuta na samani, pamoja na kuunganisha mitandao ya mawasilisano. Pia Ofisi Kuu Pemba imeweza kuimarisha Ofisi ya Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa kuwapatia Ofisi yenye mazingira rafiki wanayoweza kuitumia bila usumbufu.

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 214,115,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Shilingi 135,875,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na Shilingi 78,240,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei, 2012 ilikwisha kuingiziwa kiasi cha Shilingi 218,472,625 sawa na asilimia 102 kati ya hizo shilingi 95,242,000 sawa na asilimia 70 kwa ajili ya kuendeshea kazi na Shilingi 123,230,625 sawa na asilimia 158 kwa ajili ya mishahara.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo**:-**

1. Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Pemba.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.
3. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.
4. Kusimamia na kuratibu udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 316,659,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Shilingi 157,774,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na shilingi 158,596,000 kwa ajili ya mishahara.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika**,** majukumu makuu ya Tume ya UKIMWI ni kuhakikisha kwamba sera na mikakati ya taifa ya kupiga vita UKIMWI zinaundwa na kutekelezwa, kutafuta rasilimali zitakazotumika katika utekelezaji wa muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI, kuimarisha uwezo wa wadau katika kufanyia kazi programu za UKIMWI na kuratibu shughuli zao, kushajihisha utoaji wa huduma za tiba na matunzo kwa watu walioathirika na kuathiriwa, kufuatilia na kutathmini umakini na ufanisi wa utekelezaji wa mikakati, sera na muitiko wa kitaifa na kutoa taarifa zote zinazohusiana na UKIMWI.

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kutekeleza Mkakati wa Pili wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI, kwa kuzishirikisha sekta za serikali, sekta binafsi na Asasi za kiraia katika ngazi zote.
2. Kuimarisha utekelezaji wa programu za habari, utetezi na mawasiliano kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya tabia kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa na jamii kwa ujumla.
3. Kuimarisha mipango ya ufuatiliaji, tathmini na utafiti inayohusiana na shughuli za UKIMWI na maeneo yanayohusiana nayo.
4. Kuongeza uwezo wa Tume na wadau katika kuratibu na kutekeleza shughuli za UKIMWI.

Mhe. Spika**,** hadi kufikia Mei 2012 Tume ya UKIMWI imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-
Mhe. Spika**,** Tume imeweza kuzindua Mkakati wa Pili wa kitaifa wa UKIMWI Siku ya UKIMWI Duniani tarehe 1 Disemba 2011, baada ya uzinduzi, Mkakati huo ulisambazwa kwa wadau mbali mbali kwa kuanza kuufanyia kazi.

Aidha Tume imetayarisha Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa kitaifa wa UKIMWI wa mwaka 2012/13 hadi 2013/14. Pamoja na uzinduzi wa mkakati, Tume imezindua Tovuti yake www.zac.or.tz

Mhe. Spika**,** Tume imeweza kuzisaidia Shehia 71 katika kuandaa mipango ya Shehia dhidi ya udhalilishaji wa jinsia na UKIMWI (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 13). Pia Tume imewapatia mafunzo juu ya usimamizi wa masuala ya UKIMWI Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kuwawezesha kuongeza usimamizi wa uwajibikaji wa sekta za Serikali kwenye masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI imeweza kuimarisha utekelezaji wa programu za habari, utetezi na mawasiliano kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya tabia nchi kwa makundi maalum na jamii kwa ujumla kwa kuufanyia mapitio Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano na Utetezi ambao unaendana na Mkakati wa Pili wa kitaifa wa UKIMWI. Mkakati huo kwa sasa uko tayari kusambazwa kwa wadau kwa matumizi .

Mhe. Spika, ili mapambano ya UKIMWI yaimarike, ushiriki na ushirikishwaji wa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ni jambo la lazima. Kwa kulitambua hilo, mkutano wa kitaifa uliowashirikisha viongozi katika ngazi za maamuzi kutoka sekta mbalimbali ulifanyika. Mkutano huo ulilenga kuhamasisha umuhimu wa kuwashirikisha Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI katika mipango mbalimbali ya maendeleo. Jumla ya washiriki 55 (wanaume 35, wanawake 20) walihudhuria wakiwemo Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Aidha jumla ya shilingi milioni 15 walipatiwa ZAPHA+ kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao mbali mbali zinazolenga utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa UKIMWI. Ni matumaini ya Tume kwamba jitihada zao zitasaidia kupunguza unyanyapaa wa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na hatimae maambukizi ya VVU.

Mhe. Spika**,** Taasisi za Kidini zina mchango mkubwa katika kupiga vita suala la UKIMWI. Semina mbili za mafunzo ya viongozi wa dini zimefanyika Unguja na Pemba. Jumla ya viongozi 58 (wanaume 34, wanawake 24) wamefikiwa. Aidha, kupitia Mtandao wa Taasisi za Dini katika Mapambano dhidi ya UKIMWI, miongozo mbali mbali ya UKIMWI imechapishwa. Nakala 350 za miongozo ya afya ya uzazi na jinsia zimetolewa kwa waumini wa Kiislamu na Kikristo.

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI pia imeweza kuandaa mikutano ya utetezi wa makundi maalum pamoja na watu wenye ulemavu Unguja na Pemba, kwa kuhamasisha taasisi mbalimbali kuzingatia mahitaji ya makundi hayo katika programu mbalimbali za UKIMWI na afya kwa ujumla.

Mhe. Spika**,** Tume imeendelea kuchapisha jarida la Jihadhari. Hadi kufikia Januari, toleo nambari 15 limetoka kwa kuchapishwa nakala 5,000 ambazo zimesambazwa sehemu mbalimbali. Aidha, vipeperushi 3,000 kwa ajili ya makundi maalum vimetayarishwa na kuchapishwa.

Mhe. Spika**,** katika kukabiliana na tatizo la UKIMWI Tume ya UKIMWI imeweza kuyafikia makundi maalum (wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wanawake wanaojiuza na watu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano), kwa kuwapatia huduma mbalimbali za kujikinga na UKIMWI. Makundi haya yameweza kufikiwa kwa kuwatumia waelimishaji rika ambao wanafanya kazi katika maeneo ambayo makundi haya yanapatikana zaidi. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 14)**.**

Mhe. Spika**,** katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini, Tume ya UKIMWI imeweza kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa program za UKIMWI. Jumla ya vikundi 24 vyenye miradi 36 ya kujiongezea mapato vilifuatiliwa. Vile vile Tume iliweza kuandaa Ripoti ya mwaka ya ufuatiliaji na Tathmini kwa shughuli za UKIMWI na ripoti ya mkutano mkuu maalum wa Umoja wa Mataifa ”United Nation General Assembly Special Session” (UNGASS). Vile vile, Tume imeweza kukusanya, kuwasilisha, kuchambua na kuhakiki taarifa za fomu zinazotumiwa na wadau mbali mbali katika kukusanya taarifa za utekelezaji wa shughuli za UKIMWI (ZHAPMoS).

Mhe. Spika**,** katika kuongeza uwezo wa wadau, Tume ya UKIMWI imeweza kutoa mafunzo kwa asasi za kiraia na wadau wengine. Jumla ya asasi 55 zilipatiwa mafunzo ya uongozi, utetezi, ushawishi, ubia, utatuzi wa migogoro na uandishi wa Ripoti. Washiriki 15 (wanaune 9, wanawake 6) kutoka ZANGOC walipatiwa mafunzo ya jinsia na UKIMWI, waandishi wa habari na wasanii 25 (wanaume 15, wanawake 10) walipatiwa mafunzo juu ya ubunifu wa kazi za mawasiliano na waelimishaji rika 40 (wanaume 22, wanawake18) kutoka katika makundi maalum walipatiwa

mafunzo ya namna ya kuyafikia makundi maalum. Aidha Tume imeandaa warsha ya kuwahamasisha Waheshimiwa Wawakilishi na makatibu wa kamati juu ya muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI ili kuongeza uelewa wao.

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI imeimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanya ukarabati wa jengo lake na kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika kutimiza majukumu yake. Katika kipindi cha mwaka wa 2011/12, jumla ya wafanyakazi 3 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 6 wamepata mafunzo ya muda mfupi. (Tafadhali rejea kiambatanisho Nam. 3)

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikadiriwa kutumia Shilingi 472,000,000 kwa kazi za kawaida hadi kufikia Mei 2012 ilikwisha ingiziwa shilingi 439,648,862 sawa na asilimia 93**.** Aidha Tume iliidhinishiwa Shilingi. 90,000,000 kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia Mei 2012, ilikwisha ingiziwa Shilingi 90,000,000 sawa na asilimia 100. Kwa upande wa fedha za wahisani walitarajiwa kuchangia Shilingi 1,300,000,000 na hadi kufikia Mei 2012, wamechangia Shilingi 705,550,000 sawa na asilimia 54.3.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika**,** Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2012/13 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa Sera, Sheria na Mkakati wa Pili wa kitaifa wa UKIMWI.
2. Kuongeza uwezo wa programu za habari, utetezi na mawasiliano ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum.
3. Kuongeza utumiaji wa taarifa zinazotokana na ufuatiliaji, tathmini na utafiti katika programu za UKIMWI.
4. Kuimarisha mazingira ya kazi ili kuleta ufanisi.
5. Kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha .

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo iliyojipangia Tume ya UKIMWI kwa mwaka fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 739,000,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo shilingi 500,838,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi, na shilingi 238,162,000 kwa ajili ya mishahara. Aidha inatarajia kutumia Shilingi 50,000,000 kwa kazi za maendeleo kutoka serikalini na shilingi 893,760,000 kutoka kwa wahisani.

SHUKURANI

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliofanikisha ukamilishaji wa kazi hii. Pia napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa uongozi wako makini wa kuliongoza Baraza hili tukufu katika awamu hii ya saba, pamoja na Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza. Aidha, bila ya kuwasahau naomba niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwa wasikivu na wastahamilivu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana katika kutoa michango mbali mbali ambayo itasaidia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kutatua matatizo yanayoathiri jamii. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inaahidi kuichukua michango yote itakayotolewa na Wajumbe wa Baraza hili na kuifanyia kazi kwa maslahi ya Jamii na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi rafiki, mashirika ya Kimataifa na watu binafsi kwa kuendelea kutusaidia kuendeleza shughuli za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Nchi hizo ni pamoja na Marekani, Finland, Norway, Uingereza, Uholanzi, Australia, China, Brazil, India na Falme za nchi za Kiarabu na Oman. Pia mashirika ya kimataifa yakiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UNEP, UNODC, UNFCCC, WHO, World Bank, AIHA, CDC, ICAP, Save the Children na nchi na mashirika mengine ambayo sikuyataja, lakini kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo. Juhudi na michango yao tunaithamini sana.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako tena natoa shukrani zangu kwa viongozi wakuu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kutetea haki na fursa za watu wenye ulemavu. Taasisi hizi zinatoa mchango mkubwa na mashirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, mashirikiano yao yanasaidia kuleta

ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu. Nawaomba waendelee kutupa mashirikiano hayo kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kufikia lengo kuu la kukuza uchumi na kupambana na umasikini.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inatoa shukurani za dhati kwa vyombo vya habari vyote ambavyo tumekuwa tukishirikana navyo kuielemisha jamii juu ya athari za uharibivu wa mazingira, matumizi ya dawa za kulevya, namna ya kujikinga na VVU na umuhimu wa kuwahudumia watu wenye ulemavu. Ni matumaini yetu kuwa tutaendeleza mashirikiano haya kwa faida ya jamii yetu yote.

Mhe. Spika**,** shukurani za pekee ziwaendee wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mwisho napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu.

HITIMISHO

Mhe. Spika**,** kwa heshima nachukua nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na hatimae kuidhinisha matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ya jumla ya shilingi bilioni mbili milioni mia saba na sabini (T.Shs. 2,770,000,000) kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni moja milioni mia tano kumi na tano (T.Shs. 1,515,000,000) kwa ajili kuendeshea kazi na shilingi bilioni moja milioni mia mbili hamsini na tano (TShs.1, 255,000,000) kwa ajili ya mishahara. Aidha tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi milioni mia mbili hamsini na tano (T.Shs. 255,000,000) kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na shilingi milioni mia saba na tano na laki sita **(**T.Shs 705,600,000) fedha za wahisani (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 15 a na b).

Mhe. Spika, aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishie Tume ya UKIMWI matumizi ya jumla ya shilingi milioni mia saba thelathini na tisa (T.Shs. 739,000,000) kwa kazi za kawaida, ambapo shilingi milioni mia tano laki nane thalathini na nane elfu (T.Shs. 500,838,000) kwa ajili ya kuendeshea kazi, na shilingi milioni mia mbili thalathini na nane laki moja sitini na mbili elfu (TShs.238, 162,000) kwa ajili ya mishahara. Aidha tunaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi milioni hamsini (T.Shs. 50,000,000) kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali, na shilingi milioni mia nane tisini na tatu lakisaba sitini elfu (T.Shs 893,760,000) mchango wa wahisani (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 15 c na d).

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Mhe.Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kukutana tena jioni ya leo katika Baraza letu tukufu, ili kujadili masuala muhimu kwa ajili ya mustakabali mzima wa maendeleo ya watu wetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, vile vile ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi wa Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao ya dhati wanayotupa katika utendaji wa kazi zetu za kamati. Vile vile ninapenda kuishukuru Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kuwasilisha mbele ya kamati yetu na Baraza lako tukufu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/13, ili yapate baraka za Wajumbe wako na baadae yapitishwe kwa maslahi ya wananchi na serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, lakini pia sitosahau kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu. Naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5. Mhe. Mohamed Haji Khalid	-	Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohamed Ali	-	Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9. Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa kwa niaba ya kamati yetu naomba uniruhusu niwasilishe maoni ya kamati yetu juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais mwaka wa fedha wa 2012/13.

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Spika, tunaipongeza idara hii kwa kuandaa na kutekeleza ziara za kikazi nchi za nje, ikiwemo ziara ya India katika Majimbo ya *Andhra Pradesh, Karnataka na Kerela*, ambapo tunaelezwa kuwa kupitia ziara hizo tunategemea kupata mafanikio katika nyanja mbali mbali, zikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Elimu, Kilimo, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, kumekuwa na kawaida kwa viongozi wetu wa Kitaifa na hata mawaziri kufanya ziara za kikazi nje ya nchi na kupewa ahadi mbali mbali kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar, lakini ahadi hizo zinaishia kwenye vitabu na makabati. Hivyo, tunaiomba sana Serikali kupitia taasisi zake mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuzifuatilia ahadi hizo ili ziweze kufanyiwa kazi na kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile tunaipongeza Idara hii kwa kufungua *BLOG* iitwayo "*weblog*" inayojulikana kwa anuani ambayo Mheshimiwa Waziri amekwishaianisha katika Hotuba yake, *(http;//mkrlznz.wordpress.com).*
Tunawaomba wananchi wautembelee mtandao huo ili kujua mambo mengi yanayohusu utendaji wa shughuli zinazotekelezwa na viongozi wetu.

Mhe. Spika, kamati yetu inaiuliza serikali vipi kuhusu usafiri na wahudumu akiwemo mpishi kwa ajili ya huduma za Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais huko Pemba. Kamati inalikumbushia hili kwa sababu inafahamu kuwa suala hili lipo kwa muda sasa na linahitaji kupatiwa ufumbuzi.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, tunaipongeza Idara hii kwa kuweza kufungua tovuti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ijulikanayo kwa jina la 'www.fvpo.go.tz''. Tunawaomba pia wananchi kutembelea tovuti hii ili kujionea mambo yanayofanywa na Ofisi hii. Pia tunaipongeza Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa jitihada inazozichukua katika suala la kuwatokomeza kunguru weusi ambao nao wamekuwa ni chanzo cha uharibifu wa mazingira katika nchi yetu. Tunaiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuendelea na jitihada za kuwatokomeza ndege hawa ili kuondokana na changamoto zao.

Mhe. Spika, pia tunapongeza jitihada zinazochukuliwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba, kwa kushirikiana na Baraza la Mji la Chake Chake, kwa kusaidia ujenzi wa mtaro kupitia Idara ya mazingira, ambao kwa muda mrefu umekuwa ni kero kwa wananchi wetu. Ukweli mradi huu umesaidia sana kuunganisha mabomba ya maji machafu ambayo yalikuwa ni kero kwa wananchi. Tunawaomba wananchi wanaoutumia mtaro huu wachukue jitihada za kusafisha mazingira yao na kuutunza mtaro huo, ili kuondosha tatizo la kujaa taka ambazo zinazuia mtiririko wa maji machafu kutoka mitaani kuelekea baharini.

Mhe. Spika, suala hili lisipochukuliwa hatua linaweza kusababisha kutokezea maradhi ya mripuko yatakayowaathiri wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Kwa upande mwengine Kamati inalikumbusha Baraza la Mji Chake Chake kutekeleza jukumu la kuusafisha mtaro huu kwa kuupitia kila baada ya muda kwa lengo la kuhakikisha kuwa

mtaro huu uliojengwa kwa fedha nyingi za wavuja jasho wa nchi za Washirika wa Maendeleo unakuwa katika hali ya usafi wakati wote.

Mhe. Spika, tunalisema hili kwa sababu imekuwa kawaida kwa mtaro huu kutosafishwa mpaka Wajumbe wako wa Kamati wayatembelee maeneo hayo na kuanza kupiga kelele kuhusu usafi wa mtaro.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Spika, tunapongeza jitihada zinazochukuliwa na Idara hii katika kutekeleza majukumu yake vizuri likiwemo suala la kulitengeneza Jengo la Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ili liendane na hadhi inayolingana na Ofisi hiyo. Hata hivyo, tumebaini mapungufu katika Hotuba ya Waziri kutoelezea malengo ya Idara hii na nyenginezo katika suala la ajira, yaani Idara hazijaainisha nafasi za ajira katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, wakati kamati yetu inaelewa fika kuwa kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi, katika baadhi ya Idara na Vitengo vya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mfano mzuri kwa upande wa Pemba hakuna mpishi kwa ajili ya kumhudumia Makamo wa Kwanza wa Rais.

Aidha, katika Idara ya Watu wenye Ulemavu, tuliwahi kuelezwa kuwa idadi ya wafanyakazi iliongezwa kutoka mfanyanyakazi mmoja (1) hadi wawili (2) ambao kiuhalisia hawatoshi hata kidogo. Sasa tunamuuliza Mheshimiwa Waziri Je! Wafanyakazi alionao katika Idara na vitengo vyake wanatosheleza katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais?

Mhe. Spika, mbali na mapungufu hayo, hotuba pia imeshindwa kuainisha changamoto inazoikabili Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais. Kamati inataka kuelewa kama Ofisi hii inazo gari za kumhudumia Makamo wa kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba na Dar es salaam. Vipi kuhusu suala la Makaazi kwa Mheshimiwa huyu anapokwenda Pemba na Dar es salaam anafikia nyumba za serikali au anakodiwa?

Mhe. Spika, tunauliza swali hili ili kutaka kufahamu ikiwa viongozi wetu wa kitaifa wanapokwenda Dar es salaam na Pemba wanafikia nyumba za kukodi au nyumba ambazo hazimilikiwi na serikali, basi ni vyema serikali ikaandaa mkakati wa kuwajengea nyumba Viongozi wetu hawa akiwemo Makamo wa Kwanza wa Rais na kuondokana na utaratibu wa kukodi nyumba ambao una gharama zake.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Idara hii lakini bado kuna mapungufu mengi ya kisheria ambayo yanaikosesha Idara hii mapato makubwa yanayohitajika kwa maendeleo ya nchi yetu. Aidha, Idara hii inashindwa kuchukua hatua za kisheria za kumuadhibu yule anayeharibu mazingira iwe kwa makusudi au bahati mbaya. Idara hii inaishia kutoa *Stop Order* na haina nguvu za kisheria zaidi ya hapo. Hivyo, tunaiagiza Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuyawasilisha kwa haraka hapa Barazani marekabisho ya sheria ya mazingira ili kuipa nguvu Idara kuwachukulia hatua zaidi za kisheria wale wote wanaokiuka sheria hiyo.

Aidha, tunaiagiza Ofisi ya Makamo wa Kwanza kupitia Idara ya Mazingira kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Idara ya Ardhi ili kuhakikisha kuwa Sheria zao zinafanya kazi ipasavyo kwa lengo la kwenda sambamba na utunzaji wa mazingira. Mhe. Spika, tunaliainisha hili kwa sababu ardhi na mazingira ni watoto pacha na mmoja akienda kinyume na mwenziwe basi hali huwa ndivyo sivyo.

Mhe. Spika, serikali inakosa mapato mengi kupitia kodi ya mazingira, lakini inatumia pesa nyingi katika kuyahifadhi mazingira yaliyoharibiwa na ushahidi unaonekana katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ambapo kumetengwa pesa nyingi kwa ajili ya kuhifadhi mazingira hayo. Kamati yangu bado inaisisitiza serikali kupitia idara hii kuhakikisha kuwa hairuhusu utekelezaji wa mradi wowote kabla ya kufanyiwa tathmini ya mazingira na kupewa kibali na Idara hii. Pia tunaiagiza serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo inaongoza kwa kuharibu mazingira kwa kuchimba mashimo makubwa wakati wa ujenzi wa Barabara, kuitekeleza sheria ya mazingira ya kuilipa Idara ya Mazingira asilimia 10 (10%) ya kufidia uharibifu huo.

Mhe. Spika, pia kamati yangu tulipokuwa kwenye ziara za kamati iliishauri Shirika la Bandari kuwasaidia wananchi wanaoingiliwa na maji ya Bahari kwenye mashamba yao ya mpunga kutokana na mashimo makubwa

yaliyoachwa na Kampuni ya *Cogefer* wakati wa ujenzi wa Gati ya Mkoani huko Pemba, kwa hiyo suala hili lifuatiliwe kwa kusaidiana na Halmashauri ya wilaya ya Mkoani.

Mhe. Spika, kamati yangu haikuridhika na ujenzi uliofanywa na muwekezaji ajulikanae kwa jina la Palumbo aliyejenga hoteli huko Uroa. Muwekezaji huyu amechimba fukwe kwa kutumia Kijiko na kujenga kwenye fukwe hiyo kwa kuingia mita 20 ndani ya bahari, wakati sheria za ujenzi zinaruhusu ujenzi mita 30 kutoka kwenye fukwe. Kwa kweli hii ni aibu kubwa kwa serikali yetu, kwani kunaonekana kuwepo kwa dalili za rushwa hasa ikitiliwa maanani kwamba viongozi wote wa Mkoa wa Kusini, pamoja na maofisa mbali mbali wanaujua mradi huo tangu mwanzo wa ujenzi hadi kumalizika kwake, pamoja na uharibifu huo wa mazingira, wao walibaki kimya bila ya kuchukua hatua zozote zile. Hivyo, kamati yangu inamtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kushirikiana na Waziri anaeshughulikia masuala ya utalii, kumzuia mara moja muwekezaji huyo kutolitumia eneo hilo, kwani halikupata kibali kutoka kwenye taasisi yeyote ya serikali isipokuwa kuna *Stop Order* aliyopewa, na kwa kuwa anajua kuwa tayari ameshahonga wahusika, anaweza kufanya vyovyote atakavyo.

Mhe. Spika, kama hazitochukuliwa hatua za kumzuia muwekezaji kutolitumia eneo ambalo hakupatiwa kibali, hatutaiunga mkono bajeti hii, kwani tumeshasema sana na hata wananchi wa eneo lile tulipozungumza nao walilalamika sana, kuwa sisi viongozi tumeshawezwa na Muekezaji huyu, kwani kila kiongozi anaekwenda katika hoteli yake hupewa chakula na Soda na hakuna chochote kinachoendelea.

Mhe. Spika, kwa kweli tunashangazwa sana na mambo tunayoyafanya kwa sababu sheria ya mazingira inabainisha wazi, kuwa hata zile taasisi za serikali zinazochangia kuharibu Mazingira hutakiwa kuchukuliwa hatua, lakini cha ajabu uharibifu wa mazingira unafanyika na hakuna liwalo.

Mhe. Spika, ukweli wananchi wetu wanaofichua mashaka haya ya uharibifu wa mazingira wamekwishavunjika moyo kwani wanafanya kazi kubwa ya kufuatilia uharibifu huo na kutoa taarifa zenye ushahidi mzito na za wazi wa uharibifu huo kwa taasisi za serikali zinazohusika. Kwa ujumla wananchi hawa wanatushangaa sana na kutwambia kuwa tunapoteza muda wetu na fedha za serikali, kwa kutunga sheria ambazo zinaishia kwenye makabati, huku wageni kwa kushirikiana na wenyeji wakiyaharibu mazingira na kupelekea kuvimaliza visiwa vyetu.

Mhe. Spika, kwa taarifa ambazo tunazifahamu kutokana na mashaka tuliyonayo, Zanzibar imegeuzwa shamba la bibi kwa wawekezaji wageni kuyaharibu mazingira watakavyo na wapendavyo. Mhe. Spika, jambo la kushangaza wageni hao huchimba michanga fukweni huku wakiyaharibu mazingira na huuza mchanga huo kwa fedha nyingi kwa wawekezaji wageni wenziwao. Hali hii inasikitisha sana kwani mbali na nchi yetu kumalizwa kwa kutobolewa hapa na pale, Serikali imekuwa inayakosa mapato makubwa yanayotokana na uharibifu huo.

Mhe. Spika, hebu tujiulize, kwa mfano sisi tufanye makosa kama hayo katika nchi za wawekezaji hao, halafu ibainike kuwa tumetenda makosa hayo kwa mujibu wa sheria. Nini kitatokea? Kama si kuchukuliwa hatua na hasa ikitiliwa maanani wenzetu wanathamini sana masuala ya kuyahifadhi mazingira na usimamizi wa sheria, tofauti na sisi ambapo wengi wetu tunazungumza utunzaji wa mazingira mdomoni tu.

Mhe. Spika, umaskini wetu na uroho wetu usifikie katika hatua za kuvizamisha Visiwa vyetu, ambavyo kila leo kutokana na kuyaharibu mazingira vinapungua kieneo huku sisi wenyewe tukiongezeka kiidadi. Sasa tujiulize baada ya miaka 50 ijayo vizazi vyetu vitaishi katika pande lipi la ardhi ikiwa sisi wenyewe tunaamua kulibomoa?

Mhe. Spika, kamati inapongeza hatua zinazochukuliwa na Idara katika kuandaa rasimu ya kanuni ya kupiga marufuku uingizwaji wa kudhibiti uingizaji wa bidhaa chakavu za umeme, bila shaka kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Aidha, wazo la kuweka viwango vya uingizaji wa vifaa mbali mbali badala ya kupiga marufuku sio baya, lakini Idara iwe makini sana na suala hili kwa sababu sisi Zanzibar ni wazuri sana wa kupanga, lakini ni wabovu wakubwa katika utekelezaji. Tusipokuwa waangalifu Zanzibar itaendelea kuwa jaa la kila kitu. Kamati inaikumbusha Idara kuwa mara rasimu ya kanuni hiyo itapokamilika, itahitajika kuwasilishwa Barazani kwa ajili ya kupitiwa na Kamati ya sheria ndogo kama kanuni zetu za toleo la mwaka 2012 zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Idara ya Mazingira kwa kudhibiti uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki hapa Zanzibar, lakini bado kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao ni wakaidi wanakiuka amri hiyo. Kwa hiyo tunaitaka Idara kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaopatikana na hatia hiyo.

Mhe. Spika, kamati inaikumbusha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuipatia vitendea kazi vya kutosha Idara ya Mazingira hususan Pemba ambako hakuna usafiri wa kutosha kwa ajili ya kufuatilia masuala ya uharibifu wa mazingira. Aidha, kamati yangu inaona ipo haja Idara hii kwa upande wa Unguja ikajengewa jengo la kisasa kama ilivyo Idara yenyewe na umuhimu wake katika suala la kutunza mazingira. Mhe. Spika, ofisi ya Idara ya Mazingira iliyopo Maruhubi kiukweli hailingani na Idara hii na majukumu yake.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa watu wenye Ulemavu pamoja na changamoto zinazowakabili. Kamati kwa upande wake inazikumbusha taasisi za Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na taasisi binafsi kuitekeleza Sheria inayowahusu Watu wenye Ulemavu kwa kujenga au kuyafanyia marekebisho majengo yao, ili yawe na mazingira rafiki kwa wananchi hawa. Mhe. Spika, masuala ya watu wenye ulemavu yanamgusa kila mmoja wetu na hasa ikitiliwa maanani kwamba kila mmoja wetu anaweza kupata ulemavu wakati wowote. Hivyo, ni vyema kwa Serikali kuhakikisha kuwa Sheria zinazopitishwa na Baraza na ile Mikataba ya Kimataifa kuhusu watu wenye ulemavu inatekelezwa kwa vitendo.

Mhe. Spika, kamati yetu imebaini kuwa watu wenye ulemavu hawapati mikopo ya elimu ya juu kutokana na kuwepo kwa ushindani katika upatikanaji wa mikopo hiyo. Uhaba wa watu hawa katika ngazi ya elimu ya juu unaonekana wazi kwamba kiasilimia ni sawa na kusema hakuna wanafunzi wenye ulemavu wanaopatiwa nafasi hizo. Hata hotuba ya Mhe Waziri inadhihirisha wazi ya haya ninayosema. Mhe. Spika, kuna sababu kadhaa zinazochangia hali hii ikiwemo ya kutothaminiwa na utekelezaji mbaya wa elimu mjumuisho, ambao katika darasa moja huwajumuisha watoto wenye ulemavu wachache pamoja na wale wa kawaida ambao huwa wengi sana katika darasa. Hivyo ni vyema kwa serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuweka utaratibu wa kuwasaidia Watu wenye Ulemavu kwa kuwapatia mikopo, pamoja na nafasi za masomo katika viwango vya elimu ya Juu ili nchi yetu iweze kuwa na wataalamu mbali mbali kupitia watu wenye ulemavu.

Mhe**.** Spika, kuhusu elimu mjumuisho ambayo huwakwaza watoto wenye ulemavu, kamati inaitaka serikali kuangalia kwa kina suala hili kwa lengo la kuwafaidisha watoto hao kwani kamati yetu imebaini kuwa bado elimu hii haiwapi fursa watoto wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika masomo yao kama vile ilivyokusudiwa. Mhe. Spika, katika nchi zilizoendelea ambazo sisi tumeiga mfumo huo, zimeweza kufanikiwa kufikia malengo ya elimu mjumuisho kwa sababu ya kuwepo uwiano mzuri kati ya watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu, pamoja na mfumo mzuri wa elimu inayotolewa.

Mhe. Spika, mbali na ukosefu wa Mikopo na Nafasi za Elimu ya Juu. Kamati yetu imebaini kuwa wanafunzi wenye ulemavu hawana vifaa ambavyo huwasaidia katika masomo yao. Kamati ilibaini hilo katika skuli ambazo zinajumuisha watoto wenye ulemavu. Hivyo, kamati yetu inaona kuna haja kwa serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanapatiwa vifaa hivyo ili waweze kusoma kwa mafanikio.

Mhe. Spika, tunaipongeza serikali kwa kuongeza makadirio ya fedha za matumizi kwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Hata hivyo, kuna umuhimu kwa serikali kadri itavyowezekana kuisaidia idara hii kwa kuiongezea fedha zaidi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu nalo ni changamoto kubwa katika nchi yetu. Kuna baadhi ya watu huwabaka watu wenye ulemavu kwa makusudi na kesi zinapofikishwa kunakohusika huambiwa hakuna ushahidi, au ushahidi hucheleweshwa kwa makusudi kwa lengo la kuharibu kesi. Hali hiyo hupelekea jamii kukata tamaa kwa wabakaji kuendelea kutamba mitaani kwa kuendelea kuwabaka watu wenye ulemavu na kuongeza mzigo katika familia na jamii za watu hao. Kwa upande mwengine familia inayoathiriwa kwa kubakwa mtoto wao, kutokana na kupoteza imani kwa vyombo vya sheria, huchukua hatua mikononi mwao kwa kulipiza kisasi cha aina yoyote ile, ilimradi familia hiyo ijiridhishe kutokana na uovu alotendewa mtoto wao.

Mhe. Spika, kamati yetu, katika mwezi wa Mei mwaka huu ilipata nafasi ya kwenda Kisakasaka kumuona mtoto mlemavu aitwaye Msimu; ambaye alibakwa na baadae kufikishwa hospitali ambako alithibitika ana ujauzito. Mtoto huyu pia alipelekwa kituo cha Polisi Mazizini, ambako alitoa ushahidi wa dhahiri lakini Polisi wakasema asubiriwe azaliwe mtoto pamoja na majibu ya DNA ili upatikane ushahidi madhubuti. Polisi ilisema kuwa kipimo hicho ambacho alipimwa Msimu na yule aliyembaka kipo Dar es salaam tangu tarehe 13/03/2012 na majibu yake yatapatikana baada ya miezi 9.

Mhe. Spika, tunashangazwa na kauli ya Polisi ya kwamba ushahidi hautopatikana mpaka pazaliwe mtoto pamoja na kupatikana majibu ya kipimo cha DNA, ambayo huchukua muda mrefu kupatikana. Hivi ndivyo Sheria zinavyoelekeza au watu hujifanyia kazi kwa maslahi yao binafsi? Mhe. Spika, Mtoto Mlemavu yaani Msimu pamoja na kichanga alichokizaa hapati matunzo yoyote kutoka kwa mbakaji huyo kwa kuelewa kuwa hana kosa alilolifanya, ingawa Msimu kila anapoulizwa hata pale alipoulizwa Kituo cha Polisi Mazizini, bila ya kubabaika alikuwa akimtaja mtu aliyemfanyia kitendo hicho cha udhalilishaji.

Mhe. Spika, Kamati yetu inauliza serikali ni lini itachukua hatua madhubuti za kukomesha vitendo vya ubakaji kwa watoto wenye ulemavu na wengineo? Au tuiachie Jamii iendelee kuchukua hatua mikononi mwao? Kamati inaiagiza serikali kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Afya na Jeshi la Polisi kulifuatilia suala la Msimu ili aweze kupatiwa haki yake ya kisheria, lakini pia kuwezeshwa ili aweze kumtunza mtoto aliyemzaa kwa njia ya kubakwa.

Mhe. Spika, kamati inaiagiza Idara ya Watu Wenye Ulemavu pamoja na Jumuia ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, kushirikiana na Taasisi zinazohusika na masuala ya sheria pamoja na Tume ya Haki za Binaadamu, ili zipatiwe msaada wa kisheria na haki za Watu Wenye Ulemavu pale inapohitajika.

Mhe. Spika, kamati pia, inaitaka serikali kuchukua hatua iwezekanavyo kununua vifaa vya kupimia DNA, kwa lengo la kuondosha kero za ucheleweshwaji wa majibu lakini pia na kupunguza sababu ya kukosekana kwa ushahidi.

Mhe. Spika, kamati inaona kuna haja ya kuangaliwa upya Sheria inayowahusu Watu wenye Ulemavu hususan katika vifungu vya udhalilishaji na ubakaji, ili kuhakikisha kuwa sheria zinawabana zaidi wabakaji na wale wote wanaoharibu ushahidi katika kesi za udhalilishaji na ubakaji kwa Watu wenye Ulemavu.
Mhe. Spika, kwa mara nyengine naliulizia suala la ajira lakini sasa kwa upande wa Idara ya Watu wenye Ulemavu, tunaiuliza Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Je, ni Watu wangapi wenye Ulemavu kwa Unguja na Pemba wamefaidika na ajira katika Idara ya Watu wenye Ulemavu na taasisi nyenginezo za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30/06/2012?

Mhe. Spika, nauliza suali hili kwa sababu hotuba ya Mhe. Waziri haiainishi suala la ajira kwa watu wenye ulemavu katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Au watu hawa hawana haki ya kuajiriwa? Kamati inaamini kuwa wapo watu wenye ulemavu ambao wana sifa za kuajiriwa katika serikali, lakini vile vile kwa upande wa Pemba tatizo hili ni kubwa sana katika Idara hii. Wafanyakazi waliopo hawatoshi hivyo kuna haja ya kuongezwa wafanyakazi wengine.

TUME YA KURATIBU NA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza idara hii kwa kazi kubwa inayoifanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, katika kupambana na kuzuia dawa za kulevya. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili Idara hii pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuwa na uhaba wa vitendea kazi, pesa za mafuta na mafunzo. Hivyo, kamati yangu inaiomba serikali kuiwezesha idara hii, pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuzipatia vitendea kazi vya kutosha yakiwemo magari na pesa za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya gari.

Mhe. Spika, pia kuna haja kwa Jeshi la Polisi kupatiwa mbwa wengine ili wasaidie katika ukamataji wa wasafirishaji wa dawa hizo, kwani tunaamini kuwa mbwa mmoja ana uwezo mkubwa wa utambuzi kuwashinda binaadamu wa kawaida. Pia tunaiomba serikali kukipatia Kitengo cha Madawa cha Jeshi la Polisi pikipiki, ili kiweze kukabiliana na harakati za kupambana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, tunawapongeza wale wote waliojitolea kuanzisha nyumba za kurekebisha tabia (*Sober Houses*), kwa lengo la kuwasaidia kuwarejesha kwenye hali ya kawaida wale waliojiingiza kwenye janga hili la utumiaji wa dawa za kulevya**.** *(Makofi)*

Aidha tunaipongeza Serikali kwa kuandaa muongozo wa kuanzisha na kusimamia *Sober Houses* hizo hapa Zanzibar. Pamoja na kuchelewa kupata fedha za uandaaji wa Sera za Dawa za Kulevya.

Tunaishauri serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuendelea na jitihada hizo, kwani bila ya sera madhubuti basi hata ugawaji wa majukumu unakuwa mgumu, kwa sababu kutakuwa hakuna muongozo maalum kwa kila mtu, kwa fikra kuwa jukumu hilo si lake bali ni la wenzake.

Hali hii hatimaye inapelekea kuwa na nchi yenye rasilimali watu wengi wasiokuwa na uwezo wa kuzalisha kiuchumi, kutokana na kubobea kwa muda mrefu katika matumizi ya dawa hizo.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Tume hii kwani imesaidia kudhibiti ongezeko la maambukizi mapya. Hata hivyo, tunaiomba Tume kuendelea kushirikiana na Jumuia zinazohusika na masuala ya UKIMWI ikiwemo *ZAPHA+*, kwa lengo la kusaidia kwa hali na mali katika harakati zao za kujiendeleza kiuchumi na kijamii pamoja na kupambana na maambukizi mapya.

Aidha tunaiomba serikali pamoja na Tume ya UKIMWI Zanzibar kuisaidia miradi ya *ZAPHA+* ukiwemo ule mradi wa kutengezea sabuni uliopo Mkoani Pemba, ambao umelala kitambo kutokana na kuharibika kwa mashine na Jumuia kutokuwa na fedha za kuitengeneza mashine hiyo.

Vile vile tunamuomba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais watakapozuru Pemba kikazi, wasisahau kuipitia Jumuia hii pamoja na mradi huo uliopo Mkoani, kwa lengo la kuwahamasisha na kuwajali katika harakati zao za kujiendeleza kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, tunaiomba serikali kuanza kutenga fedha za mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI, kwani wafadhili wanaochangia masuala ya UKIMWI wameanza kutishia kusitisha misaada yao kwa Tanzania.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati, tunakushukuru na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi jioni ya leo na kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea taarifa hii, ambayo ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jana au juzi kama sijasahau nilikuwa nikimsikiliza Mhe. Mwanasheria Mkuu japo kuwa anatoka kidogo, alisema kuwa Sheria za Ardhi kidogo zina mapungufu na mimi nakubaliana naye. Lakini nikiangalia na hii Sheria ya Mazingira naona ipo haja ya kuweza kurekebishwa, ili ziende na wakati, katika ukurasa wa 19 kifungu cha 60.

Mazingira ni mazingira Mhe. Spika, hivi sasa duniani watu wanaelezea jambo kubwa suala la mazingira. Lakini pale panapo tija Mhe. Spika mazingira huwa hayapo, kwa sababu panapo tija huwa hayapo. Kwa mfano, utakuta nchi zetu hizi za Afrika kwamba uchumi wetu mwingi tunategemea katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Spika, wenzetu wana kila aina ya vivutio vya kuwaita wateja wao kutoka nchi za nchi, wanavyo vishawishi vingi. Kwa kweli mara nyingi sana husema kwamba na sisi Waheshimiwa, kwa sababu siku moja alisema Mhe. Mussa Ali Hassan alikuwa akiomba safari, lakini lengo si kwenda kuona nchi tu, isipokuwa ni kwenda kuangalia jinsi gani wenzetu wanavyoendelea siku hadi siku.

Mhe. Spika, nilikwenda Italy sehemu ya *Venice* nimekuta nyumba ziko kwenye bahari. Kwa kweli wenzetu wanatia fedha kama hawana akili vizuri. Lakini sisi leo akitokea mtu kusema kuwa kisiwa ajaribu kukiboresha au kukitengeza kwa mujibu wa mazingira yawe mazuri, basi tunasema mazingira tunaharibu.

Kwa hivyo, ndipo pale niliposema kwamba penye uchumi mazingira tuweke mbali na sheria nazo tuziboreshe, tuzitengeneze vizuri Mhe. Spika, na wala sina haja ya kusema kwamba tuharibu mazingira hapana.

Mhe. Spika, sheria kwanza lazima uanze kufanya utafiti wa lile unalotaka kulifanya, ili kuweza kuleta mazingira mazuri. Naamini vizuri kwamba wataalamu wapo na wanaweza kufanya hivyo.
Kwa mfano wenzetu kama Wataliana wanapowekeza mahoteli yao, Mtaliana haoni raha au kuja kwa wingi kama hajaona kitu kinachoitwa *Pontille*. Mhe. Spika, hiyo *Pontille* ndiyo inayowafanya wenzetu waweze kuja hapa nchini hasa Wataliana kwa ajili ya kufuata kitu kile.

Lakini ukienda kwenye mazingira, utaona ni kitu ambacho kinaharibu mazingira, kwa upande wa kutafuta fedha kwa ajili ya kujiondolea umasikini katika kisiwa chetu inakubidi uiruhusu pontille ijengwe, vyengine vyovyote Mhe. Spika tutawakosa hawa wawekezaji wa Kitaliana na wala hawatojisikia raha kama kitu hiki hakijafanyika.
Kwa hivyo, ndio maana nikasema hizi sheria zetu tunavyoziweka hebu tuziweke vizuri na tuzitengeneze, kuna mambo Mhe. Spika lazima yafanyike. Kwa mfano, wenzetu China wameweka tuta kwenye bahari, lakini wameweka tuta lile kwa mantiki yao, kuwa pale kuna suala la uchumi na wenzetu wanajua masuala ya mazingira duniani na wao ndio wa mwanzo na sisi wala hatuwafikii, lakini wamefanya kwa maslahi ya nchi yao katika masuala ya uchumi.

Mhe. Spika, na sisi wenzetu wanapofika pahala na kupatengeneza na pakawa pazuri, basi naamini na sheria ione kwa sababu mtu anaweza kwenda pahala pabaya sana, lakini anafika pahala na kupajenga vizuri na kupatengeneza. Sasa mimi sioni haja kwamba yule mtu azuiliwe na asipewe nafasi ile.

Kwa maana hiyo, ni lazima apewe uwezo ule na sheria imruhusu, ili tupate tija, vyenginevyo vyovyote Mhe. Spika tutashindwa kufanya, kwa sababu mambo mengi hata kwenye ukumbi wako humu utaambiwa mazingira tunavyofanya sivyo kama vile kukata au tunachana karatasi pamoja na mambo mengine.

Sasa tutafanya nini sisi Mhe. Spika wakati tumelazimika kuja hapa kwa ajili ya kutunga sheria kwa lengo la kuwasaidia wananchi, ukitizama mazingira tunao haribu ni sisi hapa.

Mhe. Spika, pia ukiangalia kwenye Baraza lako tukufu. Kwa mfano, leo kuna kitu kimetokezea ambapo mwenzetu mmoja alitapika humu Mhe. Spika na wewe hukuona, lakini hakuna kitu cha kuweza kumstiri kimazingira.

Kwa hiyo, ndani ya ukumbi huu mna kasoro kwa sababu ni vitu ambavyo kwa mfano, ikitokezea Mhe. Spika kwa sababu mambo mengine hayaleti taarifa yanakutokezea tu, kama mimi siku moja nilipigwa na tumbo la kuharisha na ilinitokezea tu, kwa sababu nilikuja vizuri mzima na kuweza kuchangia vizuri, lakini Mwenyezi Mungu alileta mtihani wake na tumbo likanibiruka.

Vile vile naweza kukaa hapa ikanijia kitu kichefu chefu kikatapika Mhe. Spika, na hapo tayari nimeshaharibu mazingira. Kwa hivyo, tunaomba na hili litizamwe katika ukumbi wetu vitu kama hivyo ya kuweza kutusaidia iwepo. Halikadhalika na mambo mengi katika mazingira Mhe. Spika, kwa mfano mimi nianguke nani ataweza kunibeba nyinyi, lakini kukiwekwa kitu kizuri cha kubeba mtu na kumtoa nje basi nayo ni mazingira mazuri pia.

Kwa hivyo, nafikiri suala la mazingira lina mambo mengi sana na nikisema leo niyachambue basi utanipa nafasi mpaka kesho, kwa sababu suala la mazingira ni pana sana, lakini sisi tunalichukulia tu kama ni *simple case* na hivyo sivyo.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nilisema kwamba lazima tuandae sheria za mazingira ambazo zitaweza kutusaidia, kwamba tunaweza kukiona hiki ni kitu kizuri, basi Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wakatoa fursa ya kuweza kufanyika.

Mhe. Spika, pia nikubaliane na Mhe. Waziri kwamba kweli watu hivi sasa wanachimba mchanga bila ya *plan*, hawafuati sheria au hawaendi katika Idara husika ama kwenye jopo ambalo linalotoa ruhusu ya kuchimba kwa utaratibu, watu wanapita na gari zao kisirisiri. Kwa kweli watu hawa bado hatujawatia adabu, kwa sababu *majority* gari nyingi ni zenu nyinyi Waheshimiwa tuambizane ukweli.

Kwa mfano, gari leo ikikamatwa ya Mheshimiwa imekwenda kuiba mchanga na kuharibu mazingira, basi inapigwa simu haraka sana wewe huijui gari yangu itoe hiyo. Mhe. Spika, mambo mengine na sisi wenyewe tujiseme, wachafuzi wa mazingira *number one* na sisi tumo na hilo lazima tulizungumze.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala hili lazima tu-*stick* na sheria hapa, kwamba huyu Mheshimiwa mwenye gari lake ndiye wa kumpiga faini au kumtaifisha hasa, kwa sababu ndiye muanzilishi wa uchafuzi wa mazingira hayo. Mhe. Spika, nitafurahi sana na Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho kwamba kuna gari zaidi ya 5 za Waheshimiwa nilizipiga faini kiasi kadhaa, na mimi nitafurahi sana na hotuba yake nitaiunga mkono, naomba unifanyie hivyo au unipatie idadi hiyo.

Vile vile kuna suala la ukataji wa misitu ovyo. Mhe. Spika, ushauri wangu kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais tungekuwa na plan hasa hawa watu wanaochimba mchanga hawa, kwamba yule mtu ambaye mwenye shimo lile wakati watu wanakwenda *step* ya pili, basi yeye *step* ya kwanza aanze kupanda miti na wala tusisubiri likaendelea na mpaka baadae likashindikana.
Kwa mfano, kwenye picha ambayo iko kwenye kitabu cha hotuba yako umetuonesha hatari ya watu wanavyochimba, na hiyo ni hali halisi na wala hakuna dalili ya kupandwa miti.

Lakini sheria ya mwanzo kabla mtu hujampa kibali basi mtu aambiwe hivyo, unapochimba uhakikishe *step* ya kwanza imemalizika unakwenda *step* ya pili, basi lazima ipandwe miti haraka sana iwezekanavyo, nadhani hapo kidogo tunaweza kusaidia.

Mhe. Spika, pia na hawa *contractor*s wa barabara, wamechimba sehemu nyingi sana na wala hawana marejesho ya kufanya kwamba angalau waoteshe miti nalo hilo ni kosa. Inavyosemekana Mhe. Spika, huwa wanalipa fedha, lakini fedha hizo zinakwenda wapi? Zinakwenda kwenye Idara ya masheha, na kama zinakwenda kwa masheha kwa nini wanashindwa kuunda kikundi cha kuweza kufanikisha suala hilo, hayo mambo yanayotakiwa yafanyike katika eneo lililoharibikiwa.

Mhe. Spika, hata mimi niunge mkono suala la ubebaji wa mchanga katika fukwe, tena naunga mkono kwa asilimia mia moja. Kwa kweli kuchimbua bahari bila ya kupata taaluma ni kuharibu mazingira, na tena ni kuhatarisha maisha na unaipa nguvu ile bahari ije kwa nguvu sana katika eneo lile. *(Makofi)*

Lakini ukipitia kwa wataalamu wanajua jinsi ya kuweza kukusaidia wewe, kwa sababu wengine wanakwambia tatizo la bahari kwamba tunachimba, ni kwa sababu bahari inakula kuta zao, ndio lakini wataalamu wapo waulize jinsi gani ya kuweza ku-*block* mambo hayo.

Mhe. Spika, naomba nimuunge mkono Mhe. Waziri kuhusiana na suala hili tena bila ya wasi wasi wowote, na niko pamoja na yeye bega kwa bega na hatari hiyo hivi sasa wanafanya Kiwengwa watu wenye mahoteli.

Mimi naitaka fedha, lakini kwa hali hii sikubaliani nayo, ndio maana nikasema kwamba tuchague kwa sababu kuna mambo mengine yanaweza kutusaidia katika kuinua uchumi, na mambo mengine yasituharibie mazingira kwa kutaka fedha tu, twende huku na huku.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 19, kifungu cha 68. Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri kwa kuwahusisha Rasimu hii ya Kanuni ya Kupigwa Marufuku ya Uingizwaji wa Bidhaa Chakavu za Umeme (*Electronic*), kwa sababu sasa Zanzibar imekuwa ni *damp* kubwa sana la kutupwa uchafu wa vitu kama hivyo, nakubaliana na Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, juzi moja nilishuhudia mwenyewe hata haya magodoro, basi kweli Zanzibar tuwe na upungufu wa kupata magodoro. Kwa kweli magodoro hayastahiki kwa sababu mengine ukitaka kuyaangalia ni kinyaa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, asimamie kidete suala hili, ili aweze kuondosha tatizo kabla hayajatufika maradhi, kwa sababu bora kinga kuliko tiba.

Vile vile kwenye ukurasa wa 24 Mhe. Mwenyekiti wangu hapa aliyeondoka alizungumzia sana kuhusu suala la walemavu. Mhe. Spika, nasikitika sana kwamba bado walemavu kusema ukweli hatujawatendea haki, na hili tuseme na wala sisemi kwa woga, isipokuwa nasema kweli kwa sababu mimi hivi sasa miaka yangu si chini ya 48 mpaka 50, lakini katika mazingira ambayo sijaona hata ofisi moja ambayo ina mwelekeo wa watu wenye ulemavu kuweza kupanda juu ya ghorofa.

Pili twende katika ajira wazee wangu tumewatupa sana. Kwa kweli Mhe. Spika inasikitisha kwamba mfano ukifanya sensa kwamba wangapi wenzetu watu wenye ulemavu katika wizara zetu utapata kidogo sana na hali hii inasikitisha sana. Mhe. Spika, sijui niseme vipi kwamba serikali haina fedha ya kuweza kuwaajiri, na kwa nini tusiwape kipaumbele wao kuliko sisi wazima, kwa sababu kila kukicha unasikia ajira, lakini wao hawaajiriwi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tukiondoka hapo twende kwenye Elimu ya Juu. Hivi Mhe. Waziri anaweza kuniambia kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuna walemavu wangapi ambao wamepata elimu ya juu kuhusu masuala ya mikopo pamoja na kupata taaluma hiyo. Sasa kama wako kidogo basi nitamsitiri asiseme kwa sababu ni aibu na kama wengi basi namuomba anijibu, ili nifurahike nafsi yangu kuona kama kweli hotuba yake hii inalingana na kutaka kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kuhusu ndugu zetu walemavu lazima serikali hivi sasa igeuke kama Wizara ya Fedha wamekupa fedha kidogo, basi nitakupigia debe upewe fedha nyingi, ili uweze kuajiri hawa ndugu zetu walemavu na hili ni lazima Mhe. Spika, kwa sababu ni sote tuna upungufu wa baadhi ya viungo, na hata na sisi walemavu tuseme ukweli na nani asiyekuwa mlemavu hapa.

Kwa hivyo, ikiwa na sisi tunajihisi kama ni walemavu, basi ni sawa na wenzetu walivyo na wala tusiwanyime haki Mhe. Spika.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri afanye kwa makusudi awakusanye na awaweke katika sehemu nzuri ambayo itakayowasaidia kimaisha kwa ajili ya kuwakomboa.

Kwa mfano, kuna mifuko mingi sana ambayo inaweza kuwasaidia kama vile *TASAF*, wengine wale waliokuwa katika na siku moja nataka kusema, lakini nasubiri katika Wizara ya Fedha hata hii *ZSSF* nayo ingekuwa na uwezo wa kutoa mikopo ya kuwasaidia hasa ndugu zetu walemavu ambao ni *members*, kwa lengo la kuondokana na umasikini na riba yao iwe ndogo, kwa sababu riba ni kubwa sana.

Mhe. Spika, suala hili la riba kuwa kubwa bado Waheshimiwa wetu hawajaliona, yaani riba ni kubwa sana nadhani ni vyema Mhe. Spika angewapigia debe Mhe. Waziri, na sisi wacha tupewe riba kubwa potelea mbali, lakini hawa ndugu zetu lazima wawekwe kwenye mustakbali mzuri na kuundiwa vikundi vyao vizuri kwa ajili ya kujiendesha kimaisha, lakini kwa kupata mkopo riba ya chini.

Kwa mfano, wenzetu kule Bara Mhe. Waziri hivi sasa wanafanya kwenye benki zao, wanawasaidia wafanyabiashara wa hali kama hizo za chini na sisi bado serikali yetu haijaamka kutafuta mbinu za aina hizo.

Mhe. Spika, hivi sasa *PBZ* nani asiyejua kwamba tayari inapata faida ndani ya faida, mimi peke yangu tu mkopo niliochukua *PBZ* tayari nimeshaitilia faida kwa nini ishindwe kutoa ruzuku kwa ajili ya watu wenye ulemavu, halikadhalika na benki nyengine. Kwa kweli si kitu cha mchezo na hawa ni ndugu zetu lazima tuwajali, tuwape fursa zote pamoja na haki zote zinazostahiki kama tunavyopewa sisi na wao wapewe.

Mhe. Spika, wengine utakuta hawana sehemu ya kulala, wanahangaika na vigari njiani na wewe Mhe. Spika utatokwa na machozi, jinsi vile wanavyohangaika na wala hawajui waende wapi kwa ajili ya kupata njia ya kuweza kujisaidia.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba tufanye sensa na tuwajue wangapi, ili tuweze kuwasaidia na wala isiwe sensa hiyo iishie kwenye *briefcase* au meza zetu, na lazima tufanye hivyo na mimi niko-*serious* na jambo kama hili na wala si kitu cha mchezo kwa sababu nimewaona jinsi wanavyo hangaika ndugu zetu.

Mhe. Spika, naomba na ikiwezekana basi tuwatengee Nyumba maalum, na tuitengeneze vizuri na kwenda kuwaweka katika eneo la Nyumba ya Wazee Sebleni itasaidia. Kwa mfano, wengine wanafukuzwa kwenye nyumba wanazopanga, yaani mtu hafikiri kwamba yule mtu ambaye ni mlemavu basi nimsaidie na matokeo yake anamfukuza na kumwambia toka kwenye nyumba yangu hulipi kodi, hivi yule aende wapi Mhe. Spika na nchi yake ni hii.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba hicho kitu ajitahidi sana na kuweza kuwasaidia hao, ili waondokane na dhuluma hizi wanazofanyiwa, kwa sababu sisi ndio tunaona Mhe. Spika, kwenye maeneo yetu. Vile

vile sisi ndio tunaowasaidia na posho tunalopewa ni dogo, lakini tunawasaidia hivyo kidogo na sisi tuongezeeni posho jingi, ili tuwasaidie wao kama serikali haiwezi basi tupeni sisi, ili mtusaidie na kuwasaidia wao.

Kwa hivyo, tunaomba hilo Mhe. Spika kwamba Waheshimiwa Wajumbe tuongezwe posho, ili tuweze kuwasaidia hao ndugu zetu walemavu, kwa sababu sisi ndio watu wa mwanzo kuwasaidia na halafu baadae watakuja kwenye chombo kinachohusika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, na ninavyomfahamu kwamba ataweza kulikazania na kulifikisha pahala panapostahiki.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la dawa za kulevya. Mhe. Spika, hapa ndipo panapo kifo cha wenzetu. Kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kwamba afanye ziara kwa makusudi shehia hadi shehia, unajua binadamu wakati mwengine anaweka kitu ili kufurahishe kwa binadamu wenzao, na kuna njia za kijamii ambazo ni nzuri na *security* nzuri sana Mhe. Spika za kuweza kusaidia mambo ya maovu ambayo ni hatari kwa maisha.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar pamoja na *IGP* wake kwa kuleta kitu ambacho kinaitwa Polisi Jamii. Mhe. Waziri hii itakusaidia katika masuala ya dawa za kulevya, hivyo ni vyema waite. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo nimemsikia Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ametamka rasmi kuitambua, leo na hivi sasa sijui kama haijafika mwaka hii Polisi Jamii ipo ndani ya Zanzibar, na wala silaumu ndio mambo, kwa sababu binadamu sio sote ambao tunaona, yaani unaweza kuvaa miwani, pengine mtu hanioni au inaweza kuwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary kumbe hanioni, na ndivyo ilivyo utazamaji wa kila mtu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aviimarishe hivi vikundi na kazi yake itakuwa ni ndogo tu iliyobakia, tena mwakani bajeti yake itapita vizuri sana, na wala haitokuwa na mikiki na hata leo itapita vizuri tukikubaliana na masuala yangu ambayo tunayokwenda sambamba.

Kwa hivyo, hawa jamaa wa Polisi Jamii na kuwa-*train* vizuri, atawasaidia *funds* kwa kupitia njia na wala si lazima kwenye mfuko wake hata kwa *donors*, tuwatafutie na tuwasaidie. Mhe. Spika, suala la unga nakupa *gurantee* haitatimia mwaka hapa tutafanikiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana sihaba. Kwa mfano, kuna watu wameanzisha hizi *Sober Houses*, na kuna mama mmoja jina lake limenitoka, lakini nampa pongezi kubwa sana Mhe. Spika, na huyu sijui serikali imemuona mama huyu na kumsaidia vipi, baada ya fikra yake kuizaa, baada ya yeye mmoja na hivi sasa kuna nyumba 9.

Lakini hiyo haitoshi na kwa nini serikali isitafute eneo ikajenga *special* hizo *Sober Houses* zikawa kubwa na kuliko nyumba ndogo ndogo, kwa sababu mule mutatoka ajira miongoni mwa wale wataajiriwa. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika fungu hili alitafute na *donors* wapo na hata mimi niko tayari ninao wengi *donors* wapo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Tatizo letu wengine inatupiga chenga kuandika *Project Write Up* na mimi naweza, basi wache waje na tuandike *Project Write Up* na tutengeneze hicho kitu, naomba tupewe eneo kwa ajili ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, naomba sana na kumalizia dakika zangu tano na hapa ndipo ninapokomaa. Kwa kweli Mhe. Waziri atahadhari sana kuna jambo ambalo watu wakipeleka taarifa kwenye Vituo vya Polisi wanakuwa wanawasema, na hivyo hawa polisi uwe *attention* nao, kwa sababu wanamwambia yule muuzaji kwamba amekuja fulani hapa kuja kusema kama unaendelea kuuza na wala hiyo si tabia nzuri.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikasema kwamba Mhe. Waziri aende kwa Polisi Jamii na itaweza kumsaidia, kwa sababu wale Polisi Jamii wamo katika shehia ile na wanajua mazingira yote kwamba nani anauza au yupi anakula.

Mhe. Spika, niipongeze sana Polisi Jamii ya Kwahani, kwa sababu zamani Kwahani ilikuwa hatari, lakini hivi sasa *Alhamdulillah* unaweza kujivuta kidogo na kisimu chako cha shilingi 70,000/= ukafika nacho katika mtaa mwengine, kwa kweli Polisi Jamii ya Kwahani imejitahidi na kujaribu kupunguza wimbi hilo la vijana kula unga na kuingia kwenye masuala ya wizi.

Mhe. Spika, nakubaliana na wewe kwa muda ulionipa, lakini bado ninayo mambo mengi. Kwa hivyo, namuunga mkono Mhe. Waziri wangu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniruhusu niweze kusema mambo mawili matatu katika Hotuba hii ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Kwanza naomba nitumie fursa hii kuipongeza ofisi hii na shughuli zake, pamoja na watendaji kwa jitihada zao wanazozifanya katika utekelezaji wa shughuli zao. *(Makofi)*

Pili niende moja kwa moja kwenye hotuba hii na nizungumzie kuhusu Idara ya Mazingira. Mhe. Spika, mazingira yetu yako hatarini sana na ardhi yetu ndogo ya visiwa vya Unguja na Pemba kila siku zikipita vinaendelea kudidimia baharini. Jambo la kutia hofu sana sijui hatimaye tutakaa wapi. Nimetishika sana na maeneo 148 ya Visiwa vya Unguja na Pemba ambayo tayari yameshaingiliwa na bahari. Hii ni hali ya kutisha sana kwa kweli. Nadhani kama wataalamu watapima sasa kilomita za mraba za visiwa vyetu hivi kwa kweli tutafika pahali tuanze kujiuliza nini hatima ya vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, siku moja nilikwenda Uroa miaka ya 1986, nina rafiki yangu kule alinialika nimtembelee kijijini kwao. Lakini tukawa tumekaa barazani hivi wakati maji yalipokuwa yanajaa nikaona yale maji yanakuja mpaka pale kwenye miguu yetu. Nikamuuliza sasa nyinyi mmejenga hapa vipi, hamkuona kama ni bahari hapa. Basi akanionesha mahali panapofika kilomita tatu usawa wa baharini kule akanambia mji huu ulikuwa kuleeee, lakini kila siku zikenda maji yanachukua eneo na sisi tunasogea huku na hapa halafu tutahama tutaelekea huku. Ni masafa marefu Mhe. Spika, na huko walipokuwepo mwanzo. Akanambia sababu ya lile jina la Uroa basi sababu yake ni kwamba ule mji wao uliroa maji ndio wakaita Uroa.

Sasa ni hivyo hivyo na maeneo mengine. Nilikuwa naangalia kiambatisho Nam. 8 nikakumbuka taarifa nilizozipata hivi karibuni za Kisiwa Panza. Kule kuna eneo la makaburi, lile eneo sasa hivi kuna Kamati maalum wana kijiji wameiunda kwa ajili ya kila maji yanapotoka wanakwenda pale ufukweni na wakienda wanakwenda kuokota mifupa ya watu ambao tayari kaburi zao zimeroa, wanachukua wanakwenda kuzika pahali pengine.

Hata hapa Mbweni Mhe. Spika, bahari hii hapa miaka ya 1980 nilipokuwa nasoma hapa nilikuwa nakwenda pwani kuogelea nikawa nakuta mashina ya minazi yapo ndani ya maji. Nikawa nauliza yalikuwaje? Nikaambiwa kwamba hapa palikuwa ni juu lakini sasa maji yamechukua. Kwa hivyo hii hali ni hali ya kutisha sana.

Sababu zipo nyingi Mhe. Spika, lakini sababu mashuhuri kwanza ni hii tabia ya nchi ambayo sisi kama Wazanzibar kwa kiwango kikubwa hatuna uwezo nayo. Maana hali hii inatokana na watu wa dunia ya kwanza huko ambao ndio wachafuzi wakubwa wa mazingira. Sasa tumeambiwa majabali ya mabarafu yaliyokuwepo miaka milioni na milioni sasa yanayayuka na yanaongeza maji baharini. Sasa hili ni jambo ambalo sisi hatuna uwezo nalo.

Lakini kuna mambo ambayo hapo ndani ya uwezo wetu na kama alivyoeleza Mhe. Waziri humu basi tunapaswa tufanye jitihada kubwa sana katika kuyasimamia. Kwa mfano kuna wimbi la ukataji wa miti, kuna kipindi kabla sijawa mkubwa nilikuwa nikivua kule kwetu Pujini. Nilikuwa nikenda baharini nikichokoa pweza, sasa palikuwa na pori kubwa kweli kweli la kutisha la mikoko. Lakini miaka ya hivi karibuni nilikwenda Mhe. Spika, unaweza ukalia machozi, hakuna mkoko hata mmoja, yote watu wameshaikata, wameshafanya majengo, wameshafanya mkaa. Sasa maji yanavuka yanakuja zake juu na ndio maana hata Pujini Kibaridi imeorodheshwa kwamba nako bahari sasa inakuja juu.

Mhe. Spika, kwa kweli ni tatizo kwa sababu ukitizama yale yanayofanya mpaka watu wakakata mikoko na miti mengine ya juu ni kwa sababu ya hali mbaya ya maisha, wanafanya vile wapate kuishi. Lakini kwa upande mwengine wazee walisema ukichelea mwana kulia basi utalia wewe. Tunapaswa tuwaonee huruma lakini tunapaswa tuwazuie wasiendelee kukata miti. Hapa ndio kwenye changamoto kubwa ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa sababu kuna wakataji miti kwa ajili ya nishati ya kupikia.

Kule vitongoji kunawachimba matofali, hawa wote ni watu wamejiajiri wenyewe kwa kutafuta rizki, lakini tukiendelea kusema wamejiajiri tukawaachia basi siku moja tutakuja kufanya tathmini tukute tumeathirika sana kwa sababu hizo. Changamoto iliyopo nafikiri Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itafute wataalamu wabunifu sana, watafute njia mbadala ya kuwawezesha wananchi wale kupata maisha yao kwa njia nyengine sio kwa hii. Lakini kwa kweli sasa hivi hatuna njia nyengine ni lazima masuala haya tuyasimamie ipasavyo.

Mhe. Spika, kuna tatizo la misumeno ya moto, nayo ni nyenzo moja muhimu kweli kweli ambayo kwa kweli inamaliza miti. Hivi karibuni Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ilitangaza marufuku ya misumeno ile. Lakini tuna tatizo, kwanza tuna tatizo Wazanzibari ni watu tulio na mabezo sana, tukiambiwa jambo huwa hatuamini mpaka litufike. Lakini tatizo la pili tunakabiliwa na tatizo kubwa zaidi la usimamizi wa sheria Mhe. Spika. Muhali Wazanzibari tumeufanya mwingi.

Hivi karibuni nilitembelea jimbo langu maeneo ya Kilindi, baada ya lile tangazo la marufuku, basi wale wenye misumeno ya moto waliokuwa maeneo ya barabarani huku, maeneo ya Kaskazini wote wamehama wamekuja kuhamia jimboni kwangu Kilindi. Nilisimama pahali nikasikia sauti zaidi ya pande nne huku inatoka sauti ya kukatwa kwa msumeno, huku inatoka, huku inatoka, nikakamata mikono kichwani nikasema *Lailah Hailallah,* hii hatari kubwa itakuwa. Sifa ya msumeno ule hauna siri mtu kilomita tatu mpaka kilomita nne anaweza akausikia ule msumeno. Na maeneo yote ndiyo yale yenye makarani wa misitu ambao ndio kazi yao kusimamia ile misumeno.
Mhe. Spika, kwa lugha fupi kabisa ni kwamba wale makarani wanakula rushwa. Akisikia msumeno unalia sawa sawa na paka aliyesikia ile honi ya muuza dagaa anaikimbilia mbio. Akifika yeye haendi kumzuia mtu asikate, anakwenda kumwambia nipe chochote nikuachie ukate. Kwa hivyo kwa kutumia makarani wale mimi nadhani hatutofanikiwa. Nafikiri Mhe. Waziri pamoja na Afisi yake na watendaji wake watafute njia nyengine ya kusimamia misumeno ya moto, lakini ni hatari mno, inamaliza miti.

Mhe. Spika, hii Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais nadhani ingetumia juhudi zaidi za kuwaelimisha wakulima wetu. Kwa sababu kule Pemba kilimo tulivyozowea ni kilimo cha kufyeka msitu tukapanda pale kwa kutumia mbolea ya msitu ule kwa siku nyingi. Lakini baada ya miaka miwili ile mbolea imekwisha pale tunapaacha tunakwenda kutafuta msitu mwengine tunafyeka tena. Hiyo nayo pia ni njia moja ambayo inatumalizia misitu. Wakulima kama hawa wanahitaji kusaidiwa kwa taaluma lakini pia na uwezo wa kuweza kuitumia ardhi ile kwa muda mrefu zaidi. Nafikiri nayo inaweza ikasaidia.

Lakini pia na Makampuni haya yanayokuja kututengenezea miundombinu ya barabara nayo inatusababishia mashimo makubwa sana. Nadhani kama Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi atapata nafasi ataweza kulisema kwa vizuri sana, bora nimuachie mwenyewe.

Mhe. Spika, nataka niipongeze Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa jinsi walivyosimamia mifuko ya plastiki. Ile mifuko ilikuwa imetuchafulia mazingira katika kiwango cha kutisha. Sasa hivi ukenda sokoni ukishakununua kitu, ukimwambia mfuko bwana huu, anakwambia huo bwana marufuku, kila mtu anakwambia marufuku. Natoa pongezi kwa sababu ufatiliaji hapa ulikuwa makini sana. Katwambia wamewafikisha watu Mahakamani si chini ya 192 na wamepata karibu milioni 7 na laki 6 zipo katika Mfuko wa Hazina, ni jambo la kutia moyo sana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nalo ni janga kwa sasa hivi ni hili suala la bidhaa chakavu za umeme (*used*). Bidhaa hizi wenzetu ni ajira yao kwa sababu wanapata rizki yao. Lakini ni kweli alivyosema Mhe. Waziri wanakwenda kule wanakunja madubwesho mengine yanauzika mengine hayauziki. Ukipita kwenye maduka ya namna hii unakuta kama jaa, kuna midubwasha tele imetupwa wala mtu hajui akaipeleke wapi.

Naunga mkono sana hii hoja kwamba lazima sasa tuangalie viwango vya zile bidhaa chakavu, ionekane hizi tunaweza kuziruhusu kwa sababu watu wanatafuta rizki lakini yale mengine bora yasije katika nchi yetu, Kisiwa chetu kidogo hatuna majaa. Naomba sana washirikiane na Wizara ya Biashara, bidhaa zinazokosa viwango sio

chakavu peke yake, nyengine ni mpya kabisa lakini hazina viwango, unaweza ukanunua leo kesho ukatupa haifai tena.

Nilikuwa naomba na bidhaa mpya nazo zisimamiwe ipasavyo kwa sababu wenzetu wamezowea kwenda kutafuta madubwasha rahisi wakatuletea huku, madubwasha mabovu yakija hapa ni hasara tupu. Unaweza ukanunua jambo leo kwa pesa nyingi kesho halifai, nafikiri bora tuweke mikakati, haidhuru wataleta hoja kwamba watu wa kununua bidhaa nzuri hawapo, hawana pesa Wazanzibari. Mimi nafikiria kununua bovu mara nne bora kununua nzima kwa mara moja japo kwa bei kubwa. Kwa hivyo nalo naomba sana lisimamiwe.

Jambo jengine ambalo kwa kweli ni lazima serikali tukubali kwamba hili sasa ni changamoto. Tumepewa maelezo mara kwa mara hapa kwamba kuanzia mwezi sijui wa Disemba au sijui mwezi gani, tunaanza kutumia mitambo ya *digital*. Kwa maana hiyo sasa yale ma – TV yetu maredio, madubwasha gani ya *analogy* yote yatakuwa hayana maana tena. Sijui kama tumejipanga namna gani, tunaweza tukaya *destroy*, kwa sababu yapo mengi sana. Kama tutafanya sensa kuyahesabu tunaweza tukakamata mikono kichwani kwani ni tishio kubwa. Nilikuwa naomba Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ianze kufikiria vya kufanya kuhusu ma – TV yaliyokuwa hayatotumika tena katika nchi hii.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nilikuwa nataka nizungumze kidogo tu ni suala la UKIMWI. Maradhi haya kwa kweli yanatumalizia nguvu kazi, vijana wetu wengi wanapotea kwa UKIMWI. Nilipokuwa nasoma hichi kitabu cha Mhe. Waziri kaeleza mambo ambayo ndio khasi yale ya kusababisha UKIMWI. Nilipojaribu kuyachungulia upande wa kisheria mambo haya yote yamekatazwa katika nchi hii kufanywa. Bahati mbaya sasa wanaoyafanya wanajulikana na humu ndani ya kitabu wametajwa.

Mhe. Spika, kuna kundi la watumiaji wa daya za kulevya, linajulikana kwa sababu Mhe. Waziri mpaka kawataja humu ndani ya kitabu wamewafika kwa ajili ya kuzungumza nao. Lakini kuna watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja nao pia wanajulikana na kuna wengine wanaofanya mapenzi nje ya ndoa hili ndio kundi kubwa zaidi.

Mhe. Spika, mambo haya yote kwa mujibu wa sheria za nchi hii ni marufuku yasifanywe, hata sheria za Mungu ndio zinakataza zaidi. Sasa watu wanafanya na wanajulikana, yaani wanavunja sheria na wanajulikana kama wanavunja sheria. Mhe. Spika, mimi nashangaa kila siku na nitaendeleea kushangaa na nitaendelea kusema kila siku suala hili. Hivi watu hawa mbona, mtu akiiba makoroma ya nazi anapelekwa Mahakamani halafu anafungwa, lakini mtu anayetumia dawa za kulevya bado hafungwi amapewa ushauri nasaha.

Hakuna watu wabaya kama hawa wanaofanya mapenzi ya jinsia moja wanajulikana na wapo, mbona hawafungwi. Hawa ndio wanaotumalizia nguvu kazi Mhe. Spika. Mimi siungi mkono hata siku moja na nilitaka Mhe. Waziri atupe tathmini tokea walipoanza hii mikakati ya ushauri nasaha *speed* ya kupunguza asilimia ya watu walioathirika na UKIMWI ikoje.

Kwa sababu binaadamu anayo akili, aliyemuumba binaadamu ni Mwenyezi Mungu, kitabu kizima cha Qur-an Mwenyezi Mungu katoa nasaha. Maana kwanza kasema kuiba ni dhambi, haifai, lakini mwisho akasema atakaeiba akatwe mkono, atakae zini apigwe mawe mpaka afe. Sisi tunaendelea kumshauri na mara nyengine tunamshauri, tunampelekea chakula, tunamjengea nyumba *(Soba house).* Mhe. Spika, tusitarajie kama watu hawa watabadilika hawa.

Mimi nilikuwa nasema siku zote hapa kwamba tutungeni Sheria, hapa tuna watu wazuri kweli kweli kwa kupeleleza mambo. Askari polisi tunao, watu wa usalama wa taifa, wanaweza wakapeleleza mpaka wakapata kitu cha ukweli hasa vile kilivyofanyika. Sasa tuweke ndani ya sheria yetu kwamba mtu akipata UKIMWI kwa bahati mbaya basi huyo ndio anatakiwa kupewa huduma, tusimnyanyapae. Maana kuna watu masikini ya Mungu anakaa nyumbani huko, Bwana anatoka linakwenda kumtafutia mashaka anakuja kumuwekea mle ndani. Sasa yule unaweza kumchukua kwa huruma na kumpa ushauri nasaha. Lakini huyu bwana aliyekwenda kufanya mashaka kwa makusudi akayaleta ndani hivyo na yeye pia tumpe ushauri nasaha mpaka lini?

Nilikuwa nafikiri wakati umeshafika katika kukomesha suala hili baya sana tutayarishe jela makusudi za wagonjwa wale waliyoyatafuta kwa makusudi. Sio kila mgonjwa wa UKIMWI apelekwe pale. Wale wanaojulikana kwamba huyu kaupata kwa sababu ya makusudi na makusudi ni vipi? Vile kutoka nje akamuacha mke wake ndani akenda akafanya mapenzi na mtu wa nje, ile ni makusudi. Apelekwe jela maana yake ionekane hasa kama mtu akipata

UKIMWI kwa uzembe basi awe anaadhibiwa katika nchi hii itajengeka hofu kwa watu. Kama ambavyo mtu akiiba akakamatwa akapelekwa jela akafungwa akawa anahadhari kuiba basi na huyu na yeye atafanya hadhari, hii idadi itapungua. Lakini kama tunaendelea kuwanasihi, haya.

Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Abdalla Juma Abdalla, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 28 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi kesho tarehe 28/06/2012 saa 3:00 Asubuhi)